# Sauti ya Kweli Kimataifa

(The Voice of Truth International)

Toleo la 93

Mchapaji (Publisher):
**World Evangelism Team**

Nakala ya Kiswahili (Swahili copy):
**Swahili Gospel Team**

Mawasiliano:

+255 (0) 764 792 979
+255 (0) 784 880 470
+255 (0) 765 098 981

Taarifa (Notice):

Kitabu hiki hakiuzwi, kinatolewa bure na kanisa la Kristo kupitia taasisi ya ***World Evangelism Team (WET).***
This book is not for sale, it is freely given by the church of Christ throuth the institution ***World Evangelism Team (WET).***

## Wafanya kazi:

| | | |
|---|---|---|
| Mhariri | : | Louis Rushmore |
| Mhariri Mshirika | : | Jerry Bates |
| Mhariri Mstaaf | : | Byron Nichols |
| Mhariri Mwanzilishi | : | J.C. Choate |
| Meneja wa Ofisi | : | Paula Bates |

## WAANDISHI

| | |
|---|---|
| George Akpabli | Jack Harriman |
| Felix O. Aniamalu | Parker Henderson |
| Rex Banks | Gordon Hogan |
| Wayne Barrier | Wayne Jackson |
| Paula Bates | Ancil Jenkins |
| Roy Beasley | Jeff Jenkins |
| Mike Benson | John Kachelman, Jr. |
| Ron Bryant | Dayton Keesee |
| Charles Burch | Dalton Key |
| Kyle Butt | Michael L. King |
| Frank Chesser | J. Randal Matheny |
| Betty B. Choate | Cecil May, Jr. |
| Glenn Colley | Wes McAdams |
| Lance Cordle | Colin McKee |
| Sunny David | Stan Mitchell |
| Hans Dederscheck | Kevin L. Moore |
| David Deffenbaugh | Owen D. Olbricht |
| Clarence DeLoach, Jr. | David Pharr |
| Bill Dillon | Neal Pollard |
| Bobby G. Dockery | Mark Posey |
| Hershel Dyer | Steve Reeves |
| Earl Edwards | Martha Rushmore |
| Demar Elam | Rebecca Rushmore |
| Raymond Elliott | David A. Sargent |
| Reuben Emperado | David Tarbet |
| David Everson | J.J. Turner |
| Royce Frederick | Ken Tyler |
| E. Claude Gardner | Allen Webster |
| Gary C. Hampton | R.H. Tex Williams |



# MASHEMASI HUTUMIKA

Louis Rushmore

Mashemasi ni “watumishi” wa kusanyiko la eneo ukiachilia mbali “viongozi” wa kanisa. Badala yake, Mungu ameazimia kwamba makusanyiko ya mahali-mahali ya kanisa la Bwana yaliyoratibiwa vema yanapaswa kuongozwa na “wazee” au “maaskofu”ambao wamechaguliwa kulingana na masharti ya Mungu yaliyoainisha sifa stahiki (1 Timotheo 3:1-7; Tito 1:5-7).

Basi, ni kwa njia tu isiyo rasmi, mashemasi huongoza, ukilinganisha na tofauti za majukumu ambazo Mungu aliagiza majumbani kati ya wanaume na wanawake ndivyo ilivyo kidini – leo, kanisani (1 Wakorintho 11:3; 14:34-35; 1 Timotheo 2:11-14). Kwa hiyo, sifa za “mashemasi” zinawalenga zaidi wanaume badala ya wanawake (1 Timotheo 3:8-13).

Hivyo basi, mashemasi hawana nafasi ya uongozi katika kanisa la Bwana juu ya mwanaume yeyote yule mwaminifu. Mashemasi si “wazee wadogo” na hali ya kuwa shemasi haimaanishi kwamba siku moja atapandishwa cheo na kuwa mzee. Shemasi ni mtumishi, na maamuzi yoyote atakayoyafanya yatazingatia kazi maalum aliyopangiwa na wazee, vilevile kwa ruhusa ya wazee. Ni maamuzi yaliyotarajiwa na ni muhimu kwa ajili ya kazi aliyopangiwa katika kulihudumia kusanyiko. Walakini tunakusudia kuchunguza mambo amabayo Agano Jipya linabainisha kuhusu sifa, uteuzi, kazi na ofisi ya mashemasi.

Neno “shemasi” na “mashemasi” yamejitokeza mara tano katika Biblia (“shemasi,” 1 Timotheo 3:10, 13; “mashemasi,” Wafilipi 1:1; 1 Timotheo 3:8,12).

Maneno mawili yanayofanana ya Kiyunani yaliyotafsiriwa “shemasi” na “mashemasi” kwa pamoja yametajwa mara 67. Katika

Kiyunani *diakonos* limetafsiriwa “mhudumu” (20), “mtumishi” (8) na “shemasi” (3). Kiyunani *diakoneo* limetafsiriwa “kutumika kwa” (15), “tumikia” (10), “mhudumu” (7) mengineyo (5). Fasili ya Kiyunani ya maneno haya mawili inarejea watu yakibainisha shughuli za utumishi. *Diakonos* kwa Kiyunani linamaanisha kutumwa huko na huku, kutekeleza majukumu madogo, mhudumu wa mezani, anayegawa vitu vinavyotakiwa, mfanyakazi wa mtu fulani au msaidizi. *Diakoneo* kwa Kiyunani linamaanisha kutumika, kutunza, na linashirikisha fasili nyingi zenye maana sawa na *diokons.*

Zipo taarifa za kutosha katika Agano Jipya zinazoainisha sifa, uteuzi, kazi na ofisi ya mashemasi. Vifungu vingi vilivyotumia maneno ya Kiyunani wakati mwingine vimetafsiriwa “shemasi” kuelezea kazi ambapo havirejei watumishi hao maalum wanaoitwa mashemasi. Sifa kwa ajili ya watumishi maalum wanaoitwa mashemasi zimetajwa katika 1 Timotheo 3:8-13.

## Mashemasi hutumika

Fasili za lugha za kwanza neno “shemasi” katika Kiingereza “*decon*” linamaanisha **kujishughulisha na kazi**: kutumwa huku na huku, kutekeleza majukumu madogo madogo, mhudumu mezani, mgavi wa vitu vinavyohitajika, mfanyakazi wa mtu fulani, msaidizi, mtumishi au mwenye kutunza vitu. Kwa hiyo, neno “mhudumu” au “mtumishi” au maneno yanayofanana na haya yametumika kuonyesha kazi wanazotenda. *Diakonos* linatofautiana na *doulos* (mtumwa). *Duolos* linakazia uhusiano wa mtu na kiongozi wake wa kazi, wakati *diakonos* linakazia majukumu ya mtu katika kazi zake. Kila ofisi katika kanisa ni ofisi ya uwajibikaji zaidi kuliko hadhi ya heshima. Mhubiri anahubiri! Mwalimu anafundisha! Wazee wanaongoza (Waebrania 13:7, 17) au wanaangalia (Matendo 20:28)! Mashemasi hutumika!

Mashemasi wana kazi za kufanya katika kanisa. Itakuwa hakuna maana na nje na Biblia kwa shemasi kushindwa kutumika katika maeneo fulani maalumu sawa na mhubiri kutohubiri au kwa mwalimu kutofundisha. Asili ya kazi ya shemasi kimsingi inahusu utumishi.

Matumizi mengine ya maneno ya Kiyunani “shemasi” katika Agano Jipya yanabainisha maana ya kibiblia ya “shemasi.” Kumbuka kwamba wakati mwingine neno lililotafsiriwa kama “shemasi” ni matumizi mengine katika Maandiko kama vile mtumishi wa ndani

(Yohana 2:5, 9), mtumishi wa umma (Warumi 13:4), Yesu Kristo kama mhudumu (Warumi 15:8; Wagalatia 2:17), Wakristo tunavyotumikiana sisi kwa sisi (Mathayo 20:26; 23:11), mhudumu wa Injili (Waefeso 3:7;6:21; Wakolosai 1:7, 23, 25;4:7, 1 Wakorintho 3:5; 2 Wakorintho 3:6; 6:4; 11:23; 1 Wathesalonike 3:2; 1 Timotheo 4:6), mhudumu wa kanisa (Warumi 16:1) na watumishi wa mfalme (Mathayo 22:13). [tafsiri ya RSV sisisi ya neno *diakonos* ni "*deaconess*" shemasi mwanamke. Ingawa ni wazi kwamba Fibi alikuwa mhudumu wa pekee wa kanisa, hakuna mwanamke anayekidhi vigezo mahsusi vya kuwa mume 1 Timotheo 3:11.]

## Sifa za Mashemasi

Kuzungumza kweli tupu sifa za kibiblia za mashemasi zimeorodheshwa katika 1 Timotheo 3:8-13 pekee. Anayewania nafasi ya ushemasi anapaswa awe pia "mstahivu" au "mchaji" ambayo ni kwa uzito mkubwa na heshima, mwenye busara na mwenendo inaoheshimika. Asiwe mtu wa "kauli mbili" ambazo ni njia mbili za kutaka kumpendeza mtu wakati huo, anaongea kitu kingine na kumaanisha kitu kingine au kutokuzungumza kwa ufasaha, zaidi sana, shemasi asiwe "mtu wa kutumia mvinyo nyingi" au kujihusisha na pombe au kushawishiwa nayo. Ni makosa kuhitimisha 1 Timotheo 3:3 kwamba wazee wasijihusishe na mvinyo, lakini mashemasi watumie mvinyo kidogo na ya kwamba Wakristo wengine hawana kizuizi juu ya mvinyo. Lakini vifungu hivi na vingine vinakataza matumizi ya mvinyo (yanayojulikana matumizi ya vileo kama burudani katika jamii).

Sifa zinazoendelea kutajwa ni pamoja na "kutotamani fedha ya aibu." Shemasi anapaswa kuwa mtu asiyetafuta mapato ya aibu, ni silika ya mtu ambaye atasimamia fedha kwa uaminifu pia mwenye sifa tofauti na Yuda.(Yohana 12:6). Vilevile, anaweza kutajwa kuwa "mwenye kushika siri ya imani katika dhamiri safi." Hili lina maana ya kwamba shemasi ana uelewa mzuri wa neno la Mungu na anaenenda sawasawa; anatumainiwa kutokana na uadilifu katika utendaji wake Kikristo. Injili imeitwa "siri" (Waefeso 3:3-11) kabla ya kufunuliwa yote. Waandishi wengine wanaielezea kama "dhamiri safi" (1 Petro 3:21; Waebrania 9:14; 10:22).

Kabla hajachaguliwa kuwa shemasi lazima mtu huyo awe "amethibitishwa kwanza" au "kujaribiwa" uzoefu wa kutumika katika

Ukristo, ana historia ya kufanya kazi vizuri kwa ajili ya Yesu Kristo. Kuchaguliwa kuwa shemasi sio cheo kikubwa. Kwa kuongezea, shemasi anapaswa kuwa mtu "asiyelaumiwa," asiyekemewa hadharani, asiyetiliwa mashaka kabisa na asiye na lawama. Wakristo wote wanapaswa kutokulaumiwa (1 Wakorintho 1:8; Wakolosai 1:22).

Anayetaka nafasi ya ushemasi ni mtu aliyeoa, "mume wa mke mmoja." Si mume wa wake wengi. Ni makosa kuhitimisha kutokana na kifungu hiki kwamba mgane aliyeoa au mwanaume aliyetalikiwa hana sifa ya kuwa shemasi. Kifungu kinafundisha kwamba mwanaume atakayekuwa shemasi anapaswa kuwa mwanaume mwenye mke mmoja kwa wakati huo si mume wa wake wawili. Tena hao watakaoteuliwa kuwa mashemasi lazima wajulikane ikiwa "wamewasimamia watoto wao vizuri na nyumba zao," wapate kuongoza vema familia zao ikiwa ni mtoto mmoja au zaidi.

## Watumishi wa Matendo 6:1-7

Moja ya maneno mawili ya Kiyunani yaliyotafsiriwa "shemasi" limetajwa katika vifungu hivi, "kuhudumia mezani" kutoka *diakoneo.* Wanaume katika Matendo 6:1-7 walichaguliwa kuwa wahudumu maalumu wa kanisa la Yerusalemu, ukilinganisha na huduma zingine kwa kawaida zinahusishwa na hizi za mashemasi. Hata hivyo, sifa zilizowafanya wachaguliwe katika Matendo 6 zinatofautiana na sifa za mashemasi katika 1 Timotheo 3:8-13. Hao walitakiwa wawe waaminifu na wenye kujaa Roho Mtakatifu.

Ni dhahiri kutokana na Matendo 6 sifa za wanaume wanaopaswa kuchaguliwa kulihudumia kanisa katika nafasi mahsusi kwamba lazima iwe kwa mujibu wa neno la Mungu. Asili ya kazi ya watumishi maalumu au mashemasi zinalenga kazi za kimwili (bila kujali jambo lingine wanaloweza kulifanya, mfano Filipo alifundisha, alihubiri katika Matendo 8). Kusanyiko linatakiwa kuchagua wanaume miongoni mwao ili watumike.

## Sifa Ndogo za Mashemasi

Ili mwanaume aweze kuwa na sifa za kuchaguliwa kuwa shemasi, mke wake pia anapaswa awe na sifa za kimungu. Mke wa mtu anaweza kuchangia mtu kuwa na sifa au kukosa sifa za kuwa shemasi

anayekubalika kibiblia (1 Timotheo 3:11). Kanuni hii ni kweli pia kwa wahudumu wengine wa kanisa. Mfano wazee na wahubiri kwa kiwango kikubwa wanaweza kukwamishwa katika kazi zao ikiwa wake zao wamethibitika kuwa vikwazo katika kazi zao kwa ajili ya Bwana.

Sifa za wake wa mashemasi watarajiwa ni chache kuliko idadi ya sifa za mashemasi. "Wastahivu" ina maana sawa na ile ya heshima na umakini wa shemasi, mwenye akili timamu na staha. Pia Maandiko yanasema mwanamke "asiwe msengenyaji"; asisengenye. Mke wa shemasi lazima awe na "kiasi" asiwe mlevi, wasiwe wenye kutumia mvinyo nyingi. Mke wa shemasi anapaswa kuwa "mwaminifu katika mambo yote," anayeaminika, sio mfichua siri za watu.

## Hitimisho

Mashemasi wanapaswa kutumika. Mtu hataweza kuwa shemasi mpaka hapo atakapokuwa na sifa zilizoainishwa katika 1 Timotheo 3:8-11. Mke wake pia awe na sifa maalumu zinazohitajika. Mwanaume ni kichwa cha mkewe na watoto wake. Awe na historia ya utendaji mzuri katika Ukristo. Ipo kazi ya yeye kuitekeleza, na aipende na aweze kuitenda.

Thawabu maalum wameahidiwa mashemasi waaminifu 1 Timotheo 3:13 "watendao vema," "daraja zuri" au heshima. Vilevile, mashemasi waaminifu wana "ujasiri" hujiamini au huchangamka moyoni. Roho zote zinazowajibika zinapaswa kujitoe kwa uaminifu, kuhuduma Kikristo, lakini hasa mashemasi lazima wajitahidi sana katika utumishi wa Kikristo.

Moja ya kifungu kinachotumika vibaya katika kuchagua mashemasi ni Wagalatia 3:28, imeandikwa, ***"Hapana Myahudi wala Myunani. Hapana mtumwa wala huru. Hapana mtu mume wala mtu mke. Maana ninyi nyote mmekuwa mmoja katika Kristo Yesu."*** Je, hii inaweza kumfanya mwanamke kuwa shemasi? Aya hii haizungumzii uongozi, inazungumzia haki na usawa katika imani, yani mtu anapoitii Injili na kubatizwa anapata adhi ya kuwa mtoto wa Mungu bila kujali hali yake kulingana na ahadi aliyopewa Ibrahimu (Wagalatia 3:29). Wakati wa uandishi huu kuligubikwa na wingu la ubaguzi wa kijinsia, utaifa na uchumi, haikuwezekana kuyaweka pamoja makundi haya, lakini kwa njia ya Kristo watu hao wameweza kuwa familia moja ambayo ni kanisa lake.



# Mkristo na Malaika

Jerry Bates

Katika ulimwengu wa leo tunasikia habari nyingi sana juu ya malaika, na inaonekana kwamba habari hizo nyingi hazina hasa majibu ya kibiblia. Moja ya sababu ni kwamba Biblia imezungumzia kwa uchache sana habari za malaika. Wametajwa mara chache sana, lakini hakuna fungu maalumu linalofundisha kuhusiana na malaika, na ni machache yanazungumzia kuhusu nafasi yao katika mpango wa Mungu. Tunasikia mada chache kanisani juu ya malaika. Zingatia mawazo yafuatayo kuhusu somo hili.

Kwanza kabisa, tunapaswa kutambua kwamba ni viumbe walioumbwa; kwa hiyo hawafanani na Mungu. Nehemia aliandika, "Ulifanya mbingu, mbingu za mbingu pamoja na jeshi lake lote" (Nehemia 9:6). Jeshi la mbinguni lazima lijumuishe malaika; kwa hiyo, ni viumbe vilivyoumbwa. Pia tunasoma kuhusu wana wa Mungu wakishangilia kwa furaha Mungu alipoweka misingi ya dunia (Ayubu 38:4-7). Wana wa Mungu rejea hii lazima iwe ni malaika kwa kuwa walikuwepo wakati dunia na jeshi lake lote (akiwepo mwanadamu) vikiumbwa. Malaika ni watumishi wa Mungu wenye uwezo wa kutekeleza chochote kile ambacho Mungu huwaagiza wakifanye. Wakati Danieli alipotupwa katika tundu la simba, malaika alivifumba vinywa vya simba (Danieli 6:22). Malaika si wanadamu waliopandishwa hadhi. Hakuna ushahidi wowote unaoonyesha kwamba pindi wana wa Mungu waaminifu wanapokufa wanageuka kuwa malaika.

Lipo kundi kubwa la malaika lisilojulikana. Yesu amesema katika Mathayo 26:53 kwamba angeweza kuita majeshi kumi na mbili ya



malaika ili wamsaidie. Kikosi cha jeshi la Rumi kilikuwa na askari 6,000; hivyo Yesu alisema angeweza kuwaita malaika 72,000. Ilhali idadi hiyo pengine isichukuliwe kihalisia, inaonyesha kwamba kuna idadi kubwa ya malaika humtumikia Mungu. Mwandishi wa Waebrania alisema kwamba Wakristo wameufikilia Yerusalemu wa mbinguni, "na majeshi ya malaika elfu nyingi" (Waebrania 12:22). Katika maono ya Yohana, alisema kwamba malaika waliokizunguka kiti cha enzi cha Mungu idadi yake ni "*elfu kumi mara elfu kumi, na elfu mara elfu*" (Ufunuo 5:11). Ni dhahiri kwamba malaika ni bora kuliko wanadamu, kwa sababu mwandishi wa Waebrania anaandika kwamba Yesu alipofanyika mwanadamu alikuwa "*mdogo kuliko malaika*" (Waebrania 2:7).

Dhana potofu iliyoenea kuhusu malaika ni kwamba ni wanawake wanaoruka kwa mabawa. Hili linawezekana kutokana na ukweli kwamba mara nyingi tunawachukulia wanawake kuwa wema na wenye huruma zaidi kuliko wanaume; hivyo basi, malaika lazima wawe wanawake. Kiukweli malaika ni viumbe wa kiroho, kwa hiyo, hawana jinsia. Yesu alinena habari ya ufufuo katika Mathayo 22:30, "Kwa maana katika kiyama hawaoi wala kuolewa lakini huwa kama malaika wa mbinguni."

Dhana nyingine potofu ni kwamba malaika daima ni wema, lakini hilo pia si sahihi. Baadhi yao hasa hawakuridhika na nafasi zao pamoja na enzi zao, na Mungu ameweka juu yao akiba ya adhabu kuu siku ya hukumu (Yuda 6). Tunaona kuwa hata Shetani ana malaika zake, na jehannamu ya moto imewekwa akiba kwa ajili yao (Mathayo 25:41). Katika Agano la Kale kuna baadhi ya mifano ya malaika wakiwaadhibu wasiotii (2 Samweli 24:15-16; 2 Wafalme 19:35; Hesabu 25:9; Ezekieli 9). Ingawa wana nguvu nyingi, lakini wanadhibitiwa na Mungu. Katika 2 Samweli 24:16 malaika alinyoosha mkono wake kuelekea Yerusalemu ili auangamize, lakini Mungu akanena akasema, "yatosha, sasa ulegeze mkono wako." Paulo aliandika katika 2 Wathesalonike

1:8-9 kwamba Yesu atarudi tena "pamoja na malaika wa uweza wake" na "akiwalipiza kisasi wao wasiomjua Mungu." Mwandishi wa Waebrania alinena ya kwamba Mungu alifanya malaika kuwa watumishi wakitakaswa kwa miali ya moto (Waebrania 1: 7). Hivyobasi, dhana ya kawaida kwa habari ya malaika kwamba ni wema, wenye upendo wakiwasaida tu wanadamu si sahihi kibiblia.

Vilevile malaika wanawapenda watu waliopotea. Malaika mbinguni wanafurahi pindi mwenye dhambi atubupo (Luka 15:10). Yesu alipozaliwa, kundi kubwa la majeshi ya mbinguni lilimsifu Mungu na kusema "*Atukuzwe Mungu juu mbinguni, Na duniani iwe amani kwa watu aliowaridhia*!" (Luka 2:14). Ni kwa uwingi wa upendo kwa ajili ya wokovu wa mwanadamu ungewafanya waseme hivyo. Inaonekana malaika wanafanya kazi kwa ajili ya watoto wa Mungu wanapokufa. Yule maskini alipokufa katika Luka 16:22 malaika wakampeleka kifuani kwa Ibrahimu.

Jambo hili linatupeleka katika uchunguzi wa mwisho. Ni kazi gani na majukumu yapi ya malaika? Wengi wanadhani kwamba kila Mkristo ana malaika anayemlinda. Lengo lake ni kuwalinda Wakristo kwa mambo wanayopitia maishani. Kama hilo lingekuwa sahihi, basi ni dhahiri kwamba hawafanyi kazi yao vizuri sana, kwa maana Wakristo wanapitia kadhia nyingi na ajali za kila namna na mbaya. Hata hivyo, malaika wana kazi wanazofanya kwa ajili ya Wakristo, lakini hatuna uhakika kwamba ni kazi zipi hasa. Malaika walimtumikia Yesu katika matukio makuu katika maisha yake (k.m., majaribu, Mathayo 4:11; bustanini Gethsemane, Luka 22:43). Mwandishi wa Waebrania aliuliza kwa habari ya malaika, "*Je! hao wote si roho watumikao, wakitumwa kuwahudumu wale watakaourithi wokovu*?" (Waebrania 1:14). Tena, Yesu anasema kuhusu watoto wadogo, "*Angalieni msidharau mmojawapo wa wadogo hawa; kwa maana nawaambia ya kwamba malaika wao mbinguni siku zote huutazama uso wa Baba yangu aliye mbinguni*" (Mathayo 18:10). Hivyo tunaweza kusema kwamba malaika wanatoa huduma kwetu kama watoto wa Mungu, lakini hatuwezi kuthibitisha kwa uhakika kuwa ni huduma gani hiyo.

Pia husimama mbele za Mungu na kumwabudu; hata hivyo hawapaswi kusujudiwa na mwanadamu. Mwishoni mwa kitabu cha Ufunuo, Yohana anaanguka na kumsujudia malaika ambaye alimfunulia ujumbe wote uliomo ndani ya kitabu cha Ufunuo. Mara malaika

akamwambia, "*Angalia, usifanye hivi; mimi ni mjoli wako na wa ndugu zako manabii, na wa wale wayashikao maneno ya kitabu hiki. Msujudieni Mungu*" (Ufunuo 22:9). Hivyo tunaona kwamba pamoja na kuwa malaika ni wakuu, ni watumishi hasa wa Mungu, sawa na ilivyo kwetu sisi. Mungu pekee ndiye anayepaswa kuabudiwa.

Ingawa tunaweza kuvutiwa kwa namna fulani na malaika tusiiache kumtumikia Kristo. Tusije tukajaribiwa kuwaabudu malaika au kuutukuza ukuu wao kama vile wamelingana na Mungu. Lakini, hili linapaswa kuwa jambo la kutukumbusha kuwa waangalifu daima, ya kwamba "*Ikiwa Mungu hakuwaachilia malaila waliokosa, bali aliwatupa shimoni, akawatia katika vifungo vya giza, walindwe hata ije hukumu*" (2 Petro 2:4), Ni jinsi gani Mungu atatuadhibu sisi ikiwa tutaishi kinyume na mapenzi yake?

## WANA WA MUNGU

Shadrack S. Msambaza

***"Ikawa wanadamu walipoanza kuzidi usoni pa nchi na wana wa kike walizaliwa kwao, wana wa Mungu waliwaona hao binti za wanadamu ya kuwa ni wazuri; wakajitwalia wake wo wote waliowachagua."*** (Mwanzo 6:1,2). Wana wa Mungu katika kifungu hiki si malaika kama wengine wanavyodhani. Kulingana na muktadha wa sura hii "wana wa Mungu" wanawakirisha "watu wanaomtii Mungu" (Mwanzo 4:26. Yohana 1:12-13). Neno "wanadamu" katika sura hii linawakirisha watu wasiomtii Mungu (Mwanzo 4:16-24).

Yesu alifundisha kuwa malaika hawaoi wala kuolewa, ***"Kwa maana katika kiyama hawaoi wala hawaolewi, bali huwa kama malaika mbinguni."*** (Mathayo 22:30). Malaika ni viumbe wa kiroho (Waebrania 1:14), viumbe vya kiroho havina jinsia kama binadamu hivyo hawawezi kushiriki tendo la ndoa.

Katika Ayubu 1:6; 2:1, neno "wana wa Mungu" lina maanisha "malaika" kulingana na muktadha. Hivyo, uelewa mzuri wa kifungu cha Maandiko hutegemea muktadha wa kifungu husika zaidi ya hapo kuna upotoshaji.




# Fundisho la Ukalvini

J. C. Choate

Mtu mmoja aliyeitwa John Calvin alizaliwa huko Noyon, Ufaransa mwaka 1509 na wazazi waliokuwa Wakatoliki. Alipokuwa mtu mzima Calvin aliongolewa katika Ukatoliki na kuanzisha dhana yake mapya ya wokovu inayoendana na mafundisho yaliyoenea sana huko Ulaya nyakati hizo. Ingawa Calvin mwenyewe hakuanzisha kikundi kingine cha dini tofauti, watu walioyakubali mafundisho yake wakaja kujulikana kama "Wakalvini," pamoja na madhehebu mengi siku hizi huingiza itikadi hizo katika vitabu vya miongozo yao. Akronimu (kifupi) ya msingi wa mfumo wa imani ya Calvin ni T.U.L.I.P. Herufi hizi zinasimamia nini, na ni kwa namna gani mafundisho haya yanalingana na neno la Mungu?

**T** (**Kupotea Kabisa**) hufundisha kwamba wanadamu wote wameharibika kitabia kabisa tangu wanapozaliwa, wamerithi hatia ya dhambi ya Adamu, na ya kwamba haiwezekani kwa mtu yeyote kumchagua yeye binafsi Mungu; Mungu pekee ndiye anayeweza kuwachagua wanadamu watakaookolewa.

- Neno la Mungu:

*"Roho itendayo dhambi ndiyo itakayokufa; mwana hatauchukua uovu wa baba yake, wala baba hatauchukua uovu wa mwanawe, haki yake mwenye haki itakuwa juu yake, na uovu wake mwenye uovu utakuwa juu yake." (Ezekieli 18:20)*

*"Akasema, amini nawaambia msipoongoka na kuwa kama vitoto, hamtaingia kamwe katika ufalme wa mbinguni. Basi, ye yote*

*ajinyenyekeshaye mwenyewe kama mtoto huyu, huyo ndiye aliye mkuu katika ufalme wa mbinguni. Na ye yote atakayempokea mtoto mmoja mfano wa huyu kwa jina langu, anipokea mimi." (Mathayo 18:3-5)*

*"...kila mmoja hujaribiwa na tamaa zake mwenyewe huku akivutwa na kudanganywa. Halafu ile tamaa ikiisha kuchukua mimba huzaa dhambi, na ile dhambi ikiisha kukomaa huzaa mauti." (Yakobo 1:14-15)*

Zaburi 51:5 panasema, *"...mama yangu alinichukua mimba hatiani..."* na kimakosa hufundishwa kwamba mtoto anazaliwa akiwa na dhambi, lakini mwandishi anazungumzia habari ya dhambi za mama yake ambaye ni mtu mzima, wala si dhambi zake mwenyewe.

**U**. (**Uchaguzi bila Masharti**) ikimaanisha kwamba Mungu humchagua yeye atakayeokolewa pia huyo atakayepotea, lakini mtu mwenyewe hana utashi katika jambo hilo; maamuzi ya yeye kuokolewa au kupotea yalitangulia kuwepo kabla, vilevile majaliwa yake hayawezi kubadilishwa.

- Neno la Mungu:

*"Enendeni ulimwenguni mwote mkaihubiri injili kwa kila kiumbe. Aaminiye na kubatizwa ataokoka; asiyeamini atahukumiwa." (Marko 16:15-16)*

*"Njoni kwangu, ninyi nyote msumbukao na wenye kulemewa na mizigo, nami nitawapumzisha." (Mathayo 11:28)*

*"Haya njoni tusemezane, asema Bwana. Dhambi zenu zijapokuwa nyekundu sana, zitakuwa nyeupe kama theluji; zijapokuwa nyekundu kama bendera, zitakuwa kama sufu." (Isaya 1:18)*

*"Basi imani, chanzo chake ni kusikia; na kusikia huja kwa neno la Kristo." (Warumi 10:17)*

*"Kwa maana kwa moyo mtu huamini hata kupata haki, na kwa kinywa hukiri hata kupata wokovu." (Warumi 10:10)*

*"...Namjua yeye niliyemwamini, na kusadiki ya kwamba aweza kukilinda kile nilichokiweka amana kwake hata siku ile." (2Timotheo 1:12)*

*“Nazishuhudia mbingu na nchi juu yenu hivi leo, kuwa nimekuwekea mbele yako uzima na mauti, baraka na laana; basi chagua uzima, ili uwe hai, wewe na uzao wako.” (Kumbukumbu 30:19)*

Kama wanadamu hawana hiari ya kuyakubali mahubiri ya neno la Mungu na mwaliko wake, je Mungu hatakuwa mwongo kuwaalika wote wanaomsikia wamjie yeye?

**L.** (**Neema yenye Mipaka**) hufundisha kwamba Kristo aliwafia hao tu ambao alitangulia kuwachagua kabla kwamba wangeokolewa.

- **Neno la Mungu:**

*“Naye ndiye kipatanisho kwa dhambi zetu; wala si kwa dhambi zetu tu, bali na kwa dhambi za ULIMWENGU WOTE.” (1 Yohana 2:2)*

*“Ambaye hutaka WATU WOTE waokolewe, na kupata kujua yaliyo kweli.” (1 Timotheo 2:4).*

*“Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminie asipotee, bali awe na uzima wa milele.” (Yohana 3:16)*

Mara kadhaa, katika Maandiko, Mungu anasema kwamba upatanisho ni kwa wale wote watakaomwendea.

**I.** (**Neema Isiyozuilika**) ina maana kwamba “waliochaguliwa” hawawezi kufanikiwa kuizuia neema ya Mungu, waliyozawadiwa kwa njia ya Mungu kutangulia kujua kabla kwamba wangeokolewa.

- **Neno la Mungu:**

*“Lakini kwa Israeli asema, Mchana kutwa naliwanyoshea mikono watu wasiotii na wakaidi.” (Warumi 10:21)*

*“Mwayachunguza maandiko, kwa sababu mnadhani kwamba ninyi mna uzima wa milele ndani yake; na hayo ndiyo yanayonishuhudia. Wala hamtaki kuja kwangu mpate kuwa na uzima.” (Yohana 5:39-40).*

Mungu anasema waziwazi kabisa kwamba anamjutia mtu ambaye hatamwendea ili awe na uzima.

**P.** (**Saburi ya Watakatifu**) hufundisha kwamba hao ambao "wamechaguliwa" hawawezi kupotea, na iwapo mtu anaiacha imani, basi huyo hakuokolewa hapo mwanzo.

- **Neno la Mungu:**

  *"Kwa maana wale waliokwisha kuyakimbia machafu ya dunia kwa kumjua Bwana na Mwokozi Yesu Kristo, kama wakinaswa tena na kushindwa, hali yao ya mwisho imekuwa mbaya kuliko ile ya kwanza."*(2 Petro 2:20)

Acha neno la Mungu na liwe kweli, na tuyakatae mafundisho ya wanadamu

*"Kila" [yeyote]* limetokea takribani mara 100 katika Agano Jipya, na katika mistari hiyo mingi *"yeyote"* kwa uhakika na kwa kupaza sauti huelezea bayana uongo wa Ukalvini-TULIP.

***"Na itakuwa kila atakayeliitia jina la Bwana ataokolewa"*** (Matendo 2:21).

***"Huyo manabii wote humshuhudia, ya kwamba kwa jina lake kila amwaminiye atapata ondoleo la dhambi"*** (Matendo 10:43).

***"Kama ilivyoandikwa, tazama, naweka katika Sayuni jiwe likwazalo, na mwamba uangushao; na kila amwaminie hatatahayarika"*** (Warumi 9:33).

***"Kila atakayeliitia jina la Bwana ataokoka"*** (Warumi 10:13).

***"Kila atendaye dhambi afanya uasi, kwa kuwa dhambi ni uasi"*** (1 Yohana 3:4).

***"Kila mtu aaminiye kwamba Yesu ni Kristo amezaliwa na Mungu. Na Kila mtu ampendaye mwenye kuzaa, ampenda hata yeye aliyezaliwa na yeye"*** (1 Yohana 5:1).

***"Kila apitaye cheo, wala asidumu katika mafundisho ya Kristo, yeye hana Mungu. Yeye adumuye katika mafundisho hayo, huyo ana Baba na Mwana pia"*** (2 Yohana 9).

***"Na Roho na Bibi-arusi wasema, Njoo! Naye asikiaye na aseme, Njoo! Naye mwenye kiu na aje; na yeye atakaye, na ayatwae maji ya uzima bure"*** (Ufunuo 22:17).



# Dakika 5 za Kujifunza Biblia

Paula Bates

Mche Bwana

1. Heri kila mtu amchaye Bwana__________ katika njia yake. Zaburi 128:1
2. Na _______ zake hudumu __________hata _________kwa hao wanaomcha. Luka 1:50
3. Petro akafumbua kinywa chake, akasema: hakika natambua ya kuwa ________ hana upendeleo. Bali katika kila ________mtu amchaye na kutenda haki ________ na yeye. Matendo 10:34-35
4. Basi, wapendwa wangu, kama vile mlivyotii siku zote, si wakati mimi nilipokuwapo tu, bali sasa zaidi sana mimi nisipokuwapo, utimizeni wokovu wenu wenyewe kwa _______ na ______. Kwa maana ndiye Mungu atendaye kazi ndani yenu, kutaka kwenu na kutenda kwenu, kwa kulitimiza _______ lake jema. Wafilipi 2:12-13
5. Basi kwa kuwa tunapokea ufalme usioweza _______; na mwe na neema, ambayo kwa hiyo tumtolee Mungu ibada ya kumpendeza, pamoja na _______ na kicho; maana Mungu wetu ni moto ulao. Waebrania 12:28-29
6. Sauti ikatoka katika kile kiti cha enzi ikisema, Msifuni Mungu wetu enyi________ wake wote, ninyi mnaomcha_______ kwa _________. Ufunuo 19:5

Majibu:

1. Aendaye.
2. Rehema, vizazi, vizazi.
3. Mungu, taifa, hukubaliwa
4. Kuogopa, kutetemeka, kusudi.
5. Kutetemeshwa, unyenyekevu.
6. Watumwa, wadogo, wakuu.

# Yaliyomo

## Mungu


Mungu ni mwema!.....................Mwandishi Asiyejulikana……………..…..19
Mungu hutumia taabu…………….Gary C. Hamton……………..…………21
Kristo Muumbaji…………………Keith Kasarjian……………..…………..23
Je, Umemchoka Mungu?................Therman Hodge……………..…………..25


## Ithibati


Je, Ulimwengu utadumu milele?................Kevin L. Moore……………..……..27
Samaki Anayeibuka Papo kwa Papo………David Everson……………….....29


## Neno la Mungu


Kuhuisha Shauku Yetu katika Neno la Mungu………Dan R. Owen ……….31
Neno la Mungu……………………….…. Cecil May, Jr.…………………33
Je, Liko Neno lililotoka kwa Bwana?....................John Gipson……………..35
Kwanini Kuishi kwa kuifuata Biblia?..............Larry Murdock……………...36


## Wokovu


Makundi Matano Siku ya Hukumu………..…E.Claude Gardner…………..…43
Lililopindishwa na Mungu…………………..Denny Petrillo…………..…..48
.baadhi ya Vitu ambavyo Havitakuwepo Siku ya Hukumu.…Neal Pollard…50


## Kanisa


Kanisa la Korintho……………………….Dennis Gulledge………………..53
Kanisa ni Nini?……………………….Dwight Fuqua……………………..55
Ukristo wa Agano Jipya katika Karne ya 21……...Robert Johnson………...57


## Fundisho la Kuliishi


Kuongolewa Kuwa Kitu Gani………...Owen D. Olbricht……………..……..59
Kufanana na Ulimwengu…………………Greg Tidwell…………..………..61
Kuishi Maisha ya Ufufuo………………...Bobby Dockery………..………..62


## Ukristo katika Matendo


Askari, Mwanariadha na Mkulima…………...Glenn Colley……………….…65
.Kuziokoa Roho kwa Kristo………………Dale Grissom……………..……67
Tumeitwa Kuongoza au Kutumika?............Claude Thompson…………….68


## Ibada


Ibada Yenye Maana Hasa……………….Rodney Nulph………..…………70
Je, Utakuwa Wapi?...............................Dalton Key……..…………………72
Amri Kumi kwa ajili ya Kuboresha Ibada…………...……………………73


## Maisha ya Mkristo ya Kila Siku


Safari ya Mbinguni…………………….Wes McAdam…………..…………79
Mtanziko wa Kusikitisha…………..Samwel Matthew……………………..83
Mwanafunzi ni Nani?.......................Donny Weimar……………..………86

## Nyumba ya Kikristo


Mwaminifu Daima…………….David A. Sargen……………………………88
Kuishi kwa Kiasi kwa Ajili ya Kristo…..Martha Lynn Rushmore…………..90
"Ole Wangu Bwana Wangu, Kwani Kiliazimwa!"…Michael L. King……...92


## Uchunguzi wa Vifungu


Mali zenye Thamani……………..Charles Pugh III………………………...95
Mwonekano wa Ubaya……………....T.Pierce Brown…………………..96


## Wahusika katika Biblia


Mwizi Msalabani…………………...Steve Higginbotham……..……………99
Watu waliosahaulika katika Biblia: Yusufu……..…Rebecca Rushmore..…100


## Maswali katika Biblia


Vipi Kuhusu Paulo na Siku ya Sabato?..............Russell G. Bell…………..104
Ibada ya Kweli ni Ipi?............................Ken Tyler…………..…...………106


## Chati na Muhtasari


Mwanzo wa Kuandika Hotuba…………………...Mark N. Posey……..….107


## Historia


Kiangazi (Karibia) Kiishe……………....Patrick Morrison………………..111
Imani ya Mabaki…………………....Rebecca Rushmore………………..113


## Makala, Mashairi na Vijazi


Mashemasi Hutumika………………..………Louis Rushmore…………..03
Mkristo na Malaika…………………..Jerry Bates………………………….08
Fundisho la Ukelvin……………..…J.C.Choate……………………………12
Dakika 5 za Kujifunza Biblia……………..…Paula Bates………………………16
Rubi za Robison……………………………………..……….28, 52, 89, 114
Sarafu za Kenney……………………..…………………………...34, 112
Biblia Kipimo cha Utu……………....Shadrack S. Msambaza…………..….40
Tafuta Aya………………………………Jerry Bates……………………..41
Kanisa lisilo na jina……………………Hugo McCord……....…………56
Maoni ya Haraka katika Aya Muhimu (Law. 10:3)………..………………..64
Je, Unajua?..........................................................................47, 72, 94, 110
Madhumuni ya Ibada Yetu………………Louis Rushmore…………………74
Ucheshi (Mithali 17:22)…………………..……………………………75
Je, Unatathmini Vipi?........................................................................................78
Msaka Tonge…………………...Rebecca Rushmore……………………….98
Ibada za Siku Hizi, Kusifu kusiko Rasmi…….Ernest S. Underwood……...105
Wana wa Mungu………Shadrack S. Msambaza……………………………11

**"Vitu" Vinavyovutia Kidogo!"**
**Lakini moja ni ukakika**

# MUNGU NI MWEMA!

Mwandishi Asiyejulikani



**Hakika hili linavutia – furahia!**

⇨ Pindi MUNGU anapotatua matatizo yetu, tunaamini katika uwezo wake. Pindi Mungu asipotatua matatizo yetu, yeye anaamini katika uwezo wetu.

⇨ Mtu anaweza kuona usahihi wa Mungu katika uanguaji wa mayai – ya hao kurumbiza [ndege] huanguliwa kwa siku 14; hayo ya kuku wa bundani siku 21; mayai ya bata na bukini siku 28; hayo ya bata mwitu siku 35; mayai ya kasuku na ya mbuni huanguliwa kwa siku 42.

**Zingatia, siku hizo zote zinagawanyika kwa saba, idadi ya siku hizo kwa juma!**

⇨ Angalia hekima ya Mungu alivyomuumba tembo. Mnyama huyu mkubwa mwenye miguu minne yote imepinda kwa mbele katika mwelekeo mmoja. Hakuna mnyama mwingine mwenye miguu minne aliyeumbwa hivyo. Mungu alikusudia kwamba mnyama huyu angekuwa na mwili mkubwa – mkubwa sana asingeishi kwa kutegemea

miguu miwili. Kwa sababu hii alimpa miguu minne ili aweze kusimama kwa urahisi toka ardhini. Farasi anasimama toka ardhini kwa kutumia miguu yake ya mbele kwanza. Ng'ombe anasimama ardhini kwa kutumia miguu yake ya nyuma.

**Hekima ya Bwana ni nyingi katika kazi yake yote ya uumbaji!**

⇨ Kila tikiti maji lina idadi ya mistari ni namba shufwa juu ya ganda lake.

⇨ Kila chungwa lina idadi ya pingili namba shufwa. Kila suke la mhindi lina idadi ya mistari namba shufwa. Kila bua la ngano lina idadi ya nafaka namba shufwa.

⇨ Kila mkungu wa ndizi mstari wake wa chini kabisa idadi ya ndizi ni shufwa na kila safu baada ya hiyo inapungua ndizi moja, ili mstari mmoja uwe na namba shufwa na mstari unaofuata uwe na namba witiri.

**Inashangaza! Yapo Mengine Mengi...**

⇨ Mawimbi ya bahari hufika ufukoni mara ishirini na sita kwa dakika katika mazingira yote ya hali ya hewa.

⇨ Nafaka zote hupatikana zikiwa na namba shufwa katika mabua.

⇨ Mungu ameyafanya maua kuchanua muda fulani maalum kwa kipindi cha siku. *Linnaeus*, mtaalam wa mimea, aliwahi kusema kama angekuwa na kibanda cha kukuzia miche chenye udongo unaofaa, unyevunyevu na halijoto rafiki, angeweza kubaini ni wakati gani wa mchana au usiku maua yalichanua na yapi yalijifunga.

⇨ Maisha ya kila mmoja wetu yanaweza kupangwa na Bwana kwa njia bora kwa ajili ya utukufu wake, ikiwa tu tutamtumaini yeye katika maisha yetu. Kama tunajaribu kubuni maisha yetu wenyewe tutakuwa na machafuko na kushindwa tu.

⇨ Mungu pekee aliyeziumba akili na mioyo yetu ndiye anayeweza kuilinda kwa ufanisi hadi mwisho wenye tija.

⇨ Unapoibeba Biblia, Shetani anapata maumivu ya kichwa; unapoifungua, anaanguka, anapokuona unaisoma, anaishiwa nguvu na unaposimama katika Neno la Mungu, Shetani hawezi kukudhuru! Je, ulijua haya pia….

⇨ Maisha bila Yesu ni kama penseli ambayo haijachongwa – haina ncha.

MUNGU

# MUNGU HUTUMIA TAABU

Gary C. Hampton



Paulo, akitambua umuhimu wa kufundisha na kuimarisha zaidi alimwendea Barnaba kwa habari ya kuwatembelea ndugu katika miji yote ambayo awali walihubiri humo. Barnaba aliazimu kumchukua binamu yake Yohana Marko katika safari hiyo. Paulo hakutaka kuambatana na mtu ambaye aliwaacha Perge (Matendo 15:36; 13:13). Paulo na Barnaba walikuwa wenye misimamo thabiti, hata kufikia hatua ya kughadhibika, hivyo walitakiwa kutengana.

Mungu alitumia kutoelewana kwao watu hao muhimu wa imani kutengeneza timu mbili za kuhubiri injili. Barnaba alikwenda pamoja na Yohana Marko huko Kipro, katika nchi yake (Matendo 15:39; 4:39). Paulo alimchukua Sila, mmoja wa ndugu wanaume na viongozi huko Yerusalemu. (Matendo 15:22). Walipita Kipro na Kilikia hadi Galatia ya kusini, wakiyaimarisha makanisa huko (Matendo 15:40-41).

"Jambo la kuzingatia sana katika kisa hiki ambacho vinginevyo kisingefurahisha bali kujutia ni kwamba kila upande wa mzozo huo

haukuruhusu kazi ya Mungu ikwame" (James Burton Coffman, *Ufafanuzi wa Matendo* 305). Paulo baadaye anamtaja Barnaba kama mfano bora wa mtu aliyefanya kazi ya kuhubiri kwa gharama zake mwenyewe. Vilevile anamuelezea Yohana Marko kama mtu aliyefaa kwa huduma (1 Wakorintho 9:6; 2 Timotheo 4:11).

Kutokuelewana kati ya ndugu kunaweza kuwa nyezo ya Shetani lakini kukaleta matendo mema na yaliyosimama. Wakristo wanaoruhusu matukio fulani yanayoumiza sana yawe kigezo cha kutoa visingizio vya kuketi chini na kutofanya chochote wanampatia Shetani ushindi. Yeye anayesonga mbele katika kumtumikia Mfalme anaweza kuona mazingira mabaya yakitimiza malengo ya kueneza injili (Wafilipi 1:12).

Kuna aina mbili za motisha kwa maana ya kuhubiri injili – motisha ya ubinafsi au upendo. Si kazi yetu kuchunguza mioyo huku tukitafuta kurekebisha kila nia iliyo ovu. Badala yake, kama Paulo, tunapaswa kusema, *"Yadhuru nini? Lakini kwa njia zote, ikiwa ni kwa hila, au ikiwa ni kwa kweli, Kristo anahubiriwa, na kwa hiyo nafurahi, naam, nami nitafurahi"* (Wafilipi 1:18).

**Dunia yote na imwogope BWANA;**

**Wote wakaao duniani na wamche.**
**Maana yeye alisema, ikawa;**
**Na yeye aliamuru, ikasimama…**
**Nafsi zetu zinamngoja BWANA;**
**Yeye ndiye msaada wetu na ngao yetu.**
**Maana mioyo yetu itamfurahia,**
**Kwa kuwa tumelitumainia jina lake takatifu.**
**Ee Bwana fadhili zako zikae nasi,**
**Kama vile tulivyokungoja wewe.**

**(Zaburi 33:8,9; 20-22)**

MUNGU

# KRISTO MUUMBAJI

Keith Kasarjian

Binti mdogo pamoja na mama yake walikuwa wakilijadili somo la Biblia katika darasa la watoto la Jumapili jinsi Yesu alivyopaa kwenda mbinguni na kuketi karibu na Baba. Punde mama akaona upinde wa mvua, na hakutaka kupoteza fursa ili kumfundisha habari za Mungu, akamwambia binti yake, "Tazama upinde wa mvua ulivyo mzuri Mungu ameupaka rangi kwa ajili yetu." Binti huyo mdogo alikiri kisha akasema, "Ebu fikiria, aliyafanya yote hayo kwa mkono wake wa kushoto." Mama akiwa amechanganyikiwa akamwuliza, je, Mungu hawezi kutumia mikono yake yote?" Binti akamjibu, "Hapana. Yesu ameketi mkono wake wa kuume!" Binti huyo mdogo alikuwa amepotoshwa kidogo, lakini umewahi kutafakari uwezo wa Yesu wa uumbaji?



**Kristo ndiye Muumbaji wa ulimwengu**. Tunafahamu kwamba "*Katika Yeye vitu vyote viliumbwa*" (Wakolosai 1:16) na kwamba *"Wala pasipo Yeye hakikufanyika chochote kilichofanyika"* (Yohana 1:3). Ukiongezea hapo "*Na vitu vyote hushikana katika Yeye*" (Wakolosai 1:17). Yesu ni Muumbaji na ndiye anayeufanya ulimwengu uendelee kuwepo. **Kristo ndiye Muumbaji wa maisha yetu mapya**. Kwa hili tunamaanisha kwamba yeye ndiye anayefanya maisha mapya yawepo. *"Hata imekuwa mtu akiwa ndani ya Kristo, amekuwa kiumbe kipya; ya kale yamepita tazama! Yamekuwa mpya"* (2 Wakorintho 5:17). Bila Yesu, tumekufa katika dhambi zetu, wenyewe tukitumikia tamaa za mwili na kuwa

watoto wa hasira (Waefeso 2:1-3). Hata hivyo, kwa sababu ya Yesu, maisha yetu yanaweza kuwa tofauti kabisa. Tunamshukuru sana Kristo, tunaweza kuishi maisha mapya yenye hulka ya upendo, furaha, msamaha na matumaini.

**Kristo ndiye Muumbaji aliye na thawabu yetu ya milele.** Yesu amesema kwamba anaandaa makao nyumbani mwa Baba yake na siku moja atatupokea huko (Yohana 14:1-3). Maisha yetu hapa duniani siku zote si mepesi. Wakati mwingine yamejaa taabu, shida na dhiki. Hakika, Yesu alisema maneno yaliyo hapo juu kwa kusudi la kuwafariji wanafunzi wake. Lakini, mbali ya kwamba ulimwengu huu una dhiki zake, tumaini, motisha na thawabu yetu ni mbinguni. Kama tunavyoimba, "Mbinguni kuna makao mazuri sana!" Sawia na mtu mmoja alivyosema, "Ikiwa Yesu anaandaa kwa muda huu wote, patakuwa pazuri sana!"



Yesu Muumbaji! *"Mungu ashukuriwe kwa sababu ya kipawa chake tusichoweza kukisifu kama ipasavyo!"* (2 Wakorintho 9:15).

MUNGU

# Je, Umemchoka Mungu?

Therman Hodge

Kama ilivyokuwa katika siku za Malaki, hata leo shida ni hiyo hiyo ya kwamba watu wengi wanajali sana nafsi ya mtu kuliko kanuni, na kwa sababu ya kutokujua Maandiko, wanaweza kwenda njia yoyote ile. Siku moja *Franklin Camp* alifafanua, "Unapoiacha kanuni na umhimu wa mamlaka ya Biblia safari yako haina mwisho na hauwezi kurejea nyuma."

Je, hatuwezi kuona kuwa hili ni sahihi? Basi masuala ya ibada na maadili msingi wake utakuwa juu ya kile wanachotaka wanadamu badala ya mambo anayoyataka Mungu (Mithali 14:12; Yeremia 10:23; Walawi 10:1-2; 1 Yohana 2:3-5). Watu wa Mungu wamekumbatia dhambi siku hizi na kutaka kukubaliwa na watu wengi pamoja na kutafuta umaarufu ulimwenguni. Waliamua kutoa tamko la amani dhidi ya dini za uongo zilizopo leo hii. Haishangazi basi kuona kwamba watu wa Mungu tayari wameikubali miungu. Si jambo la ajabu, Mungu akiwahoji watu wake, "Je, mmenichoka?"

Tunaona mwendelezo. Ustahimilivu huleta kukubaliwa, kisha kukubaliwa huko humeleta ushirikiano wa pamoja. Rafiki zangu, mambo haya matatu hayajazishusha tu hadhi dini kipindi hiki chote, lakini pia huvuruga masula mazima ya maadili. Hapa tutayataja mawili tu, mapenzi ya jinsia moja na utoaji mimba. Leo hii watu wanapokuwa tayari kuzifuata falsafa za uongo za ulimwengu wanajikuta wakizama katika mmomonyoko wa maadili na upotofu kidini, halafu, haijajitambui bayana kwamba wao pia wamemchoka Mungu (Warumi 1:24-32; Mithali 23:23). Mika, kama Hosea, walikerwa na unafiki wa bibi arusi wa Yehova, Israeli. Aliwahubiri kwa ujasiri. Tunahitaji mahubiri yenye ujasiri wa aina hiyo hata leo (2 Timotheo 4:1-4)!

Je, tunaweza kuona mambo matatu kati ya yale yaliyotokea siku za Mika na siku hizi zetu? Kwa sababu ya ujinga wa neno la Mungu, watu wa Mungu walivutwa na ulimwengu uliowazunguka, pia na dini za uongo za siku na nyakati hizo. Tunakumbuka tamaa zao mbaya kwa kuufuata ulimwengu. Tunasikitika kuona kwamba watu wa Mungu waliridhia kupotosha ukweli ili kutafuta kukubalika. Tabia zao za

uzembe kuhusiana na ukweli ziliwapelekea kuondoka katika ibada ya Mungu.

**Mosi,** mojawapo ya haya ni juu ya mitizamo mibaya katika ibada. Walidhani kwamba wangebadilisha mifumo na mioyo yao isiathirike. **Pili**, walidhani kwamba wangeweza kushika kanuni za dini huku wakipuuza haki. **Tatu**, walidhani wasingedhurika kwa kuingiza baadhi ya vitendo vya ibada kutoka kwa majirani zao, walakini hili lilipelekea kumwacha Mungu pamoja na ukweli katika ibada zao. Hatima ya huko kumwacha Mungu kukawapelekea kuabudu sanamu. Kuondoka hatua chache tu katika ruwaza (kiolezo) ya Mungu kuliwaongoza hadi kwenda umbali mrefu wa ukengeufu.



Vipi kuhusu ibada leo? Je, imegeuka kuwa desturi au mazoea? Je sisi tunashiriki kikamilifu katika ibada au mashuhuda tu? Je, mioyo yetu inasujudu kwa unyenyekevu mbele za Mungu wa kweli aliye hai? Je, mimi bado najali kuhusu kile kilichoamriwa katika ibada (Yohana 9:24; Warumi 1:9; Wakolosai 3:17)? Je, tunatambua ukuu wa Mungu kama ndiye tunayekutana naye na ya kwamba tunapaswa kutoa kile kinachompendeza Mungu? Je, tunahitaji kukumbushwa tena kwamba njia pekee itakayotuwezesha kujua kile kinachompendeza ni hayo yaliyofunuliwa katika Neno lake. Hata sasa swali zuri kwa walio wengi ni. “Je, ummemchoka Mungu?”

HARAKA YA NINI?

Inapotokea mtu anauhitaji wa jambo fulani hutamani kuarakisha mambo yatokee papo hapo. Inapotokea jambo hilo kukawia kulingana na matarajio, wengi hutafuta njia mbadala, mara nyingi njia hizo huwa ni makosa mbele za Mungu. Kusubiri ndio njia ya busara na yenye mafanikio makubwa ingawa haifurahishi.

# Je, Ulimwengu Utadumu Milele?

Kevin L. Moore

Neno “milele” kimsingi linamaanisha “bila kikomo; kudumu daima.” Hata hivyo, neno la Kiebrania “*olam*,” mahali tumepata tafsiri hii lina maana nyingi hivyo basi ni lazima tulielewe kwa kuzingatia mazingira ambamo limetumika. Wakati mwingine linabeba maana moja kama lilivyo neno la Kiingereza (Zaburi 29:10; 45:6). Hata hivyo, mahali pengi lilipotokea, “*olam*” linamaanisha tu kipindi fulani cha muda. Kwa msingi huo, linaweza kumaanisha “siku hata siku” au “kuendelea” kama katika Zaburi 61:8, “*Ndivyo nitakavyoliimbia jina lako daima* [olam], *ili niondoe nadhiri zangu kila siku.”* Linaweza pia kumaanisha “wakati uliopita” kama katika Mwanzo 6:4, “watu hodari zamani [*olam*], watu wenye sifa”… linaweza likatumiak kuonyesha “muda mrefu” kama vile Isaya 42:14 “*siku nyingi* [olam] *nimenyamaza kimya*” … linaweza kuwa na wazo juu ya siku zijazo zisizo na kikomo kama vile Kumbukumbu 23:3, “*wasiingie katika mkutano wa Bwana, wala hata kizazi cha kumi mtu wao asiingie katika mkutano wa Bwana milele”* [olam]… wakati mwingine lina maana “kadri mtu anavyoendelea kuishi,” kama katika 1 Samweli 1:22-28, *“hapo ndipo nitakapomleta, ili ahudhurie mbele za Bwana, akae huko daima”* [*olam*]… *siku zake zote atakazoishi ahudhurie mbele za Bwana”* (*linga*. Kutoka 21:6; Kumbukumbu 15:17; 1 Samweli 27:12).

Neno “*olam*” linapotumika kulinganisha na vitu vya muda mfupi, ni dhahiri linabeba dhana ya jambo ambalo limepangwa kwa muda fulani. Kwa mfano ukuhani wa Kilawi ulipaswa kudumu “***milele***” (Kumbukumbu 18:5), hata hivyo ukuhani ulibadilishwa (Waebrania 7:12). Wazo lilo hilo hupatikana likirejea nchi ya ahadi kwa Israeli pamoja na tohara (Mwanzo 17:7-13; Kutoka 32:13), Pasaka (Kutoka 12:14-17), kinara cha taa katika hema (Kutoka 27:21; Walawi 24:3), suruali za makuhani (Kutoka 28:43), sadaka ya kuinuliwa (Kutoka 29:28), utaratibu wa kunawa (Kutoka 30:21), Sabato (Kutoka 31:17), sadaka ya nafaka na vinywaji (Walawi 6:18-22; Hesabu 15:15), sadaka ya makuhani (Walawi 7:34-36; 10:15), siku Upatanisho ya kila mwaka (Walawi 16:29-34; 23:31), karamu na sadaka ya malimbuko, Pentekoste na vibanda, (Walawi 23:14, 21,41), mikate ya karamu (Walawi 24:8-9),

sauti za tarumbeta (Hesabu 10:8), sadaka ya utakaso (Hesabu 19:10), mawe ya ukumbusho (Yoshua 4:7), urithi wa Kalebu (Yoshua 14:9), Israeli kama wana wa Mungu (2 Samweli 7:24), Hekalu (1 Wafalme 9:3), Yerusalemu (Zaburi 48:8). Kwa kuwa dunia haitadumu daima (Zaburi 102:25-26; Mathayo 24:35; 2 Petro 3:10-12), Biblia inapotaja habari za dunia kudumu daima "*olam*" ("milele"), inamaanisha kwamba itakuwepo kwa muda huo uliokusudiwa kuwepo - hadi Kristo atakaporejea.

**Kevin L. Moore anatumika kama Mkurugenzi wa masomo ya umisheni katika chuo kikuu cha Freed-Hardeman huko Henderson, Marekani.**



## Rubi za Robison

Watu wengi huvutiwa sana na historia ya wapi wametoka, wakitafiti vizazi vyao vya nyuma katika maktaba rekodi za kumbukumbu pamoja na huduma za mitandaoni kadri zitakavyo wasaidia.

Unafahamu kwamba mojawapo ya ushahidi mkubwa wa historia ya asili ya Yesu Kristo ni majina ya vizazi vilivyoorodheshwa kwa mapana katika Biblia? Injili ya Mathayo inasimulia kupitia upande mmoja wa familia yake, na Luka anasimulia kupitia mwingine. Rekodi za Agano la Kale katika kitabu cha Mwanzo na vitabu vya Mambo ya Nyakati vinatoa maelezo mengi zaidi. Kristo si mtu wa kufikirika tu au hadithi zilizobuniwa na watu. Kristo alithibitika bayana kwa kanuni za kawaida za kihistoria.

**Andy Robison ni mhudumu wa kanisa la Kristo Hillview na Mkurugenzi wa Shule ya Mahubiri West Virginia huko Moundsville, West Virginia, Marekani.**

ITHIBATI

# Samaki Anayeibuka Papo Kwa Papo

David Everson

Tia maji kwenye udongo na tope, samaki huyo ataibuka kwa dakika chache kama 10 hivi! Je, hili ni kama tangazo la biashara ya bidhaa mpya ya vyakula vikavu vilivyogandishwa? Hapana! Ni mojawapo ya viumbe visivyo vya kawaida ambavyo Mungu ameviumba. Hebu tujifunze kidogo kuhusu samaki huyu asiye wa kawaida.

Samaki huyo anaitwa Salamanda, anaishi Australia. Samaki huyu urefu wake wapata inchi 2 na anaishi kwenye mabwawa na maziwa yenye kina kifupi. Mara ya kwanza ukimwona anaonekana kama ni samaki wa kawaida, lakini umbile lake lisilo la kawaida halibainiki waziwazi hadi kipindi kirefu cha majira ya joto kinapotokea Australia. Kadri maji yanavyozidi kukauka bwawani samaki hawa hupotea. Hupotea hadi mvua zinaporejea tena, na kwa dakika chache tu, wanaibuka. Samaki huyu anaweza kuishi nje na maji kwa miezi kadhaa hadi majira ya mvua yanapojiri. Samaki anawezaje kuishi nje ya maji kwa miezi mingi hivyo?



Inaonekana kwamba kiumbe huyo wa Mungu wa ajabu amepewa uwezo wa kupumua kupitia ngozi yake. Akiwa katika hali ya kawaida hupumua kama samaki wengine kwa kutumia matamvua yake, kipindi kirefu za ukame, samaki huvuta oksijeni kupitia ngozi yake. Mabwawa yanapoanza kukauka samaki huzama matopeni. Anazama chini kiasi ambacho asikauka kabisa, samaki anaweza kuishi maadamu tu ngozi

yake inapata unyevunyevu. Pengine samaki huyu huwa katika hali ya ubwete (*dormancy*), ambayo hupunguza nguvu za kimetaboliki [ujenzi na uvunjaji wa kemikali mwilini], hivyo anahitaji kiwango kikubwa cha oksijeni. Maji yanaporejea na kuinyeshea ardhi kavu, samaki huyu hujikung'uta toka matopeni bila ya athari yoyote kutokea.



Wanasayansi walivyotafiti juu ya kiumbe hiki cha ajabu wamegundua pia kuwa si tu uwezo wake wa kuishi nje na maji kuwa wa kipekee, vilevile yapo hasa mazingira mengine magumu sana kwa samaki wengine kuishi. Huko Australia nyakati za mchana kwa kawaida, joto katika mabwawa ambamo wanaishi linafikia nyuzi joto 30. Kustahimili kuishi katika kiwango hiki cha joto si jambo la kawaida kwa samaki, na haijabainika wazi ni kwa jinsi gani samaki Salamanda anaweza kustahimili joto. Pia anaweza kuvumulia kiwango kikubwa cha asidi katika mazingira yake, kitu ambacho si cha kawaida pia.

Hivyo, wanasayansi na wanamageuzi wanajaribu kuchunguza ni kwa jinsi gani samaki huyu duni ameweza kuwa na uwezo usio wa kawaida, tutakubaliana na mwandishi wa Zaburi. *"Nitakushukuru kwa kuwa nimeumbwa, kwa jinsi ya ajabu ya kutisha, matendo yako ni ya ajabu, na nafsi yangu yajua sana"* (Zaburi 139:14).

**David Everson ni mzee katika kanisa la Kristo Belington, West Virginia, Marekani.**

# Kuhuisha Shauku Yetu katika Neno la Mungu


Dan R. Owen

Tunajisikiaje juu ya Neno la Mungu? Tunaonaje kuhusu kulisoma, kulitafakari au kusikia likihubiriwa? Je, linakusisimua, haulijali, halieleweki, linakutia hamasa, linakuweka wazi, linakufunga, linakuvutia au linakuchosha? Uhusiano wako na neno la Mungu ni upi? Unalikaribiaje neno katika ibada za halaiki au za kwako binafsi?

Ili kuwa na shauku kubwa kwa habari ya Neno la Mungu sharti pawepo na tabia fulani. Tunapaswa kushukuru jinsi hasa neno lilivyo. Ni pumzi ya Mungu. Ni zao la Roho Mtakatifu. Ujumbe wa Maandiko ni maneno yenye uzima wa milele. Ni maneno ya Mungu yanayotuongoza kuelekea kwa Mungu na wokovuni. Je, hili unalielewa? Tunapaswa pia kushukuru faida maridhawa ambazo Maandiko hutupatia. Neno la Mungu hutuongoza wokovuni, linatuweka mbali na dhambi, linatutia nguvu tunapokuwa na huzuni, ni taa na mwanga wa hatua zetu, linatupatia furaha kwa njia ya ahadi za Mungu, na kutufariji katika dhiki zetu. Kuyafahamu hasa Maandiko jinsi yalivyo pamoja na mambo tunayotunufaisha husaidia kuwa na mtizamo sahihi juu yake.

Ili mtu awe na shauku kubwa juu ya Neno anahitaji ujuzi wa neno. Hatumfurahii mtu hadi tunapopata nafasi ya kumjua vema mtu huyo. Ndivyo ilivyo pia hata kwa neno la Mungu. Lazima tuazimie kulitafuta, hasa kuongeza juhudi katika kulisoma. Fanya hivyo tu, ingawa inakuwa vigumu kwa mara ya kwanza. Kariri mafungu machache muhimu yenye faida kubwa, vilevile rudia mara kwa mara. Yaweke moyoni mwako daima. Elekeza moyo wako katika neno hasa kwa kunuia kuzingatia kinachozungumzwa. Waambie wengine habari hiyo unayosoma na kusikia. Unapokielewa kitu, kiishi kitu hicho katika maisha yako mwenyewe. Mambo haya huleta shauku kubwa juu ya Neno.

Maoni mbalimbali ya utekelezaji wa mambo yanaweza kusaidia. Uwe msikilizaji makini huku ukiwa na Biblia, daftari na kalamu mkononi. Pigia mstari chini na uandike katika Biblia yako. Chukua maelezo. Anza kusoma kitabu kimoja na ukisome kwa mfululizo.



Kwanza soma sehemu uliyoichagua (sura au fungu lolote lile). Halafu, rudia kusoma kwa makini na pigia mstari chini jambo lililokuvutia. Halafu, ingiza mawazo na muhtasari wako katika daftari, yakiwemo mambo ambayo utayafanyia kazi katika maisha yako kutoka fungu husika. Sali kwa ajili ya jambo ulilolisoma, na umwombe Mungu akusaidie ulielewe na kuliishi. Liendee Neno kwa unyenyekevu na weupe wa moyo, huku ukimruhusu Mungu azifinyange akili na moyo wako. Fanya uzoefu wa hotuba kama njia pana ya kulitafakari Neno kila siku. Kwa njia hiyo, utakuwa mtafutaji na mtendaji mkubwa wa Neno badala ya kuwa mtazamaji tu na unayeangaliwa kwa pembeni. Kujaa shauku kubwa juu ya Neno la Mungu ni hiari ambayo kila mmoja wetu anapaswa afanye ili kumpendeza Mungu.

**Dan R. Owen anafanya kazi na kusanyiko la Broadway huko Paducah, Kentucky, Marekani.**

## Tafakari!


**Hivi, inafahamu kwamba unaweza kupotea kama hulijui neno la Mungu hata ingawa unaweza kudhani kuwa upo sehemu sahihi? (Mathayo 22:29).**

# NENO LA MUNGU

Cecil May, Jr

Neno la Mungu ndiyo namna ambayo Mungu anawasiliana pamoja na kutenda. Hapo mwanzo, ***"Mungu alisema na ikawa"*** huelezea kazi yake ya uumbaji (Mwanzo 1- 2). ***"Maana yeye alisema, ikawa; na Yeye aliamuru, ikasimama"*** (Zaburi 33:9).

Yesu aliposhutumiwa "kujifanya kuwa sawa na Mungu" (Yohana 5:18), alijibu si kwa kukataa madai hayo bali kwa kufafanua kuwa alipewa mambo mawili na Baba ayafanye ambayo Mungu pekee ndiye




awezaye kuyafanya: kutoa uzima na kuhukumu (Yohana 5:21-23). Yesu aliyatimiza hayo yote mawili kwa uweza wa Neno lake. Kwa ajili yake kadhalika kwa ajili ya Baba, alitimiza alichoongea. Vitu vikawa kupitia neno lake.

Yesu alisema, *"Amin, amin, nawaambia, saa inakuja, na sasa ipo, wafu watakapoisikia sauti ya Mwana wa Mungu, na wale waisikiao watakuwa hai"* (Yohana 5:25). Alizungumza kuhusu uweza wa neno lake – uweza wa Injili – kuwageuza waliokufa kiroho na kisha kuwapa uzima kiroho.

Alikazia hoja hiyo kwa kuongezea, "*Msistaajabie maneno hayo; maana saa yaja ambayo watu wote waliomo makaburini wataisikia sauti yake. Nao watatoka; wale waliofanya mema kwa ufufuo wa uzima, na wale waliotenda mabaya kwa ufufuo wa hukumu"* (Yohana 5:28-29).

Tunajua uweza wa neno lake wa kufufua wafu. Alimwamuru "Lazaro toka nje," akaurejesha uhai kwa maiti aliyeharibika kisha kumfufua Lazaro toka kaburini. Kama *Marshall Keeble* alivyosema,

"Kama Yesu asingemwita Lazaro kwa jina, kila mfu makaburi hapo angefufuka." Ni Neno la Yesu huyo huyo, ambaye ni Mungu, siku ya mwisho hakika, litamfufua kila aliyewahi kufa atoke katika kaburi lolote lile au katika hali watakayokuwa na kuhuishwa fahamu zao.

Mwanamatengenezo, aliyeongolewa katika ulevi alidhihakiwa na marafiki zake walevi wa zamani, "Je, unasadiki kwamba Yesu aligeuza maji halisi kuwa divai njema huko Kana ya Galilaya?" "Naamini alifanya hivyo." Mmoja akasema "Kwa kuwa Biblia inasema hivyo. Mbali na hilo, nilimwona akigeuza bia, divai na wiski kuwa chakula, samani na nguo nyumbani kwangu." Huo ndio uweza wa Injili hubadilisha maisha siku hizi. Neno la Mungu, Maandiko ni mbegu ambayo inatufanya tuzaliwe upya (1 Petro 1:23), ni mwanga ambao unatuongoza (Zaburi 119:105), ni chakula ambacho tunakula (Waebrania 5:13-14) na ni msingi ambao tunajengwa juu yake (Waefeso 2:20). Linatujenga (Matendo 20:32). Ni ukweli ambao unatutakasa (Yohana 17:17). Ni neno linaloweza kuokoa roho zetu (Yakobo 1:21). Ni kipimo ambacho siku moja ulimwengu wote utahukumiwa (Yohana 12:48).

Usithubutu kulikataa neno la Mungu. Mungu anatenda kupitia neno lake. Lipokee kwa furaha ili uokolewe na kubadilika.

**Cecil May, Jr. ni mkuu mstaafu wa kitivo cha idara ya Biblia katika chuo kikuu huko Montgomery, Alabama, Marekani.**



### Sarafu za Kenney

*"Yeye asiyejua dhambi alimfanya kuwa dhambi kwa ajili yetu, ili sisi tupate kuwa haki ya Mungu katika Yeye"* (2 Wakorintho 5:21.)

Ikiwa umepigwa na bumbuwazi ukitakari kwa nini alifanya hivyo, utakuwa umejiandaa kumwabudu yeye aliyefanya hivyo. Hoja si mambo unayoyapata ibadani. Bali ni kitu gani unakileta mbele za Mungu na kumtolea yeye! Inahuzunisha sana kuona wengine wanaonekana kusahau hili!

# "JE! LIKO NENO LILILOTOKA KWA BWANA?"

John Gipson

Nabii wa Mungu Yeremia alipigwa na kutiwa gerezani ambamo alikaa siku nyingi. Mwishoni, mfalme Zedekia alimwita Yeremia na kumwuliza kwa siri nyumbani kwake. Kitu kimoja ambacho mfalme alitaka kujua ni, "*Je, liko neno lililotoka kwa Bwana*?" Bila kusita Yeremia akajibu "*Lipo*" (Yermia 37:17).

Nyakati fulani, ukiwachunguza wahubiri mbalimbali kwenye luninga, hubainika kwamba wengi wao hawajui hasa kama kuna neno lolote kutoka kwa Bwana au la. Wanaweza kuongoza makundi yao na kusoma kwa sauti mwongozo unaofafanua imani nzima ya Yesu kuzaliwa na bikira na kufufuka kwake kimwili kutoka kwa wafu, alafu wimbo mmoja au mbili baadaye, wanaweza kuhubiri hotuba inayoelezea kwamba Yesu hakuzaliwa na bikira, au lingine kwamba hakufufuka kimwili. Mniwie radhi kama nimechanganya kidogo kuhusiana na matamko na makanusho yao.

Kwa nini mambo ni hivyo, baada ya kusoma mafungu yao mbele ya kusanyiko, baadhi ya wahubiri wanatumia muda wao mwingi kufafanua kwa nini Maandiko hayo hayamaanishi hasa hicho yanachosema? Hotuba inapofikia tamati, ukweli wa neno la Mungu unakuwa umefunikwa na kutobainika wazi hata kuwa vigumu kuelewa.

*Oliver Wendell Holmes* aliwahi kujiuliza ni kitu gani kingetokea kwa wanamahesabu ikiwa mbili ilimaanisha mbili kwake, lakini mbili hiyo ikawa ishirini na mbili kwa mwingine vilevile mia mbili kwa mwingine. Ukizingatia baadhi ya vitu ninavyovisikia kwa jina la Ukristo, nadhani naijua sababu.

Lingekuwa jambo la kupendeza sana kuuliza swali, "*Je! lipo neno litokalo kwa Bwana*?" kisha kusikia jibu, "*Ndio*." Ikiwa namwelewa vizuri mtume Paulo, kazi ya mhubiri ni "kuhubiri Neno."

**John Gipson anafanyakazi na kanisa la Bwana Windsong huko Little Rock, Arkansas, Marekani**

Neno la Mungu

# Kwanini Kuishi kwa Kuifuata Biblia?

Larry Murdock

Sababu gani hasa uifanye Biblia iongoze maisha yako? Kuna wakosoaji wanaobeza watu wanaoishi kwa kuzingatia kanuni zinazopatikana kwenye Biblia. Wakosoaji huwadhihaki wanaoiamini Biblia wakiwaita kwa majina ya kuchukiza, majina kama “wenye itikadi kali ya Biblia,” “wapumbavu” “wajinga” “wanao wahukumu wengine” na labda jina baya zaidi ya yote, “wasiostahimili.” Nilipoamua kuiamini Biblia kuwa kiongozi wa maisha yangu, nimejihatarisha kwa kupachikwa majina hayo. Lakini kwanini nikifanye kitabu cha kale kiongoze maisha yangu? Kwanini wewe pia unapaswa kufanya hivyo?

Watu ambao wanaiamini Biblia kwa dhati kama Neno la Mungu wanapenda kuishi kwa kanuni za Biblia. Watu hawa huziamini kanuni hizo za Biblia zilizowafikia kutoka kwa Mungu. Watu wanapozitenda kanuni za Biblia, wanakuwa vielelezo bora kabisa juu ya tabia ya mwanadamu popote ulimwenguni! Hilo ni kweli! Ndiyo sababu murua ya kufuata mafundisho ya Biblia kwa sababu kanuni hizo ni bora kabisa ulimwenguni tunazotakiwa kuziishi.

Ndugu yake Yesu, Yakobo alisema hivi; ***“Nani aliye na hekima na ufahamu kwenu? Na aonyeshe kazi zake kwa mwenendo wake mzuri katika upole wa hekima. Lakini, mkiwa na wivu wenye uchungu na ugomvi mioyoni mwenu, msijisifu, wala msiseme uongo juu ya kweli. Hekima hiyo siyo ile ishukayo kutoka juu, bali ni ya dunia, ya tabia ya kibinadamu, na Shetani. Maana hapo palipo wivu na ugomvi ndipo palipo machafuko, na kila tendo baya. Lakini hekima itokayo juu, kwanza ni safi, tena ni ya amani, ya upole tayari kusikiliza maneno ya watu, imejaa rehema na matenda mema, haina fitina, haina unafiki. Na tunda la haki hupandwa katika amani na wale wafanyao Amani.”*** (Yakobo 3:13-18).

Haya ni maelezo mazuri sana kwa Mkristo ambaye ameyakabidhi maisha yake kwa Yesu Kristo na kuziishi kanuni zake za kibiblia. Je, hii inamaanisha kwamba kila anayemwaamini Kristo anaishi kwa kufuata kanuni za Kristo? Hapana! Kwa bahati mbaya si kila anayeitwa Mkristo anaamini na kuifuaata Biblia.

Yakobo anatuonyesha kwamba kwa kawaida zipo aina mbili za hekima ulimwenguni. Yakobo anaitaja mojawapo kuwa ni ya kidunia na nyingine ya kimbingu; hekima ya kimbingu inatoka kwa Mungu. Hekima ya kidunia msingi wake ni *kuwa mbele ya wengine* kimaisha. Yote ni kuhusu mimi! Mwenendo wangu unakuwa si wa kiroho badala yake wa kishetani ninapoishi kwa wivu na kutimiza matakwa yangu. Kwa upande mwingine, nikiishi kwa kanuni za kimbingu, hivyo basi kanuni hizo kwanza ni safi. Yaani, kanuni za kimbingu unaziishi bila ya ajenda iliyofichama ndani yako. Badala ya kuingilia mambo ya watu wengine, matendo yangu yatakuwa, "yenye amani, ya upole, tayari kusikiliza maneno ya watu, yenye rehema tele na matunda mema, haina fitina, haina unafiki." Je, wewe hupendi kuwa karibu na mtu mwenye mwenendo huu? Rafiki, kama wewe si Mkristo, lakini unaishi kulingana na kanuni hizo za mbinguni, kwa namna fulani umejifunza kwamba hii ndio njia bora zaidi ya kuishi. Hakika, kwa kuwatendea hivi watu wengine, unaitimiza sheria ya dhahabu ya Yesu kwa kuwatendea wengine vile ungependa wewe utendewe. (Mathayo 7:12).

Mtume wa Yesu, Petro alikuwa na haya ya kuwaambia Wakristo: **"*Wapenzi, nawasihi kama wapitaji na wasafiri, ziepukeni tamaa za mwili zipiganazo na roho. Mwe na mwenendo mzuri kati ya mataifa, ili, iwapo huwasingizia kuwa watenda mabaya, wayatazamapo matendo yenu mazuri, wamtukuze Mungu siku ya kujiliwa. Tiini kila kiamriwacho na watu, kwa ajili ya Bwana; ikiwa ni mfalme, kama mwenye cheo kikubwa; ikiwa ni wakubwa, kama wanaotumwa naye ili kuwalipiza kisasi watenda mabaya na kuwasifu watenda mema. Kwa sababu ndiyo mapenzi ya Mungu, kwamba kwa kutenda mema mzibe vinywa vya ujinga vya watu wapumbavu; kama walio huru, ila wasioutumia uhuru huo kwa kusitiri ubaya, bali kama watumwa wa Mungu. Waheshimuni watu wote. Wapendeni ndugu. Mcheni Mungu. Mpeni heshima mfalme."* (1 Petro 2:11-17).**

Rafiki, ushauri wa Petro ulitoka kwa Bwana Yesu Kristo. Karne ya kwanza Wakristo walikuwa wakibezwa sawa na ilivyo leo. Wakristo waliishi maisha ambayo watu wengi walidhani kuwa ni ujinga kabisa. Lakini, Wakristo hao waliifuata hekima ya mbinguni; kupitia mitume waliovuviwa walipata maelekezo yao kutoka mbinguni! Hilo ni sahihi kabisa! Naam, unapaswa kuifuata Biblia kwa sababu hutuongoza katika njia bora kabisa ya kuishi hapa duniani. Katika sura inayofuata ya barua

yake, Petro aliendelea kutoa hoja za aina moja juu ya jinsi ya kuenenda katika maisha. ***"Neno la mwisho ni hili; mwe na nia moja, wenye kuhurumiana, wenye kupendana kama ndugu, wasikitikivu, wanyenyekevu; watu wasiolipa baya kwa baya, au laumu kwa laumu; bali wenye kubariki; kwa sababu hayo ndiyo mlioitiwa ili mrithi Baraka. Kwa maana,*** [Petro sasa ananukuu katika Biblia yake!] ***atakaye kupenda maisha na kuona siku njema, auzuie ulimi wake usinene mabaya, na midomo yake isiseme hila. Na aache mabaya atende mema; atafute amani aifuate sana. Kwa kuwa macho ya Bwana huwaelekea wenye haki, na masikio yake husikiliza maombi yao; Bali uso wa Bwana ni juu ya watenda mabaya.*** (Zaburi 34:12-16). ***Naye ni nani atakayewadhuru, mkiwa wenye juhudi katika mema? Lakini mjapoteswa kwa sababu ya haki mna heri. Msiogope kutisha kwao, wala msifadhaike; bali mtakaseni Kristo Bwana mioyoni mwenu. Mwe tayari siku zote kumjibu kila mtu awaulizaye habari za tumaini lililo ndani yenu; lakini kwa upole na kwa hofu. Nanyi mwe na dhamiri njema, ili katika neno lile mnalosingiziwa, watahayarishwe wale wautukanao mwenenndo wenu mwema katika Kristo. Maana ni afadhali kuteswa kwa kutenda mema, ikiwa ndio mapenzi ya Mungu, kuliko kwa kutenda mabaya."*** (1 Petro 3:8-17)

Naam rafiki, sababu moja kubwa ya kuishi kwa mujibu wa Biblia ni kwa sababu kuishi kwa kufuata kanuni hizo huleta furaha kubwa duniani pamoja na amani ya moyo.

Hata hivyo, ipo sababu nyingine ya kuishi maisha kwa mujibu wa mafundisho ya Biblia. Sababu hiyo ni rahisi: kuna maisha baada ya haya! Hilo ni sawa kabisa! Kuna maisha baada ya haya ya dunia, na ni zawadi kwa hao wanaomtii Yesu Kristo hapa duniani! Biblia inamwandaa mtu hapa duniani ili apokee **"*urithi miongoni mwao walitakaswa kwa imani*"** (Matendo26:18) katika Yesu Kristo. Yesu alisema ipo thawabu katika ulimwengu ujao. Siku moja Mtume Petro alimwaambia Yesu, ***"Tazama, sisi tumeacha vyote tukakufuata wewe."*** Yesu akasema, ***"Amini, nawaambieni, hakuna mtu aliyeacha nyumba, au ndugu waume, au ndugu wake, au mama, au baba, au watoto au mashamba, kwa ajili yangu na kwa ajili ya injili, ila atapewa mara mia sasa wakati huu, nyumba na ndugu waume, na ndugu wake, na mama, na watoto na mashamba pamoja na udhia; na katika ulimwengu ujao uzima wa milele"*** (Marko 10:28-30).

Chochote anachokiacha mtu kwa ajili ya Kristo na Injili atapokea mara mia hapa duniani. Hata hivyo, kuna kitu kingine ambacho mtu huyo atakipokea katika ulimwengu ujao; mtu huyo atapata "uzima wa milele." Kuishi milele pamoja na Kristo ni ahadi kwao watakaoziishi kanuni za Kristo hapa duniani. Rafiki, kanuni hizo zipo katika Biblia yako, na hasa sehemu ile ya Biblia iitwayo Agano Jipya la Yesu Kristo.

Hakika uzima wa milele ni ahadi kubwa. Rejea zake zimetokea pia katika Agano la Kale. Nabii wa kale Malaki, katika kitabu cha mwisho cha Agano la Kale alikuwa na haya ya kusema; ***"Ndipo wale waliomcha Bwana waliposemezana wao kwa wao. Naye BWANA akasikiliza, akasikia; na kitabu cha ukumbusho kikaandikwa mbele zake, kwa ajili ya hao waliomcha Bwana, na kulitafakari jina lake. Nao watakuwa wangu, asema BWANA wa majeshi, katika siku ile niifanyayo; naam, watakuwa hazina yangu hasa; nami nitawaachilia, kama vile mtu amwachiliavyo mwanawe mwenyewe amtumikiaye. Ndipo mtakaporudi nanyi mtapambanua kati ya wenye haki na waovu, na kati ya yeye amtumikiaye Mungu na yeye asiyemtumikia."*** *(Malaki 3:16-18).*

Mungu anatambua tofauti iliyopo kati ya wenye haki na waovu. Je! wewe unaweza? Biblia ni kitabu kinachoelezea tofauti hizi bayana! Angalia maneno haya kuhusu waovu.

**"*Kwa kiburi chake asiye haki mnyonge anafuatiwa kwa ukali; na wanaswe kwa hila zizo hizo walizoziwaza. Maana mdhalimu hujisifia tamaa ya nafsi yake, na mwenye choyo humkana BWANA na kumdharau. Mdhalimu kwa kiburi cha uso wake asema, hatapatiliza. Jumla ya mawazo yake ni, hakuna Mungu.*** [Mtu mwovu] ***Njia zake ni thabiti kila wakati. Hukumu zako ziko juu asizione, adui zake wote awafyonya. Asema moyoni mwake, sitaondoshwa, kizazi baada ya kizazi sitakuwamo taabuni. Kinywa chake kimejaa laana, na hila na dhuluma.*** [Mtu mwovu] ***chini ya ulimi wake kuna madhara na uovu, hukaa katika maoteo ya vijiji. Mahali pa siri humwua asiye na hatia, macho yake humvizia mtu duni. Huotea faraghani kama simba pangoni. Huotea amkamate mtu mnyonge, akimkokota wavuni mwake. Hujikunyata na kuinama. Watu duni huanguka kwa nguvu zake. Asema moyoni mwake*** [mtu mwovu], ***Mungu amesahau, auficha uso wake haoni kamwe. Bwana uondoke, ee Mungu, uuinue mkono wako usiwasahau wanyonge"*** (Zaburi 10:2-12).

Mungu wa mbinguni hatawasahau wanyonge na wala hatawasahau waovu. Aina mbili tofauti za mitindo ya maisha – falsafa mbili tofauti za maisha! Kuna mtu mkweli, na kuna mtu mwongo. Kuna mkarimu na anayenyang'anya, mwizi. Kuna mbinafsi – anayejali mambo yake mwenyewe, na kuna mtu anayejali wengine. Kuna mtu ambaye ana uchungu na kila fedha anayoipata, na tena yupo mtu anayetoa hadi sarafu yake ya mwisho kwa anayehitaji zaidi kuliko mwenyewe. Kuna mtu atakayekuponda na kuna mtu atakayekunyanyua! Biblia inafundisha, ***"Msitende neno lolote kwa kushindana wala kwa majivuno; bali kwa unyenyekevu, kila mtu na amhesabu mwenziwe kuwa ni bora kuliko nafsi yake. Kila mtu asiangalie mambo yake mwenyewe, bali kila mtu aangalie mambo ya wengine."*** (Wafilipi 2:3-4).

Aina mbili tofauti za mitindo ya maisha – zenye hatima mbili tofauti! Kwa nini usiikubali Biblia kuwa mwongozo wako wa maisha? Yesu na awe nahodha wa wokovu wako! Usiutarajie ulimwengu ujao bila ya yeye. Tembelea kanisa la Kristo lililo karibu nawe mahali ambapo wanaamini na kufundisha kanuni muhimu za Biblia.

**Karry Murdock ni mwandishi, mtayarishaji na mzalishaji wa jumbe za Injili katika redio za ndani na za kimataifa. Ni mhubiri wa kanisa la Kristo la Gandy huko Lawrenceburg, Tennessee, Marekani.**


## Biblia Kipimo cha Utu

Shadrack S. Msambaza

Mtu mmoja aliniuliza, "unataka kusema watu watendao mema wataangamia kwa sababu tu hawakubatizwa?" Kimsingi hili ni swali la walio wengi. Ndiyo, inawezekana kuwapata watu wema bila ya Maandiko, lakini wema huo ni kwa mujibu wa kipimo gani? Bila shaka ni kwa mujibu wa vipimo vya kidunia, utamaduni na mila za jamii husika.

Paulo akivuviwa na Roho Mtakatifu aliandika kuwa ili mtu wa Mungu akamilike na kupata kutenda kila tendo jema anahitaji Maandiko yenye pumzi ya Mungu (2 Timotheo 3:16-17). Ukamilifu ndiyo shabaha kuu, huo hauwezi kupatikana nje ya Neno la Mungu.

# Tafuta Aya



## 1 WAKORINTHO 8:1-13

**Jerry Bates**

1. Ujuzi humfanya nini mtu, vilevile upendo humfanya nini mtu? (8:1)
2. Sanamu inathamani gani? (8:4)
3. Kuna Miungu mingapi ya kweli? (8:6)
4. Kwa habari za Yesu, Paulo alisema, “ambaye kwake vitu vyote____________ kwake, nasi __________ kwake.” (8:6)
5. Paulo anasema dhamira zao ni ______________ hao wanaodhani kuwa ni makosa kula nyama zilizotolewa sadaka kwa sanamu (8:7)
6. Dhamiri zao zitakuwaje watu ambao watakula nyama ambazo wanafikiri hazipaswi kuliwa? (8:7)
7. Je, chakula kinaweza kumfanya mtu ampendeze Mungu Zaidi? (8:8)
8. Ni lazima mtu awe makini, kwa sababu uhuru wa mtu unaweza ____________ wale walio dhaifu. (8:9)
9. Ikiwa mtu awaye yote anadhani ni makosa kula nyama hizo akakuona wewe ukila. Je, ni kitu atajaribu kufanya? (8:10)
10. Ikiwa watakula, ni kitu gani kitawapata? (8:11)
11. Ni kitu gani kitatokea kwa Mkristo ambaye ni imara kiroho atakayekula licha ya kujua kitakachoweza kuwapata ndugu walio dhaifu? (8:12)
12. Paulo alisema kuwa asingefanya nini ikiwa itamfanya ndugu yake akwazike? (8:13)

## Tafuta aya

1 Na kwa habari ya vitu vilivyotolewa sadaka kwa sanamu; Twajua ya kuwa sisi sote tuna ujuzi. Ujuzi huleta majivuno, bali upendo hujenga. 2 Mtu akidhani ya kuwa anajua neno, hajui neno lolote bado, kama impasavyo kujua. 3 Lakini mtu akimpenda Mungu, huyo amejulikana naye.

4 Basi kwa habari ya kuvila vitu vilivyotolea sadaka kwa sanamu, twajua ya kuwa sanamu si kitu katika ulimwengu na ya kuwa hakuna Mungu ila mmoja tu. 5 Kwa maana ijapokuwa wako waitwao miungu, ama mbinguni ama duniani, kama vile walivyo miungu mingi na mabwana wengi. 6 Lakini kwetu sisi, Mungu ni mmoja tu, aliye Baba, ambaye vitu vyote vimetoka kwake, nasi tunaishi kwake, yuko Bwana mmoja Yesu Kristo ambaye kwake vitu vyote vimekuwapo na sisi kwa yeye huyo.

7 Bali ujuzi huu haumo ndani ya watu wote; ila wengine kwa kuizoelea ile sanamu hata sasa hula kana kwamba ni kitu kilichotolewa sadaka kwa sanamu; na dhamiri zao, kwa kuwa dhaifu, hunajisika. 8 Lakini chakula hakituhudhurishi mbele za Mungu; maana tusipokula hatupunguziwi kitu, wala tukila, hatuongezewi kitu.

9 Lakini angalieni huu ujuzi wenu usije ukawakwaza wale walio dhaifu. 10 Kwa maana, mtu akikuona wewe uliye na ujuzi, umeketi chakulani ndani ya hekalu la sanamu, je! dhamiri yake mtu huyo, kwa kuwa yu dhaifu, haitathibitika hata yeye naye ale vitu vilivyotolewa sadaka kwa sanamu? 11 Na yule aliye dhaifu aangamizwa kwa ujuzi wako, naye ni ndugu ambaye, Kristo alikufa kwa ajili yake. 12 Hivyo mkiwatenda dhambi ndugu zenu na kuitia jeraha dhamiri iliyo dhaifu, mnamtenda dhambi Kristo. 13 Kwa hiyo chakula kikimkwaza ndugu yangu, hakika sitakula nyama hata milele, nisije nikamkwaza ndugu yangu.

ANGALIZO: Katika kifungu hiki, Paulo anazungumzia wajibu wetu kwa Wakristo wenzetu. Baadhi ya Wakristo waliamini kwamba kwa kuwa sanamu si kitu, hivyo nyama iliyotolewa sadaka kwa sanamu ilikuwa ni sahihi kuila. Paulo anawataja hao ndugu kuwa imara. Kwa upande mwingine, baadhi walikuwa dhaifu, na waliamini kwamba kama mtu akila nyama iliyotolewa sadaka kwa sanamu, basi kwa namna fulani angeshiriki kuabudu sanamu hiyo, na kwa hiyo angetenda dhambi. Paulo anaonyesha kwamba chakula alichokula mtu hakina uhusiano na masuala ya kiroho ya mtu.

Tatizo hasa halikuwa mtu kula. Badala yake tatizo lilikuwa wale walio imara hawakujali au kuwaonea huruma walio dhaifu. Walionyesha kutokuwa na upendo kwa ndugu zao na kutozingatia kwamba matendo yao yangewafanya ndugu walio dhaifu wakwazike. Ikiwa mtu atainajisi dhamira yake, atakuwa ametenda dhambi. Hata hivyo, Paulo pia alisema ikiwa matendo yetu yatamfanya mwingine kuinajisi dhamira yake, tunakuwa tumemkosea yeye na Kristo, ingawa matendo yetu yanaweza yasiwe makosa. Basi, mtu hatakiwi kujiuliza swali hili pekee “Je, kitendo hiki ni sahihi au ni kosa?” Bali tunapaswa pia kuuliza, “Je, vitendo vyangu vitakuwa na athari gani kwa Mkristo mwenzangu?” Ikiwa kitendo kitamkwaza mtu, basi kwa upendo, hatuna budi kujizuia tusifanye.

# MAKUNDI MATANO SIKU YA HUKUMU

E. Claude Gardner

"Wazo moja madhubuti lililowahi kuingia akilini mwangu ni kwamba nitalazimika kukutana na Mungu katika hukumu" maneno hayo yalisemwa kwa busara na *Daniel Wester,* anayefahamika sana Marekani. Hisia hizo zinapaswa kubainishwa na kila moyo mnyofu. Naam, "Je, atakapoita majina huko juu nami nitakuwepo."

Hukumu ni ya hakika kwa majira yaliyoamuriwa na Mungu. *"Na kama vile watu wanavyowekewa kufa mara moja, na baada ya kufa hukumu"* (Waebrania 9:27). Hakuna mtu atakayeachwa wala asiye na umhimu kuyakwepa yatakayojiri baadaye. Yesu alisema, *"Na mataifa yote watakusanyika mbele zake"* (Mathayo 25:32). Hii itakusanya taifa la Marekani pamoja na ulimwengu mzima. Kila aliye raia atakuwepo, na hakuna hata mmoja atakayekwepa, bila kujali matamanio ya mtu. Paulo alionya, *"Kwa maana imetupasa sisi wote kudhihirishwa mbele ya kiti cha hukumu cha Kristo, ili kila mtu apokee ijara ya mambo aliyoyatenda kwa mwili, kadri alivyotenda, kwamba ni mema au mabaya"* (2 Wakorintho 5:10). Kila mtu atatoa hesabu yake mwenyewe wala si ya mtu mwingine – familia au rafiki. Hakuna atakayetoa hesabu au kumlaumu mume au mke, mama au baba, mwana au binti. Hili litakuja kuwashtua hao ambao waliwategemea wengine kwa karibu asilimia 100 kila wakati.

## Mbinguni na Jehannamu

Yesu alitangaza aina mbili za hatima ya safari: Mbinguni na Jehannamu. Katika hukumu ya watu wote kila mtu aliyewahi kuishi atakuwepo, kisha atawatenganisha wanadamu katika makundi mawili. Alisema ni **nani** na **nini** kitawapata wakati atakaposema, ***"Na hao watakwenda zao kuingia katika adhabu ya milele; bali wenye haki watakwenda katika uzima wa milele"*** (Mathayo 25:46). Mahali pabaya panaonyesha adhabu ya milele na pazuri uzima wa milele na kudumu kwa muda ulio sawa. Jehannamu haitakwisha muda wake. Itadumu muda sawia na muda wa mbinguni, ambao ni "wa milele."

Yesu alifafanua safari ya mwisho kwa kutofautisha njia mbili. Mfano huu dhahiri unatoa maonyo mazito. ***"Ingieni kwa kupitia***

***mlango ulio mwembamba; maana mlango ni mpana, na njia ni pana iendayo upotevuni, nao ni wengi waingiao kwa mlango huo. Bali mlango ni mwembamba, na njia imesonga iendayo uzimani, nao waionao ni wachache"*** (Mathayo 7:13-14).

Hatima hizi mbili, kwa nyakati za mwisho, zinagawa watu makundi matano. Kwa utashi wa kuchagua, mtu anaweza kuchagua ni kundi gani atataka awe [isipokuwa watoto na mtu ambaye hawajibiki daima]. Makundi hayo matano ni watoto, wasio na dini, maprofesa wa dini, washiriki wa kanisa wasio waaminifu na Wakristo waaminifu.

## Watoto Wachanga na Wasiowajibika

Watoto wachanga na hao ambao kiakili hazijapevuka, hawatapotea. Wako salama wala **hawakuokolewa**. Kristo anafaida gani kwao? Kwa njia yake wana uhakika wa ufufuo. *"**Kwa kuwa kama katika Adamu wote wanakufa, kadhalika katika Kristo wote watahuishwa**"* (1 Wakorintho 15:22). Hawana dhambi hivyo hawahitaji msamaha. Hawawezi kurithi dhambi kwa sababu dhambi ni kutendo na wala sio urithi. Yohana alitamka kuwa dhambi ni kutendo. *"Kila atendaye dhambi afanya uasi, kwa kuwa dhambi ni uasi"* (1 Yohana 3:4).

Inatia ukakasi kufikiri kwamba mtoto wamezaliwa na dhambi. Fundisho hili la kurithi dhambi lilifundishwa na mwanamageuzi Mprotestanti maarufu, John Calvin. Aliikuza dhana hii potofu miaka ya 1600, na imezidi kupenyeza katika dini leo hii. *David Hester* anatoa maelezo ya theolojia hii mbaya mno.

John Calvin aliamini kwamba watoto wote wamezaliwa katika dhambi na ya kwamba asili yao inapaswa kugeuzwa. Katika kanuni zake aliandika kwamba watoto, "wanazaliwa na uharibifu toka tumboni mwa mama zao" (kanuni II 1340). "Hakika, asili yao yote ni zao la dhambi: inawezekana kuwa chukizo na karaha kwa Mungu" (Kanuni I, 251). Calvin alieleza kuwa "wanapaswa kuoshwa kabla hawajaingizwa katika ufalme wa Mungu, maana hakuna kitu kichafu au najisi kitakachoingia humo" (Kanuni II, 1340). Alitetea, "dhambi ya asili, basi, hiyo inaonekana kuwa upotofu wa kurithi na uharibifu wa asili yetu" (Kanuni I, 251).

Kama watoto hawawezi "kuamini," hawawezi kubatizwa. Yesu alisema, ***"Aaminiye na kubatizwa ataokoka; asiyeamini atahukumiwa"*** (Marko 16:16).

## Haukuwahi Kukiri Kuwa Mkristo

Watu wengi hawakiri na hawajawahi kukiri kuwa Wakristo. Hali zao zikoje, na makao yao ya milele yatakuwa ni wapi? **"*… na kuwalipa ninyi mteswao raha pamoja na sisi; wakati wa kufunuliwa kwake Bwana Yesu kutoka mbinguni pamoja na malaika wa uweza wake katika mwali wa moto, huku akiwalipiza kisasi wao wasiomjua Mungu na wao wasioitii injili ya Bwana wetu Yesu; watakaoadhibiwa kwa maangamizi ya milele, kutengwa na uso wa Bwana na utukufu wa nguvu zake.* "**(2 Wathesalonike 1:7-9).

Kwa nini hawa hawakubali mafundisho ya Biblia? Pengine hawafikiri kwamba wanapaswa kuitii Biblia. Pengine hawatambui kwamba wanapaswa kuitii injili. Hata hivyo, ni wajibu kwa wanadamu wote. "Watu wote" kila mahali wanapaswa watubu. *"Basi zamani zile za ujinga Mungu alijifanya kama hazioni; bali sasa anawaagiza watu wote wa kila mahali watubu"*(Matendo 17:30).

Kwa nini watu wanapotea? Je, wanapotea kwa kuwa wameikataa injili waliyoisikia? Ni kweli watapotea kwa kukataa kuitii injili lakini sababu ya msingi wanapotea kwa sababu wametenda dhambi. Injili haikutolewa ili watu wapotee. Wanapotea dhambini kwa sababu ni wenye dhambi.

Tunapoiendea "Afrika ya giza" au mataifa mengine yaliyoharibika, si kuwafanya watu wapotee bali ni kurusha "kamba ya Injili," tukitumaini kwamba wataishika. Wako katika hali ya kuzama (kuzama dhambini) ambapo wanahitaji wokovu. Ikiwa mtu anazama, ni kwa sababu yupo katika mazingine ya kuzama. Injili ndio tiba. Hili hujibu swali la kwa nini wapagani wanapotea kadhalika wanahitaji Injili. Wako dhambini pia katika hali ya kuzama. Ni lazima "tuwarushie kamba ya kuokoa maisha."

## Wanaokiri Kuwa Wakristo

Dhana hii ni ya kidini kwa watu wengi wanaodai kuwa Wakristo. Kwa masikitiko, wanaomcha Mungu wengi na wenye nia njema kabisa hawajaitii injili. Wanaweza "kujieleza vinginevyo" mafundisho ya Biblia yanawahimiza watii injili (Marko 16:16; Matendo 2:38; 1 Petro 3:21; Yohana 3:5-7). Yesu alisema watakuwepo watu wa dini watakaodai kutenda mambo kwa jina lake. ***"Si kila mtu aniambiaye, Bwana, Bwana, atakayeingia katika ufalme wa mbinguni; bali ni yeye***

***afanyaye mapenzi ya Baba yangu aliye mbinguni. Wengi wataniambia siku ile, Bwana, Bwana, hatukufanya unabii kwa jina lako, na kwa jina lako kutoa pepo, na kwa jina lako kufanya miujiza mingi? Ndipo nitawaambia dhahiri, sikuwajua ninyi kamwe; ondokeni kwangu, ninyi mtendao maovu!"*** *(Mathayo 7:21-23)*

Alisema, *"**Sikuwajua ninyi kamwe**."* Ni lazima kwamba tunadumu kufundisha Mathayo 7:21. **Sisi si mahakimu**, bali hakimu ni Kristo. *"Yeye anikataaye mimi, asiyeyakubali maneno yangu, anaye amhukumuye; neno hilo nililolinena ndilo litakalomhukumu siku ya mwisho"* (Yohana 12:48).

## Waliowahi Kuwa Wakristo

Kweli wakati fulani waliwahi kuitii injili na kuishi kwa uaminifu kwa muda kitambo. Watu hawa kwa dhati ya moyo walitubu na kwa dhati walimkiri Kristo alafu wakabatizwa. Walifanya kama Paulo alivyosema, *"Lakini Mungu na ashukuriwe, kwa maana mlikuwa watumwa wa dhambi, lakini mliitii kwa mioyo yenu ile namna ya elimu ambayo mliwekwa chini yake"* (Warumi 6:17). Waliacha maungamo yao ya kweli na kurejea katika ulimwengu usio na matumaini. "*Kwa maana wale waliokwisha kuyakimbia machafu ya dunia kwa kumjua Bwana na Mwokozi Yesu Kristo kama wakinaswa tena na kushindwa, hali yao ya mwisho imekuwa mbaya kuliko ile ya kwanza" (2 Petro 2:20).* Mtu anapoanza safari ya Ukristo, ni muhimu kuendelea kufanya kazi kwa ajili ya Bwana. Wengi wanahitaji kurudi na kuhuisha upya viapo vyao vya utiifu kwa Kristo.

Mungu ametoa sheria ya msamaha kwao walioanguka na wasiojali. ***"Bali tukienenda nuruni, kama yeye alivyo katika nuru, twashirikiana sisi kwa sisi, na damu yake Yesu, mwana wake, yatusafisha dhambi yote*"** (1 Yohana 1:7). Inamlazimu mtu kutubu na kuomba. **"*Basi tubia uovu wako huu, ukamwombe Bwana, ili kama yamkini usamehewe fikira hii ya moyo wako"*** *(Matendo 8:22).*

## Waliobaki Mwaaminifu

Hawa ndio wale waliozingatia kielelezo cha wale elfu tatu siku ambayo kanisa lilianza. ***"Basi nyumba yote ya Israeli na wajue yakini ya kwamba Mungu amemfanya Yesu huyo mliyemsulubisha kuwa Bwana na Kristo." Walipoyasikia hayo, wakachomwa mioyo yao,***

***wakamwambia Petro na mitume wengine, "Tutendeje ndugu zetu?" Petro akawaambia, "Tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa jina lake Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu; nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu. Kwa kuwa ahadi hii ni kwa ajili yenu, na kwa watoto wenu, na kwa watu wote walio mbali, na kwa wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie." …wakimsifu Mungu, na kuwapendeza watu wote. Bwana akalizidisha kanisa kila siku kwa wale waliokuwa wakiokolewa."*** (Matendo 2:36-39, 47)

Hawa watasikia Kristo akiwakaribisha kwa furaha siku ya hukumu. *"Kisha mfalme atawaambia wale walioko mkono wake wa kuume, njoni mliobarikiwa na Baba yangu, urithini ufalme mliowekewa tayari tangu kuumbwa kwa ulimwengu"* (Mathayo 25:34).

## Kundi Lipi

Kati ya makundi hayo matano ambayo yatakuwepo siku ya hukumu, inafaa sana kutafakari kuhusaina na kundi gani wewe utakuwa. Na tupate nafasi na kuwa pamoja na Wakristo waaminifu.

**E. Claude Gardner ni Raisi-Mstaafu wa chuo kikuu cha Freed-Hardeman huko Henderson, Tennessee, Marekani.**

# Je, Ulijua?

Rebecca Rushmore

Katika Mwanzo 45:18, Farao alimwaambia Yusufu akawatwaye watu wa nyumbani mwa baba yake. Mwanzo 46:26 tunaambiwa jumla yao ilikuwa watu 66. Nyakati hizo, ilikuwa desturi uwajumuisha katika hesabu wazazi, babu na bibi, watoto walioolewa pamoja na wenzi wao na watoto, watoto ambao hawajaoa au kuolewa, watumishi/watumwa na watoto wao, na mgeni yeyote aliyeishi pamoja na familia kwa kipindi fulani kama sehemu ya watu wa nyumbani.

# Lililopindishwa Na Mungu

Denny Petrillo

"Tafakari vema kazi yake Mungu, *"Kwa sababu ni nani awezaye kukinyosha kitu kile alichokipotosha* [alichokipindisha] *yeye?"* (Muhubiri 7:13). Sulemani anatukumbusha "tutafakari" kazi ya Mungu. Mambo ambayo Mungu aliyafanya katika uumbaji yanafaa kuyatafakari kwa sababu yapo mengi ya kujifunza. Mtu mwenye hekima mara nyingi "hutafakari kazi ya Mungu." Anapofanya hivyo, anabaini ukweli ufuatao.

Kwanza, **vipo vitu ambavyo Mungu amevipotosha** [amevipindisha]. Mungu alipoumba ulimwengu, aliweka baadhi ya kanuni zisizobadilika. Ndege wanahitaji anga, samaki wanahitaji maji. Mwanadamu anahitaji chakula. Vitu hivi ili viendelee kuishi hutegemea hayo. Hata hivyo, inamaanisha nini kwamba "amevipotosha" baadhi ya vitu? Inamaanisha kwamba vipo vipengele fulani katika mpango wa Mungu Mtakatifu ambavyo (amevipindisha) na ni makosa siku zote. Mapema kabisa Sulemani alisema "*Yaliyopotoka hayawezi kunyoshwa, wala yasiyokuwapo hayahesabiki*" (Muhubiri 1:15). Wanadamu wanaweza kuamini kwa ujinga kwamba wana haki au mamlaka ya kubadilisha sheria za Mungu. Hili sio kweli.

Paulo alimwamuru Timotheo kwamba alipaswa "*kulitumia neno la Mungu kwa halali" (*2 Timotheo 2:15). Leo hii watu wa Mungu wanatambua kwamba wanatakiwa kulichunguza neno la Mungu ili kuubaini ukweli wa Mungu wa kiroho usiobadilika-badilika. Katika Warumi 7:7-8 Paulo alisema kwamba hakujua kuwa kutamani ni makosa hadi alipojifunza amri ya Mungu. Mungu alisema kutamani ni "kupindisha." Ni pale tu tunapoitafakari kwa kina Biblia ndipo tunapoyafahamu mambo yote ambayo Mungu ameyapindisha.

Pili, **yapo mambo ambayo mwanadamu anajaribu kuyanyoosha**. Licha ya ukweli kwamba Mungu ameweka bayana sheria za kiroho zisizobadilika, lakini wanadamu kwa ujinga wanajaribu kubadilisha au kuzitengua sheria hizi. Wanafanya hivyo kwa sababu hawapendi kuishi chini ya sheria za Mungu. Yesu alizungumzia habari

za watu hawa. "*Maana kila atendaye mabaya huichukia nuru, wala haji kwenye nuru, matendo yake yasije yakakemewa" (Yohana 3:20).* Unaona, Mungu tayari "ameyafunua wazi" matendo haya. Yamepotoka. Ni maovu. Ni makosa. Bila kujali wanadamu wanaweza kufanya nini, bila kujali ni wangapi wanafanya hivyo – hayo bado ni makosa! Zaidi ya hayo, Mungu hawatazami kwa wema hao wanaojaribu kunyoosha yale yaliyopotoka. Mungu kupitia Isaya alisema, *"Ole wao wasemao kwamba uovu ni wema, na kwamba wema ni uovu"* (Isaya 5:20). Ushoga na utoaji mimba ni makosa, bila kujali wanaosema kuwa hayo ni mema. Ngono kabla ya ndoa ni makosa, hivyo tu! Haijalishi watu wamesema hayo ni mema.

Kwa kuzingatia ukweli kwamba watu wote watakutana na Mungu siku ya hukumu (Ufunuo 20:11-14) na watahukumiwa kulingana na jinsi walivyofuata maelekezo yake, ni vema zaidi tukaa mbali na upindishaji pia masuala ya kunyoosha yaliyopindiswa. Mwenye mamlaka hayo ni Mungu na Mungu pekee. Sulemani aliuliza, "ni nani" awezaye kunyoosha kile kilichopotoshwa? Jibu? Hakuna! Ole wake anayejaribu!

**Denny Petrillo ni Raisi wa Taasisi ya Biblia ya Bear Valley huko Denver, Colorado, Marekani.**

## Kujenga Katika Msingi Imara.

Martha Lynn Rushmore

Unajengaje nyumba? Je, unajenga juu ya mchanga au katika msingi imara? Mpumbavu hujenga nyumba yake juu ya mchanga, mwenye hekima hujenga nyumba yake juu ya mwamba. Tunaambiwa katika Mathayo 7:24-47 tujenge katika msingi imara. Yesu ndiye msingi wetu imara.

Hatuna budi kuyajenga maisha yetu juu ya Yesu na neno lake. Tunapaswa kufuata ruwaza (ramani) ya kibiblia, sawa na mjenzi anavyokuwa na ramani ili kujenga nyumba. Kama mipango haijazingatiwi vema, nyumba haitaonekana murua. Ikiwa hatutazingatia mpango wa wokovu, kusikia (Warumi 10:7), kuamini (Matendo 2:38), kutubu (Luka 13:3-5), kumkiri Kristo (Warumi 10:17) na kubatizwa kwa ajili ya ondoleo la dhambi (Marko 16:16). Hatujajenga juu ya msingi imara wa wokovu. Mwisho, tunapaswa kuwa waaminifu siku zote (Ufunuo 2:10).

Hivyo basi, wewe utajenga juu ya msingi imara wa Bwana wetu Yesu Kristo? Au, ungependa kuyajenga maisha yako juu ya mchanga?

# Baadhi ya Vitu Ambavyo Havitakuwepo Siku ya Hukumu

Neal Pollard

Kiti cha hukumu kitaonekanaje? Kristo ambaye ni Jaji atakuwaje? Je, hukumu tutaishuhudia kwa kuona kwa macho? Ni kitu gani kitakuwepo hapo tofauti na maisha haya? Ni kitu gani kitabadilishwa?

Biblia inanena mara nyingi habari za siku ya kuhesabu, waliokufa wote wenye haki na waovu (Yohana 5:28-29) pamoja na wote walio hai (Mathayo 25:31-33) watasimama mbele za Mfalme wa wafalme kutoa hesabu ya matendo yao waliotenda katika mwili (2 Wakorintho 5:10). Tunapojaribu kuchora taswira katika akili zetu juu ya siku ya hukumu, hatutakiwi kutarajia baadhi ya vitu hapo, kwa sababu havitakuwepo.

**Siku ya hukumu hapatakuwepo na asiyeamini** (Wafilipi 2:10-11). Kwa utambulisho ambao mbingu pekee ndiyo itautoa, Yohana alisema kwamba Yesu atakuja na mawingu, kila jicho litamwona na makabila yote ya dunia wataomboleza kwa ajili yake (Ufunuo 1:7). Hakuna mtu atakayeweza kuendelea kaatika kutoamini kwake. Suala la imani litakuwa historia ya nyuma. Ushuhuda juu ya nguvu za Mungu na kazi za ahadi zake vitakuwa ng’ambo ya pili ya zama za matumaini na katika uwanja wa vinavyoonekana kabisa (Waebrania 11:1). Utani wa kudhihaki mapenzi ya Mungu utafutika mioyoni mwao hao wabaya wenye kubeza. Siku ya hukumu hakutakuwa na wenye kushuku, waagnostiki (wanaodai hatuna habari za kutosha kuhusu Mungu), wenye mashaka, na makafiri.

**Siku ya hukumu hapatakuwa na kumiliki mali** (2 Petro 3:10). Wakaazi wa sayari hii, wanaonekana kujisumbua sana na masuala ya kusaka mali kila siku. Bwana anaviita vitu hivi “viharibikavyo” (1 Petro 1:18) na hazina duni (Mathayo 6:19). Watu wanatafuta mali ili kuwa na maisha yenye furaha, amani na faraja. Tutatoa hesabu ya usimamizi wetu kuhusiana na mali. Tutajibu “ndiyo” au “hapana” tutakapoulizwa iwapo tulimwibia Mungu (Malaki 3:8), lakini hakuna mtu atakayeleta mali zake au utajiri aliojilimbikizia katika mahakama tukufu ya haki.

**Siku ya hukumu hakutakuwa na kesi batili** (Matendo17:31). Kila mmoja wetu atadhihirishwa mbele ya kiti cha hukumu cha Kristo (Warumi 14:10). Kila mmoja wetu "atajibu madai" (2 Wakorintho 5:10). Kristo, ndiye "kweli" pekee (Yohana 8:16), Mhukumu wa wote (Matendo 10:42), atahukumu kwa haki (Matendo 17:31). Mungu amemweka (Warumi 2:16) na yu tayari (1 Petro 4:5). Jaji ataketi kusikiliza madai ya kila mmoja aliyetimamu kiakili aliyewahi kuishi. Yesu atahukumu bila upendeleo (Waefeso 6:9) akitegemea rekodi za mbinguni zenye maelezo yote ya maisha ya mtu (Ufunuo 20: 12). Atahukumu kulingana na "*sheria kamilifu ya uhuru*" (Yakobo 1:25). Hakuna atakayeweza kulalamika kabisa kuwa "anaonewa." Kitabu cha sheria kitakapofungwa na hukumu ya mwisho kutolewa, hakuna mtu atakayeweza kutafuta mwanya au kasoro jinsi kesi zilivyoendeshwa ili achiwe huru au kukata rufaa ya kesi. Hakutakuwa na dosari au uzembe.

**Siku ya hukumu mambo ya siri hayatakuwepo** (Warumi 2:16). Hivi sasa Mungu anajua dhambi za siri za kila mtu (Zaburi 90:8), na atazileta siri hizo hukumuni (Muhubiri 12:14). Mungu huona kila mahali pa siri (Yeremia 23:24). Hufunua siri za ndani kabisa, huyajua yaliyo gizani kabisa (Danieli 2:22). Siku ya hukumu, mambo kama hayo yatahukumiwa (Warumi 2:16). *"...lakini vitu vyote vi utupu na kufunuliwa machoni pake yeye aliye na mambo yetu"* (Waebrania 4:13b).

**Siku ya hukumu hakutakuwa na eneo la kubatizia**. Watu wengi wataingia katika umilele bila ya kuoshwa, kutakaswa na kuhesabiwa haki (1 Wakorintho 6:11). Kama Kristo anapozibagua kondoo na mbuzi, atanufaika mtu yule aliyeitii injili kikamilifu (1 Petro 3:21; Warumi 6:3-4; Wakolosai 2:12; Matendo 2:28; Wagalatia 22:16; Marko 16:16). Pengine watu watapasa sauti wakiomba mtu mwingine awabatize. Hofu kubwa itawapata wengi ambao waliisogeza mbele tarehe ya kubatizwa wataikumbuka watakaposimama mbele ya Kristo bila ya damu yake ifunikayo dhambi zao.

**Siku ya hukumu hapatakuwa na wimbo wa mwaliko**. Tarumbeta itakapolia, hakuna hotuba itakayohubiriwa kuwashawishi waliopotea kuitii injili. Hapatakuwa na suala la kuwasihi walio vuguvugu na Wakristo wasio waaminifu. Hakuna mwimbishaji atakayesimama mbele ya umati huo usiohesabika kuwasihi waliopotea na walioanguka. Mioyo ya majeshi itayeyushwa kwa nguvu za Mungu.

Hofu nyingi itawajaa wale wasio tayari kukutana na Yesu. Pengine wengi watalia kwa sauti kuu ili wapewe nafasi nyingine, lakini fursa ya mwisho ilishapita.

Atakuwepo Mhukumu wa haki ambaye atamhukumu kila mtu kwa haki. Kila mtu atatoa hesabu. Hukumu ya milele itatolewa kwa kuzingatia maisha ya mtu alivyoipokea au kuikataa dhabihu ya Kristo. Hapatatolewa msamaha wa kuachiwa huru, kusubiri adhabu au msamaha kwa waliopotea. Sisi sote tunahitaji neema nyingi ili tuweze kusimama mkono wake wa kuume, lakini Maandiko yanatueleza jinsi gani neema imetufikia. Hatuna budi kujiandaa kwa hilo katika maisha haya (Waebrania 9:27).

**Neal Pollard ni mhubiri wa kanisa la Kristo Bear Valley huko Denver, Colorado, Marekani.**

## Rubi za Rubison




Limekuwa ni tatizo la kudumu kwamba jamii inaweza kuyageuza mambo yakawa shaghala-baghala. Hata watu wa Mungu walitenda hivyo. Walifikia pahali ambapo walitoa watoto wachanga dhabihu siku za Yeremia. Katika siku za Isaya takribani miaka 700 kabla ya Kristo, Isaya alisema, *"Ole wao wasemao kwamba uovu ni wema, na kwamba wema ni uovu; watiao giza badala ya nuru, na nuru badala ya giza; watiao uchungu badala ya utamu, na utamu badala ya uchungu!"* (Isaya 5:20). Wakati mwingine tunashindwa kuelewa jinsi mwanadamu anavyozama katika lindi la uharibifu na kusahau kanuni za utauwa. Wewe unafikiri nini? Je! sisi tunaishi zama ambazo uovu unagezwa kuwa wema, na wema kuwa uovu?

**Andy Robison ni mtumishi wa Kanisa la Kristo Hillview Terrace na Mkurugenzi wa Shule ya Mahubiri West Virginia huko Moundsville, West Virginia, Marekani.**

# Kanisa la Korintho

Dennis Gulledge

Kanisa lililokuwa Korintho lilianza sawa kabisa na jinsi ambayo makanisa ya Kristo yanavyoanza. Matendo 18:8 panasema, "***Na Krispo, mkuu wa sinagogi, akamwamini Bwana pamoja na nyumba yake yote, Wakorintho wengi waliposikia, waliamini, wakabatizwa***." Tunajifunza nini? Tunaitambua hadhira – wenyeji wa mji wa Korintho. Tunajua hatua walizopitia kukutana na injili – "walisikia" (Warumi 10:17). Tunajua jinsi walivyopokea ujumbe - "walibatizwa" (Marko 16:15-16). Tunajua matokeo yake: Wakristo hao walikusanyika katika mji wa Korintho, hivyo wakawa "kanisa la Mungu" (1 Wakorintho 1:2). "Waliitwa [na injili] (2 Wathesalonike 2:14) kuwa watakatifu" (1Wakorintho 1:2). Walipoka neema ya Mungu kwa njia ya Yesu Kristo (1 Wakorintho 1:4). Waliingia katika ushirika na Yesu Kristo (1 Wakorintho 1:9).




Je, mambo haya yote yanamaanisha kuwa kanisa la Korintho lilikuwa kamilifu? La hasha! Sawa na baadhi ya makusanyiko leo, kanisa la Korintho lilikuwa na matatizo mengi. Walikuwa na matatizo

kiasi kwamba tunabaki tukishangaa kwa nini Paulo na Bwana waliwavumilia. Paulo kama mtumishi na mtume aliwapenda, na alitafuta namna ya kutatua matatizo yao. Kuhubiri injili hakuepushi matatizo ya kanisa, lakini hutoa utatuzi wa Biblia (2 Timotheo 4:2).

Hakika baadhi ya wahubiri hupenda kukazia zaidi matatizo yaliyolikabili kanisa la Korintho. Kinyume na hoja ya matengenezo kabisa inayohoji "Ni kanisa lipi tunalotaka kulirejesha? Je, kanisa la Yerusalemu na ubaguzi wake dhidi ya watu wa Mataifa? Je, kanisa la Korintho pamoja na matatizo yake?" Mtazamo huu maarufu una maana kwamba urejeshaji hauwezekani kuwepo kama washirika wa kanisa hawajapevuka kiroho kama wanavyopaswa kuwa. Baadhi ya wahubiri wanaonekana kuliangalia kanisa la Korintho kuwa mfano wa kusanyiko la kisasa linalolegeza masharti lenye mafundisho yake na vitendo tofauti. Mtizamo wao ni kwamba ikiwa tutachukuliana na kanisa la Korintho, mbali ya tofauti kubwa za imani na vitendo vyao, bila shaka tunaweza kushirikiana na chochote ambacho baadhi ya ndugu wanachofundisha au kukitenda leo.

Kuna sababu kuu mbili kwa nini makanisa yana matatizo. Kwanza, kanisa linaundwa na watu wenye ngazi tofauti za ukuaji kiroho. Wengine ni watoto (1 Wakorintho 3:1-3). Wengine ni watu wazima. Uwezekano wa kuanguka upo kwa wote (1 Wakorintho 10:12). Kutokukua kiroho kunatoa mwanya kwa mafundisho ya uongo kupata nafasi makanisani (Warumi 16:17-18).

Pili, kanisa limekuwepo katika mazingira ya ulimwengu unaolichukia (1 Wakorintho 6:9-10). Kama lilivyokuwa Korintho, kanisa lilikuwa duniani, kama lilivyopaswa kuwa, lakini ulimwengu pia ulihamia kanisani ingawa halikupaswa kuwa hivyo (1 Wakorintho 5:9-10). Pengine Korintho linakaribia kufanana na hali zetu sasa kuliko kanisa lingine lolote katika Agano Jipya.

Utafiti wa kanisa la Korintho ni muhimu kwa sababu ya matatizo yao na majibu aliyoyaainisha Paulo. Wakorintho wa Kwanza kiliandikwa kwa faida ya kanisa la Korintho na "***pamoja na wote wanaoliitia jina la Bwana wetu Yesu Kristo***" (1 Wakorintho 1:2). Yaani, mafunzo kutoka kanisa la Korintho yana umhimu kwetu leo.

**Dennis Gulledge ni mhubiri wa kanisa la Kristo huko Mabelvale, Arkansas, Marekani.**

# Kanisa Ni Nini?

Dwight Fuqua

"***Nami nakuambia, wewe ndiwe Petro, na juu ya mwamba huu nitalijenga kanisa langu; wala milango ya kuzimu haitalishinda***" (Mathayo 16:18). Neno "kanisa" limetokea zaidi ya mara 100 katika Agano Jipya. Limetajwa kwa njia iliyo wazi hata halina ugumu wa kulielewa.

Neno "***kanisa***" (ekklesia katika Kiyunani) lina maana "walioitwa." Kanisa linaundwa na watu walioitwa na injili watoke ulimwenguni (2 Wathesalonike 2:14). "***Akatuhamisha na kutuingiza katika ufalme wa Mwana wa pendo lake***" (Wakolosai 1:13-14). Wale "*Waliotakaswa*" au watakatifu kwa Mungu (1 Wakorintho 1:2).

Kanisa linaundwa na watu waliookolewa. Mungu anawazidishwa waliookolewa katika kanisa (Matendo 2:47). Unaonaje mabishano ya kwamba mtu anaweza kuokolewa nje na kanisa? Ni la kulibeza hilo! Kanisa ni hao waliookolewa! Mabishano haya ni njia tu kudhihirisha kiwango kikubwa cha kushindwa kuelewa habari za kanisa moja lililopo.

Katika Agano Jipya, neno "kanisa" halijawahi kurejea madhehebu. Kwa nini? Kwanza, kwa sababu kanisa la Bwana lilikuwepo miaka mingi sana kabla ya madhehebu kuibuka. Pili, kwa sababu mtu anaweza (na ndivyo anavyotakiwa) kuwa mshiriki wa kanisa la Bwana bila ya kuwa mshiriki wa madhehebu.

Kumbuka pia kwamba neno "kanisa" halijawahi kutajwa katika Agano Jipya likimaanisha jengo. Wanadamu wanaweza kujenga nyumba za mikutano, lakini Kristo alijenga kanisa (Mathayo 16:18). Kanisa ni nyumba ya kiroho Wakristo ndio matofali (1 Petro 2:5).

Ni kwa njia gani mtu anafanyika mshiriki wa kanisa la Kristo? Siku ya Pentekoste watu walioisikia na kuiamini injili, waliuliza na kutaka kujua mambo ya kufanya ili waokoke (Matendo 2:37). Waliambiwa watubu na kubatizwa **wapate** ondoleo la dhambi (Matendo 2:38). Walipotii mapenzi ya Mungu, walisamehewa dhambi zao na Bwana aliwazidisha katika kanisa lake (Matendo 2:47).

Je, unataka kuwa mshiriki wa kanisa la Bwana? Unaweza kuwa mshiriki wa kanisa leo kwa njia ile ile ambayo waume kwa wake walifanya miaka elfu mbili iliyopita!

**Dwight Fuqua ni mhubiri wa kusanyiko la Findlay huko Sparta, Tennessee, Marekani.**

# Kanisa Lisilo Na Jina

Hugo McCord

Makanisa mengi yana majina maalumu, lakini kanisa la Agano Jipya halina jina. Madhehebu yana majina mahususi. Neno la Kiingereza "*denominate*" lina maana kukipa kitu "jina." Kanisa la Agano Jipya linaitwa nyumba ya Bwana, familia ya Mungu, mwili wa Kristo na ufalme wa Kristo (Wagalatia 6:10; Waefeso 1:22-23; Wakolosai 1:13; Waebrania 3:5-6; 1 Timotheo 3:15), lakini halina jina moja mahususi.

Washiriki wa kanisa la Agano Jipya wana jina mahususi. Jina lao mahususi si "mwanafunzi," ingawa ni mwanafunzi (Matendo 9:1). Jina lao si "ndugu" ingawa wao ni ndugu (Matendo 9:30). Jina lao si "watakatifu" ingawa ni watakatifu (Matendo 9:32). Jina lao mahususi walilopewa kutoka mbinguni ni "Wakristo" (Matendo 11:26; 1 Petro 4:16), lakini kuliita kanisa "kanisa la Wakristo" ni kuigawa taasisi hiyo kubwa.

Ni sahihi kulitaja kanisa la Agano Jipya kama "Kanisa la Kristo" sawasawa na kusema "kanisa la Mungu" (Warumi 16:16; 1 Wakorintho 1:2), hakuna kati ya hayo lililo jina maalumu. Kusema makusanyiko ya "kanisa la Kristo," wahubiri wa "kanisa la Kristo" ni kulipa jina maalumu kanisa hilo. Kanisa la Agano Jipya halina jina maalumu.

**Hugo McCord (1911-2004) alikuwa ni Profesa wa Biblia katika chuo kikuu cha Kikristo cha Oklahoma huko Edmond, Oklahoma, Marekani.**

# Ukristo Wa Agano Jipya Katika Karne ya 21

Robert Johnson



Miaka ya hivi karibuni, tumeona makundi kadhaa ya kidini yakipuuza mafundisho ya umoja katika ushirika na mipango. Katika jamii inayoepuka maneno au matendo ya kukwaza wengine, ambapo kukubaliwa na watu ndio jambo la msingi, mafundisho hayana maana tena kwa watu wengi. Kiukweli, mhubiri mmoja maarufu wa kimadhehebu alililisema hili waziwazi; "Masuala ya mafundisho yanapaswa kusahaulika na kuwekwa nyuma." Kwa wengi, mambo ya msingi zaidi ni kumkubali Mungu kuwa Baba na Yesu kuwa Mwana wa Mungu; kwao kitu kingine chochote ni cha ziada tu na cha hiari.

Haya yote ni sahihi kwa madhehebu ambayo hawatambui tena mamlaka ya Maandiko kwa namna yoyote ile. Hata hivyo, kanisa la Bwana halitashiriki katika hayo, ikiwa litashikilia ukweli wa wito wake. Ni dhahiri Yuda amesema kwamba tunatakiwa "***Tuishindanie Imani walioyokabidhiwa watakatifu mara moja tu***" (Yuda 1:3). Kuna imani moja tu ambayo Mungu ameikabidhi, ambayo inatuongoza wokovuni (Waefesoo 4:5), sio imani nyingi tofauti. Kuiacha imani hiyo ni kupotosha Injili ya Kristo na kuiteketeza kazi ya Mungu aliyoikamilisha kwa injili hiyo (Wagalatia 1:6-9). Yeye Mungu anataka utiifu wa mapenzi yake kwa njia ya imani aliyoyafunua kwetu (Mathayo 7:21-23).

Ili kuwa mkweli, pia mwaminifu, mafundisho ya kimadhehebu hayatokani na Mungu. Bali ni ya kibinadamu, hakuna hata moja

linalomtukuza Mungu. Lipo kanisa moja tu (Waefeso 1:22-23; 4:4). Ingawa tunaweza kuwa na sifa fulani zinazofanana na madhehebu, Kanisa la Bwana si madhehebu, bali kanisa lilinunuliwa kwa damu ya Kristo, ambalo pekee ndilo "nguzo na msingi wa kweli" (1 Timotheo 3:15). Wajibu wetu si kuungana nao, bali kuwaleta katika maarifa ya kweli, imani katika kweli na utiifu katika kweli, ili kwamba Mungu awazidishe katika kanisa lake la kweli. Huu ndio upekee kuhusu kanisa la Agano Jipya. Si ubunifu na utashi wa mwanadamu, bali lile lililoanzishwa na Mungu kupitia Kristo (Mathayo 16:18), likafunuliwa katika Maandiko na kujulikana kwa kutii mamlaka ya Mungu.

Mhubiri mmoja maarufu katika ndugu aliniambia miaka mingi iliyopita, "kanisa la Kristo litakuwa madhehebu ya mwisho! Kwa hilo, alikuwa akisikitikia kutokuwepo ushirika wetu katika ulimwengu wa madhehebu. Nitasahihisha mawazo yake kwa kusema, "Kanisa la Kristo pekee ndilo kanisa lake, halitalegeza ukweli wake na kuwa madhehebu." Kama tunafuata mafundisho ya Kristo yaliyofunuliwa katika Maandiko, tutalingana na jinsi tunavyosema, Kanisa la Kristo, na tukidumu kuwa waaminifu katika wito huu, tunaweza kujihakikishia wokovu tulioushikilia imara. Kama Petro alivyohimiza, sisi nasi tunahimiza, "***Mtu akisema, na aseme kama mausia ya Mungu***" (1 Petro 4:11).



**Robert Johnson ni mhubiri katika kanisa la Bwana huko Longview, Texas, Marekani.**

# Kuongolewa Kuwa Kitu Gani?

Owen D. Olbricht

Tunapaswa kuwaongoa wengine waweje au wamfuate nani? Yesu aliwashutumu watoza ushuru na Mafarisayo kwa sababu wongofu wao ulikuwa mbaya zaidi kuliko kabla ya kuongolewa na kuwa Wayahudi (Mathayo 23:15). Walikuwa wakiwaongoa kuwa wafuasi wazuri wa mapokeo ya Kiyahudi badala ya kuwa watumishi wa Mungu.

## Uongofu Mbaya

"Ongoka" limetafsiriwa kutoka *epistrepho*, neno lenye maana ya "rejea." Petro na Paulo waliwaambia watu kwamba walipaswa kutubu na "kurejea" (Matendo 3:19; 26:20).

Msingi mbaya wa uongofu unaweza kujumuisha kuwaongoa katika mtizamo fulani wa mafundisho, wa kanisa, wa mhubiri au mambo mengine kadha wa kadha. Watu wanaweza kuvutiwa na haya, lakini hayatakiwi kuwa msingi wa uongofu.

Uongofu katika jambo fulani ambalo ni la pili kwa uzito si kosa, lakini ni kosa ikiwa ndio msingi pekee wa kuongoka na huanza kabla ya lile la msingi. Vivutio vinginevyo vitafungua mlango wa fursa ili kufundisha jambo muhimu, lakini kutii jambo hilo la kwanza sharti kuwe ndio msingi wa uongofu.

## Msingi wa Kwanza

Yesu na kanisa la awali walifundisha kwamba lengo la kwanza kwa wafuasi wa Yesu ni kuwaleta watu kwa Yesu. Ikiwa watu wataongolewa kwake kama Bwana na Kristo, basi matokeo yake yatakuwa kumtii yeye kama Bwana (Luka 6:46).

## Jambo Alilofundisha Yesu

Yesu alisema kwamba amepewa mamlaka yote mbinguni na duniani; kwa hiyo, wanafunzi wake walipaswa kwenda na kuwafanya mataifa yote kuwa wanafunzi, wafuasi wake, kisha walipaswa kuwafundisha kuyashika yote aliyoyaamuru Yesu (Mathayo 28:18-20). Yesu alitarajia wafuasi wake wangewashawishi watu wawe wanafunzi wake, wakiwabatiza na kuwafundisha namna ya kumtii yeye.

## Jambo Alilofundisha Petro

Katika hotuba ya kwanza ambamo msamaha ulihubiriwa katika jina la Yesu, kama Yesu alivyotabiri (Luka 24:46, 47), Petro aliwasilisha utangulizi (Matendo 2:14-21) kisha akatoa ujumbe kuhusu Yesu ambao ulihitimisha kwamba Yesu ni Bwana na Kristo (Matendo 2:22-36). Wale walioongolewa na kumwelekea Yesu kama Bwana na Kristo walichomwa mioyo yao na wakataka kujua wanachotakiwa kufanya. Petro akawaambia watubu na kubatizwa ili wapate ondoleo la dhambi zao (Matendo 2:38).

Kiini cha ujumbe wa Petro kwa viongozi wa Kiyahudi (Matendo 3:12-26) na kwa Kornelio alikuwa ni Yesu (Matendo 10:34-43). Jambo la kwanza kabisa katika hotuba za Petro ilikuwa Yesu; ujumbe wake ulikuwa Yesu na hitimisho lake lilikuwa Yesu.

## Jambo Walilofundisha Filipo na Paulo

Filipo alikwenda Samaria na kuhubiri habari za Kristo (Matendo 8:5). Walisikia, wakaamini na wakabatizwa (Matendo 8:12).

Filipo alianzia Isaya 53, fungu ambalo Mwethiopia alikuwa analisoma, akamhubiri Kristo. Towashi alipojifunza habari za Kristo aliomba abatizwe (Matendo 8:30-39).

Paulo alivyomtii Yesu, baada ya kumtokea akiwa njia kuelekea Dameski, ni ushuhuda kwamba kipindi hicho Paulo aliongolewa kikamilifu kwa Kristo (Matendo 26:16-19). Alipoongoka, Paulo alibatizwa siku tatu baadaye ili kuosha dhambi zake (Matendo 22:16). Nafsi yake iliyokufa, ilihuishwa upya katika Yesu baada ya kubatizwa (Wagalatia 2:20; Warumi 6:3-8).

Kiini cha mahubiri ya Paulo ni Yesu naye amesulibiwa (1 Wakorintho 2:1-3). Madhumuni ya kuhubiri kwake ni kuteka nyara kila fikra za wasikilizaji wake “zipate kumtii Kristo” (2 Wakorintho 10:5).

## Hitimisho

Tunaweza kuwaongoa watu kwa mambo mengi katika Ukristo, lakini uongofu wa kwanza sharti uwe kwa Yesu aliye Bwana na Kristo, baada ya uongofu huo ndipo mambo mengine yote ambayo wanaweza kuongolewa kwayo yatakuwa na maana na faida. Kuwaongoa watu kwa Yesu ili awe Kristo hapana budi kufanyika kwa moyo, roho na nguvu zetu zote. Ikiwa kuwaongoa watu kwa Kristo sio lengo letu, basi tumekwepa lengo kuu kwa habari ya kazi yetu kama wafuasi wa Yesu.

# *Kufanana na UlImwengu*

Greg Tidwell

***"Basi msifanane na hao; maana Baba yenu anajua mnayohitaji kabla ninyi hamjamwomba"*** (Mathayo 6:8).

"Hotuba ya mlimani" anaielezea mwandishi Mwingereza J. R. W. Skott, *"labda sehemu hiyo ndio inayojulikana sana katika mafundisho ya Yesu, ingawa kimijadala, ndio sehemu inayoeleweka na wachache sana, na pengine ndio sehemu walau wachache wanaitii."* Pengine ufunguo wa hotuba hii unaweza kubainika katika hitaji la Mungu la kudumu la utakatifu. Katika Maandiko yote, Mungu anawataka watu wake wajitenge na dunia. Kujizatiti katika utakatifu huilinda sheria ya Musa, kama tunavyosoma katika Walawi 18:2-4: *"Mimi ndimi Bwana Mungu wenu. Nanyi msifanye matendo kama yale ya nchi ya Misri mliyokaa, wala msifanye matendo kama yale ya nchi ya Kanaani, nitakayowapeleka; wala msiende katika amri zao hao. Mtazifanya hukumu zangu, nanyi mtazishika amri zangu, ili mwenende katika hizo, mimi ndimi, Bwana Mungu wenu."*


Maagizo haya huanza na kuhitimsha na kumbusho "***Mimi ni Bwana Mungu wako***." Mungu ambaye anaorodhesha namna ambavyo watu wake wanapaswa kuwa. Utakatifu wetu ni mfano wa utakatifu uliotukuka wa Mungu mwenyewe.

Walakini, watu wa Mungu, kwa muda mfupi walipoteza hali ya kuwa tofauti. Wakizikana sheria za Mungu, waliomba na kumpata mfalme ili kwamba "***sisi nasi tufanane na mataifa yote***" (1 Samweli 8:20). Hali ikazidi kuporomoka kwa kuongeza ibada ya sanamu. "***Sisi tutakuwa sawasawa na mataifa***," watu wakadai **"Sawasawa na jamaa za nchi nyingine, kutumikia miti na mawe"** (Ezekieli 20:32).

Akiwa kinyume na hali yao ya kurudi nyuma kwa uasi, Mungu akawaonya kwa rehema kupitia manabii wake na kwa kuwaadhibu. Mwishowe, Mungu alinena kupitia mwanawe Yesu Kristo. "***Basi msifanane na hao***," Yesu aliwaonya juu ya kuiga namna ya ulimwengu ya sala, *"Maana Baba yenu anajua mnayohitaji kabla ninyi hamjamwomba."* Hatimaye lengo la ujumbe wake ilikuwa waishi kwa imani wala si kwa kuufuatisha ulimwengu.

# KUISHI MAISHA YA UFUFUO

Bobby Dockery



Alfajiri, Jumapili asubuhi hapo zamani, wanawake wenye huzuni, wakiwa njiani kuzuru kaburi la Yesu, waliona jambo la ajabu. Walikuta jiwe limeviringishwa katika mlango wa kaburi lililotelekezwa. Ghafla, wakakabiliwa na watu wawili wakiwa wamevalia mavazi ya kumeta-meta nao wakauliza, ***"Kwa nini mnamtafuta aliye hai katika wafu? Hayupo hapa, amefufuka"*** (Luka 24:5-6).

Hayupo hapa…! Maneno haya yanajumuisha tumaini na utukufu wa imani ya Kikristo (1 Petro 1:3; 21). Ukristo unalenga msalaba uliotiwa madoa ya damu pia kaburi tupu! Ufufuo unahusu kile hasa tunachoamini, tunachotenda na kuishi kama wafuasi wa Kristo.

Kwa bahati mbaya, baadhi ya hao wanaopenda kuwa Wakristo huliona fundisho la ufufuo kama aibu kuliko kuwa chanzo cha kusherehekea. Mtume Paulo alilibaini hili kuwa sahihi katika siku zake. Alipotangaza habari za ufufuo alikabiliwa na dhihaka (Matendo 17:32), dharau (Matendo 26:24) na hofu na hasira (Matendo 23:9). Hata sasa mambo yako hivyo. Huko Uingereza, hivi karibuni kanisa la Anglikana limeingia katika mzozo kutokana na uteuzi wa askofu ambaye anapinga hadharani historia ya kweli ya ufufuka kwa Kristo. Huko Marekani,

“kongamano la Yesu” limetumia juhudi na werevu mwingi kuonyesha kwamba ufufuo haukutokea kabisa. Profesa wa seminari aliibua mashaka mengi aliposema, “Mimi siwezi kuamini tena, kutilia maanani uwongo wa ufufuo.”

Tena, tunapaswa suala la ufufuo kulichukulia kwa uzito mkubwa kama tunamwelewa Mungu na neno lake kwa uzito! Kama Kristo hakufufuka, Paulo anasisitiza, basi kuhubiri kwetu ni bure, imani ni bure, sisi tu maskini kuliko watu wote, tungali katika dhambi zetu (1 Wakorintho 15:15-17). **Hatupaswi kuamini tu katika ufufuo kama jambo la kweli, bali tunatakiwa kulifanya liwe jambo halisi katika maisha yetu** (Wafilipi 3:7-11). **Haitoshi tu kuamini kwamba Yesu alifufuka toka kwa wafu miaka 1900 iliyopita. Ni lazima imani yetu ibadilishe maisha yetu. Lazima tuitangaze imani yetu katika ufufuo kwa jinsi tunavyoishi**.

Ni huzuni isiyoelezeka kwamba Wakristo wanaendelea na maisha yao kana kwamba Kristo bado amekufa. Kwa kawaida mitizano, tunu na mitindo ya maisha yao haina tofauti kabisa na jinsi majirani zao wasioamini wanavyoishi.

Hakika kuiishi imani yetu katika ufufuo, hatuna budi kuishi maisha tofauti. Hatupaswi kuendelea kuishi kama vile maisha hasa ndiyo basi. Badala yake, lazima tujifunze kuuona ulimwengu huu nyuma ya pazia ya milele. Kama tutauchukulia ufufuo kwa uzito mkubwa, tutaviona vitu katika taswira mpya, maamuzi yetu juu ya vitu yatabadilika, njia mpya ya kupambanua mambo muhimu na yasio na maana. Ikiwa kweli tutaanza kuuishi ufufuo, tutakuwa watu wa kutoa zaidi kuliko kupokea, kutumika zaidi kuliko kutawala na kusamehe zaidi kuliko kulipiza visasi. Tutajifunza kuangalia mambo, si kama yanavyoonekana katika zama zetu, bali kama Mungu anavyoyaona!

Ufufuo ni wa kweli. Asubuhi ya zamani zile za Uyahudi, ni dhahiri malaika wawili waliwasalimu kundi la wanawake katika kaburi la Yesu kwa maneno haya *“Hayupo hapa, amefufuka…”* Je, unaamini? Je, unayaishi?

**Bobby Dockery ni mwandishi na mhubiri huko Fayetteville, Arkansas, Marekani.**

# Maoni ya Haraka katika Aya Muhimu (Mambo ya Walawi 10:3)

"Bwana akamwambia Musa, Enenda kwa watu hawa, ukawatakase leo na kesho, wakazifue nguo zao," (Kut. 19:10).

"…Nitatakaswa mimi katika hao wanikaribiao, nami nitatukuzwa mbele ya watu hao wote. Haruni akanyamaza kimya." (Law 10:3).

"Wala msiifuatishe namna ya dunia hii; bali mgeuzwe kwa kufanywa upya nia zenu, mpate kujua hakika mapenzi ya Mungu yaliyo mema, ya kumpendeza, na ukamilifu." (Rum. 12:2).

"Usilitaje bure jina la Bwana, Mungu wako, maana Bwana hatamhesabia kuwa hana hatia mtu alitajaye jina lake bure." (Kut. 20:7).

"Na ye yote atakayemkosesha mmojawapo wa wadogo hawa waniaminio, afadhali afungiwe jiwe la kusagia shingoni mwake, na kutupwa baharini." (Mk. 9:42).

Uvaaji wetu mara nyingi unaweza kuwa ni maelezo yanayoonesha tabia zetu kwa Mungu. Kama Wakristo, tunakumbushwa kwamba hatupaswi kulitaja bure jina la Mungu. Hivyo, kama Wakristo, tukumbuke kwamba tunamwakilisha **Bwana wetu** katika ulimwengu huu uliharibika.

Kuna ongezeko la uvaaji usio rasmi miungoni mwa Wakristo pindi wanapojiuzulisha mbele za Bwana katika ibada. Ingawa ni kweli tunaishi chini ya "Agano Jipya" na sio chini ya "Agano la Kale" lakini deni letu la kicho na heshima kwa Mungu wa ulimwengu bado lipo palepale kama ilivyokuwa zamani.

Badala ya kuvaa vazi ambalo lingekuwa maalumu msibani, lakini nyakati fulani mwanaume huvaa vazi lisilo rasmi katika ibada; kwa mfano imewahi kutokea hivyo hata wakati wa kushiriki "meza ya Bwana".

Kwa kufuata utamaduni wa ulimwengu, baadhi ya wanawake katika maisha yao ya kila siku huvaa mavazi mabaya pasipo haya kabisa na kuingia nayo katika ibada huku mavazi yameshikana na mwili kana kwamba ni ngozi yao ya pili, brauzi fupi na nguo zenye mpasuo unaoleta bumbuwazi kwa watazamaji, na kusababisha matatizo kwa wanaume ambao ni lazima wapite karibu yao ili kuwahudumia meza ya Bwana, na sketi zao fupi na za kubana ambazo hazisitili sana.

Na tuwe makini ili tufanane na Kristo katika uchaguzi wa uvaaji wetu katika Siku ya Bwana na kila siku. Ikiwa pekee alichonacho mtu ni "mavazi makuukuu na marapurapu," anamtolea Mungu dhabihu kwa kadiri ya alichonacho, hata ajapo kuabudu akiwa na mavazi hayo. Hivyo, tunapaswa kuweka akilini kwamba daima Mungu anatarajia tumtolee dhabihu zetu zilizo bora.

# Askari, Mwanariadha na Mkulima

**Glenn Colley**

Paulo alikuwa gerezani Rumi, pengine alijua kuwa kifo chake kilikaribia, na kwa uvuvio alimwandikia kijana Timotheo. Katika 2 Timotheo 2:2-3-6, alilinganisha kazi ya mhubiri na aina tatu za shughuli za kawaida – askari, mwanariadha na mkulima. Sasa swali ni hili: "Vipi kuhusu wahubiri? – au Wakristo kwa ujumla kwa msingi huo – wanafanana vipi na watu hawa?

"***Ushiriki taabu pamoja nami, kama askari mwema wa Kristo Yesu***." Hakuna askari anayekata tamaa mambo yanapokuwa magumu atatumika kwa hali yoyote ile chini ya mkuu wa kikosi. Hakika, mkuu wa kikosi anapaswa kujua kwamba askari wake watatekeleza wajibu wao hata kama itawagharimu maisha yao. Haya hayakuwa maneno matupu. Paulo alikuwa anakaribia kuuawa kwa ajili ya Bwana wetu. Bwana, tusaidie tusinung'unike kabisa tunapopitia siku ngumu kama Wakristo na imani yetu inapopingwa, pia utusaidie tusikate tamaa kabisa.

"***Hakuna apigaye vita ajitiaye katika shughuli za dunia, ili ampendeze yeye aliyemwandika awe askari***." Askari anatakiwa awe huru isiwepo shughuli nyingine inayovuruga kazi aliyopangiwa. Ni hivyo pia kwa Mkristo. Kwa miaka mingi ni watu wangapi hujishughulisha na masuala ya ulimwengu huu kiasi kwamba hawana muda wa kutosha kujishughulisha na mambo ya ulimwengu ujayo? Mkumbuke Dema (2 Timotheo 4:10).

"***Hata mtu akishindana katika machezo hapewi taji, asiposhindana kwa halali***." Hapa ni rejea ya michezo ya Kigriki,

inafanana sana na michezo ya olimpiki leo. Yeye anayekuwa wa kwanza hata kupigiwa makofi bado hapati tunzo mpaka anaposhindana kulingana na sheria za mchezo. Kudanganya ni kupoteza matumaini ya kushinda. Mhubiri anayetamani kulikuza kanisa lakini analegeza mafundisho ya Agano Jipya anaweza kupigiwa makofi, lakini hatakubaliwa na Mungu akifanya hivyo. Kumbuka ukweli hututakasa (Yohana 17:17), na ni ukweli huo pekee unaotuweka huru (Yohana 8:32). Kanisa ni "nguzo na nsingi wa kweli" (1 Timotheo 3:15).



"***Yampasa mkulima mwenye taabu ya kazi kuwa wa kwanza wa kupata fungu la matunda***" (2 Timotheo 2:6). Hili linaonekana kuwa ufafanuzi wa kile ambacho Paulo alikifundisha awali katika 1 Wakorintho 9:14, "***Na Bwana vivyo hivyo ameamuru kwamba wale waihubirio injili wapate riziki kwa hiyo injili***." Timotheo alitakiwa ajitahidi sana, adumu katika kufundisha injili ya Kristo na kanisa limsaidie kifedha kwa kazi yake.

**Glenn Colley ni mhubiri wa kanisa la Kristo West Huntsville huko Huntsville, Alabama, Marekani.**

Ukristo katika Matendo

# Kuziokoa Roho kwa Kristo

Dale Grissom

***"Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele. Maana Mungu hakumtuma mwana ulimwenguni ili auhukumu ulimwengu, bali ulimwengu uokolewe katika yeye"*** (Yohana 3:16-17). Kanisa hukua pale waaminio wanapobatizwa katika Kristo, na Mungu anawazidisha katika kanisa hao wanaookolewa (Matendo 2:47). Wakristo wanapohama kutoka kusanyiko moja kwenda lingine kanisa hapo halijaongeza. Hakuna ukuaji hadi hapo anayeamini anatii mpango wa wokovu wa Injili.

Kama kanisa katika jamii yetu halikui, ni kwa sababu hatuwaendei watu na injili ya Kristo. Tunatoa visingizio kwamba hakuna atakayetusikiliza, lakini tunajuwaje? Je, kweli tumejaribu? Hatuna shida kuzungumzia mpira au vitu, lakini tunatoa udhuru juu ya kwanini hatujaieneza Injili. Hatuna budi hasa kujifunza kuzungumza masuala ya kiroho na kwa upendo tukiwaendea waliopotea na kueleza ni wapi roho zao zitakuwa milele.

Ni rahisi kuota kuhusu kumtumikia Bwana, lakini kujitoa kikamilifu kwa Kristo kunahitaji juhudi kwa upande wetu. Hatima ya milele ya roho nyingi hutegemea utayari wetu na kutia juhudi hizo. Kila mmoja wetu anaweza kuazimu kufanya sehemu yake katika kuokoa roho! Tuombe ili Bwana ajaze roho zetu upendo kwa waliopotea, kwa wingi ili tuwe tayari kujitoa dhabihu kitu chochote kile muhimu ili kuipeleka injili kwa waliopotea na ulimwengu unaoangamia.

Yesu Kristo, mfano bora kabisa wa kuigwa, aliwaamuru wanafunzi wake kueneza injili. *"Basi, Enendeni mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba, na Mwana na Roho Mtakatifu; na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi; na tazama mimi nipo pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari"* (Mathayo 28:19-20). Ulimwengu unaanzia nje ya mlango wako!

**Dale Grissom (1927-2014) alijitoa katika uinjilisti binafsi na kufanyakazi na kanisa la Kristo huko Dexter, Missouri, Marekan**

# *Tumeitwa Kuongoza au Kutumika?*

Claude Thompson



Maneno, "kiongozi" na "uongozi" yametumika mno na mara nyingi siku hizi hupotoshwa kanisani. Basi, inawezekana kabisa yameeleweka vibaya. Mara chache sana tunawatambua tu wazee au mhubiri kama "viongozi" wa makusanyiko yetu, au tunaweza kusema ibadani ndugu "tuongoze" meza ya Bwana au katika sala. Huwa tunafasili "uongozi" kama kusimamia au kuelekeza na "kiongozi" ni kama bwana au mtu anayetoa maagiza. Hata hivyo, Biblia inaainisha taswira tofauti kabisa juu ya uongozi wa kweli kiroho.

Neno la Kiyunani lililotafsiriwa "ongoza" *(hodegeo)* lina maana "kusafiri pamoja" au "kulinda" mtu fulani. Kwa ufasaha linaweza kutumika kiistiari kwa waalimu kufundisha, ikiwa ni waalimu wa kweli (Waebrania 5:12) au wa uwongo (2 Petro 2:1).

Tena, Agano Jipya kwa nadra limetumia neno "ongoza" na "kiongozi" na kila mara yanapotumika, ni katika mazingira hasi. Yesu aliwaita waalimu wa kiroho siku zake ***"viongozi vipofu wa vipofu"*** (Mathayo 15:14). Bwana wetu kipekee anatushauri tusijiite viongozi wala tusiwaone wengine kama viongozi au "mabwana" kwa sababu, Yeye, Kristo, ndiye kiongozi wetu pekee (Mathayo 23:10). Awali alipowaita watu kuanzisha na kuongoza kanisa lake, Yesu aliwachagua

wavuvi badala ya manahodha wa bahari kadhalika wachapa kazi badala ya watawala (Mathayo 4:18-21). Alitaka na kutamani wachapakazi badala ya watawala kwa ajili ya ufalme wake (Luka 10:2), waume kwa wake wenye sifa na wanaopenda kuwatumikia wengine. Hao ndio viongozi wa kweli wa kanisa – ***"kiongozi ni sawa na yeye anayetumika"*** (Luka 22:26).

**Yesu anatuita tutumike badala ya kuongoza**. Ingawa ni Mungu kamili na anayestahili heshima zote (Ufunuo 4:9-11), alituonyesha kielelezo thabiti cha utumishi na kufundisha kwamba mtumishi ni mkubwa kuliko bwana (Yohana 3:5-16). Wale ambao Yesu aliwatambua kuwa wakubwa katika ufalme wake ni hao **walioonyesha** imani (Mathayo 8:10-13) na wale waliotumika kimya kimya (Mathayo 26:10-13). Wakristo wameumbwa na Mungu vilevile wamefinyangwa upya katika Kristo ili watenda kazi yake ya utumishi (Waefeso 2:10).

**Utumishi wa kiroho msingi wake ni upendo zaidi kuliko umaarufu au kutaka zawadi.** Mungu mwenyewe ni mfano bora kabisa wa utumishi ambao msingi wake ni upendo (Yohana 3:16). Wakristo wao kwa wao wanapaswa kutumikiana kwa upendo (Wagalatia 5:13). Kama wafuasi wa Yesu, tunapaswa kuwapenda hata maadui zetu (Luka 6:35). Tunapowatumikia wengine, ni kama tunamtumikia Mungu, na utumishi lazima utoke katika mioyo safi (Waefeso 6:5-6).

**Utumishi wa kiroho una hali kutambulika na thawabu zake** (1 Wakorintho 3:8). Wakristo wanapaswa kuwatambua na kuwaheshimu hao wanaowaongoza katika kuwahudumia, iwapo ni katika ulimwengu wa kimwili (Waefeso 6:2; Warumi 13:7-8; 1 Timotheo 6:1) au ulimwengu wa kiroho (1 Wakorintho 12:23-25; Wafilipi 2:19-20; 1 Timotheo 5:17). Bila kujali sifa zozote zile tunazoweza kuzipata katika maisha haya duniani, heshima yetu kubwa na iliyo muhimu zaidi tutapata mbinguni (Mathayo 5:11-12; Ufunuo 11:18). Tunapaswa kufanya kazi kwa uvumilivu, tukigonjea thawabu yetu (Yakobo 5:7). Watumishi wa Kikristo lazima tuwe makini kwamba hatufanyi shughuli zetu za kiroho ili watu watuone, bali sifa na utumishi wa kweli apewe Mungu (Mathayo 6:1-6).

**Claude Thompson ni mkazi wa Dallas, Texas, Marekani.**

# Ibada Yenye Maana Hasa

Rodney Nulph

Kwa watoto wa Mungu waadilifu na waliojitoa, kuabudu ni jambo la muhimu katika kila juma. Ni fursa yenye heri na heshima kusujudu mbele ya [***Mungu] Mkuu Aliyeko Daima***. Yesu alifanya ibada kama kipaumbele muhimu sana (Luka 4:16). Cha kuhuzunisha, mara nyingi ibada imepungua thamani yake na hata kuwa "desturi" tu, au mazoea ya kawaida (Mathayo 15:7-8). Mungu ndiye anayestahili kuabudiwa, na kama ndivyo, hastahili tu, bali anataka usikivu wetu wote na kujizatiti. Inasikitisha wanadamu wanaposhindwa kabisa kumwabudu Mungu wa Mbinguni. Watu wengi wanaokiri kuwa Wakristo wanakariri vitendo fulani hatua kwa hatua wakivirudia-rudia na kisha huondoka hapo bila ya kuabudu kibiblia. Yesu aliitaja ibada kwamba ni muhimu alipoketi katika kisima cha Yakobo na kuzungumza na mwanamke Msamaria ***"Mungu ni Roho; nao wamwabuduo yeye imawapasa kumwabudu katika roho na kweli"*** (Yohana 4:24).



Kwanza, ibada inamlenga **nafsi maalumu**; "Mungu ni Roho…" Mambo yanayotendeka katika ibada karne 21 hasa hasa ni kuwaburudisha waliofika hapo. Mwanadamu amekuwa ndiye "mhusika

mkuu" na lazima afurahie sana na kushangaa. Tunapima ufanisi wa mhubiri, uwezo wa mwongoza nyimbo na "msisimko" wa jengo linalotuzunguka. Tunaipima ibada sawa na vile tunavyoipima filamu kwenye *skrini kubwa*. Wakati huo tunashindwa kuelewa ukweli wa Maandiko kwamba Mungu ndiye Mhusika mkuu; yeye ndiye tunayekusudia kumpendeza na wala sio sisi wenyewe!

Pili, ibada inawahusisha **washiriki**; **"…** ***nao waabuduo***…" Ibada ni **kazi ngumu**! Tumekuwa na desturi ya kuwa na majengo yenye viti vya kuegama pamoja na viyoyozi vya kudhibiti hali ya joto kiasi cha kwamba wengi wanaiona ibada kama **wakati wa burudani** – wakati wa kustarehe na kupumzika. Hata hivyo, ibada yenye tija kubwa hupima akili zetu, kiwango cha umakinifu wetu na hata uwezo wetu kimwili. Kuimba, kujifunza, kusali, kutoa na kumkumbuka Bwana wetu vinahitaji juhudi na nguvu. Hatuna budi kutulia kiakili na kimwili, ili tushiriki kikamilifu kama Mungu anavyotaka. Neno "ibada" lenyewe linamaanisha mtu kusujudu, kama vile mkulima anavyoanguka mbele ya mfalme. Hili ni taswira tofauti kabisa na kujifunza huku tukiketi kwenye viti mwororo!

Tatu, ibada inajumuisha ruwaza (ramani) iliyoelekezwa; *"wamwabudu katika roho na kweli*." "***Roho***" inahusisha hisia na utashi wa mwenye kuabudu. Ibada ambayo haigusi hisia si kuabudu katika roho! Inawezekana vipi waabuduo halisi wasiguswe wakati wanatafakari upendo na dhabihu kuu iliyotolewa kwa ajili ya kila mmoja wetu? "***Kweli***" hurejea anachotaka Mungu hasa hasa **vitendo vya ibada**. Viwili vyote kweli na roho lazima viwepo ili ibada itimie kibiblia.

Ibada ni **suala zito**. Mungu anachukia pale watu wanapojaribu kuabudu na kushindwa kuifanya kwa usahihi (Walawi 10:1-3). Muda mwingine haupo tunakuwa karibu na Muumba wetu isipokuwa wakati tunapomsujudia na kumwabudu. Hata hivyo, kinyume chake ni sahihi pia. Ibada yenye manufaa hasa iwe ndio kipaumbele chetu, na kila siku *"tuingie malangoni mwake kwa kushukuru, nyuani mwake kwa kusifu…"* (Zaburi 100:4a).

**Rodney Nulph ni mhubiri wa Injili na mhariri mshirika wa jarida la mtandaoni la Gospel Gazette. Ni mkazi wa Spences, Wisconsin, Marekani.**

# Je, Utakuwa Wapi?

Dalton Key

Ibada ni kwa ajili ya roho sawa na chakula kizuri kwa mwili. Ni muhimu sana kwa ajili ya ukuaji na ustawi wetu kiroho. Tunapoiinua mioyo yetu mbinguni katika sala, tunapoimba nyimbo kwa pamoja, kwa heshima nyingi tunapokumbuka msalaba wa Kalvari kwa njia ya kushiriki Chakula cha Bwana, tunapotoa mali zetu na kujifunza mapenzi ya Mungu, tunashiba na kujazwa matumaini mapya, tunapata nguvu na kujitoa katika utauwa.

Daudi alifurahi aliposikia maneno, *"Na twende nyumbani mwa Bwana"* (Zaburi 122:1). Paulo alisubiri Troa siku saba, hadi siku ya Bwana, ili akusanyike pamoja na wanafunzi katika ibada (Matendo 20:6-7). Kabla ya hayo, huko Filipi, Paulo na Sila walitupwa "***chumba cha ndani***" gerezani miguu yao ikiwa imefungwa kwa mkatale, walitumia muda wao vizuri kwa "kuomba na kuimba sifa kwa Mungu" (Matendo 16:24-25).

Mara nyingi roho za wenye haki zimefanywa imara daima kwa njia ya ibada safi na inayogusa moyo. Ibada ni nzuri kwa ajili ya nafsi.

Kwa mwanga wa ukweli huu, hatushangai kusoma maonyo makali, yaliyovuviwa: *"Wala tusiache kukusanyika pamoja kama ilivyo desturi ya wengine; bali tuonyane na kuzidi kufanya hivyo kwa kadiri mwonavyo siku ile kuwa inakaribia"* (Waebrania 10:25).

Utakuwa wapi siku ya Bwana inayokuja? Je, utakutana na watakatifu ibadani? Kama hapana, kwa nini hapana?

**Dalton Key ni mhariri wa jarida la Old Paths na mhubiri kwa miaka 10 katika kusanyiko lililopo Rockford huko Tulsa, Oklahoma, Marekani.**

## Je, Unajua?

Hekalu lililojengwa na Mfalme Sulemani lilikuwa na urefu mikono 60 (futi 90.), upanda mikono 20 (futi 30.) na kimo kwenda juu mikono 30 (futi 45) (1 Wafalme 6:2). Hekalu lililojengwa na Zerubabeli (Hagai 2:3-4, Ezra 6:3-12) lilikuwa urefu mikono 60 (futi 90) na upana mikono 60 (futi 90).

**Rebecca Rushmore ni mwandishi katika jarida la Sauti ya Kweli Kimataifa.**

# Amri Kumi Kwa Ajili Ya Kuboresha Ibada

**Mwandishi Asiyejulikana**

Je, umewahi kusikia mtu akisema, “Sinufaiki sana na huduma ya ibada”? Wakati mwingine hili humbainisha mtu alivyo zaidi kuliko huduma za ibada. Hapa kuna baadhi ya nasaha ambazo zitakusaidia ibada yako iwe na manufaa zaidi unapokusanyika pamoja na watakatifu siku ya Bwana.

1. **Ifanye Jumapili iwe kipaumbele**. Ni jambo muhimu sana kujitoa katika juma. Hakuna jambo lingine zito kuliko hili la kukutana na Mungu.
2. **Usimletee Mungu mabaki**. Siku zote Mungu ametaka “matunda ya kwanza.” Hawezi kuridhika na makombo. Pata usingizi wa kutosha Jumamosi usiku na uje ibadani ukiwa umechangamka na akili mpya.
3. **Jiandae kiakili**. Nidhamu huanzia katika akili. Kadhalika hali ya uanafunzi. Jizoeshe akili yako kuzingatia masuala ya kiroho.
4. **Fika kwa wakati**. Hali ya kukimbia-kimbia kutokana na kuchelewa itaondoa umakini na kuwasumbua wengine wanaoabudu. Kama inawezekana amka mapema kidogo.
5. **Njoo na Biblia**. Kufika ibadani bila ya Biblia yako ni sawa na kwenda kuendesha gari lako bila ufunguo.
6. **Fungua mdomo wako na uimbe**. Kuimba si hiari. Ni amri. Isitoshe hao wanaokiuka amri hii wana hatia sawa na hao wanaoacha kukusanyika.
7. **Kaa kiti karibu na mbele**. Uzoefu unaonyesha kwamba baadhi ya washiriki dhaifu wa kanisa wanaona bora wabadilishe makusanyiko kuliko kubadilisha viti. Utafiti unaonyesha kuwa kiwango cha kushiriki kihisia na kiakili hupungua pale mtu anapozidi kuketi viti vya nyuma.
8. **Kabla na baada ya ibada – uwe rafiki**. Ibada huimarika ikifanyika kama familia. Wanafamilia wanapaswa kufahamiana na kupendana kila mmoja.
9. **Sikiliza hotuba kwa makini**. Kuchukua maelezo kwafaa sana. Fuatilia somo katika Biblia yako. Uchukulie ujumbe kwa uzito

mkubwa. Utakufaa. Itamtia moyo mzungumzaji. Itawaonyesha wasio Wakristo kuwa wewe u makini.

10. **Ifanye ibada yako kuwa Mungu ndiye kitovu, wala si mwanandamu**. Kimsingi kuabudu ni hali ya kujisalimisha. Hao wanaosema, "Sinufaiki sana katika ibada" wanachokitafuta sicho. Ni katika kujitoa wenyewe ndipo tunapata. **Hakuna kutoa – hakuna kupata**.

# Madhumuni ya Ibada Yetu

Louis Rushmore

Madhumuni ya ibada ya Kikristo ni Mungu Mkuu (Kutoka 20:1-6; Yohana 4:23) na yeye pekee (2 Samweli 20:21; Mathayo 4:10). Yeye, kadhalika, ndiye hadhira anayewatazama Wakristo wakiabudu "katika roho na kweli" (Yohana 4:24). Hilo linamaana kwamba Wakristo wanapaswa kumwabudu Mungu kwa njia ambayo yeye kupitia Roho mtakatifu (2 Petro 1:20-21) ameagiza katika Agano Jipya. Kwa hiyo, anakifurahia mwanadamu na matakwa yake katika ibada ya Kikristo havina uzito kuliko mambo anayoyatarajia Mungu kutoka kwa watoto wake. Hivyo, kile ambacho mwana wa Mungu anakikabidhi katika ibada ni muhimu zaidi kuliko anachojua anapokea katika ibada. Lakini, hao waliozoelea kiroho kumwabudu Mungu kwa wakati na katika njia anayotaka wanapaswa vilevile kuridhika na ibada hiyo.

Si muhimu sana ibada kuiongezea mbwembwe au kujaribu kuifanya iwe ya kiroho zaidi. Hakuna kitakachokuwa cha kiroho zaidi ya kumwabudu Mungu kwa njia ambazo amewaagiza wanadamu wamwabudu. Ni dhahiri, watu wengi leo wamebadilisha vitendo vya ibada ili viwafae wao zaidi kuliko Mungu au kupata idadi kubwa ya watu. Hata hivyo, kanisa la Agano Jipya liliweza kuupindua ulimwengu (Matendo 17:6) kwa njia ya injili rahisi ya Yesu Kristo. Injili safi isiyo na madoido (Wagalatia 1:6-9) "ni uweza wa Mungu uletao wokovu" (Warumi 1:16) kwa watu wote. Kwa injili hiyo mtu anaweza kutambua namna ya kumwabudu Mungu na kukubalika (Mathayo 15:8-9).



Siku moja asubuhi mke alimwambia mume wake, "tumepata mbwa mjanja. Kila siku asubuhi analeta gazeti."

Mume wake akajibu, "Sawa, lakini mbwa wengi wanaweza kufanya hivyo."

Mkewe akajibu, "Lakini kamwe hatujawahi kuchangia gazeti lo lote lile!"



Ada ya dola moja ilikutana na ada ya dola ishirini na kusema, "Wewe, ulikuwa wapi? Sijakuona sehemu kwa muda."

Yule wa ishirini akajibu, "Nimekuwa nikitembelea makasino (majumba ya starehe), nikaenda kwenye meli za starehe, na kufanya mizunguko katika meli, na kurudi Marekani kwa muda, na kwenda kwenye michezo kadhaa ya baseball, katika masoko makubwa vitu vya namna hiyo. Vipi kuhusu wewe?"

Yule wa tozo ya dola moja akasema, "Unajua nini? Kanisa lilelile lazamani lisilolipa, kanisa, kanisa tu."



Gari ya Alice mara kwa mara lilikuwa si la kutegemea, kila wakati linapopata shida humwita mumewake AI ili amwendeshe. Siku moja AI akapigiwa simu.

**AI :** "Kimetokea nini safari hii?"

**Alice :** "Breki zangu zimeachia, unaweza kuja kunichukua?"

**AI :** "Upo wapi?"

**Alice :** "Nipo katika duka la dawa."

**AI :** "Na gari iko wapi?"

**Alice :** "Lipo hapa pamoja nami."



Binti mdogo mwanafunzi alikuwa akisomea falaki (sayansi ya sayari) na kufurahia sana. Siku moja asubuhi wakati wa kifungua kinywa akasema, "Ijumaa moja tunamtihani

katika mwezi." Mdogo wake wa kiume akapiga kelele, "Mama, unamwacha aende?"



Johnny alimwuliza bibi yake (nyanya wake) kuwa ana umri gani.

Bibi akajibu, "Therasini na tisa na bado nashikilia."

Johnny akifikiria kuhusu hilo kisha akauliza, "Sawa, kama ungeachilia ungekuwa na umri gani?"



Becky mwenye umri wa miaka sita alikuwa na mazungumzo na bibi yake (nyanya wake) wakati wakipata kifungua kinywa.

**Becky :** "Bibi, mimi ni kibonge mzee."

**Bibi :** "Becky! Umesema nini?"

**Becky :** "Mimi ni kibonge mzee.:

**Bibi :** Sasa Becky, kwanini unasema kitu kama hicto?"

**Becky :** "Sawa, kila mtu husema naonekana kama baba yangu."



Mtu mmoja aliiandikia barua hoteli iliyopo mjini aliyopanga kuitembelea wakati fulani katika wiki zijazo.

Aliandika: "Ningependa sana kuja na mbwa wangu. Anamwonekano mzuri sana na mwenye tabia nzuri. Je, mko tayari kuniruhusu nikae naye katika chumba change usiku?"

Majibu ya haraka yakatolewa na mmiliki wa hoteli: "Bwana, nimekuwa niiendesha hoteli hii kwa miaka mingi. Katika kipindi chote hicho, kamwe sijawahi kuwa na mbwa anayeiba mataulo, mashuka, mapambo ya mezani, au picha za ukutani. Kamwe sijawahi kulazimika kumfukuza mbwa mpangaji usiku wa manane kwa sababu ya ulevi na vulugu. Na kamwe sijawahi kuwa na mbwa anayeikimbia tozo ya hoteli.

"Ndiyo, bilashaka, mbwa wako anakaribishwa katika hoteli yangu. Na, ikiwa mbwa wako atakudhamini, wewe pia unakaribishwa kukaa hapa."



Mjukuu wa kiume wa rafiki yangu mwenye miaka sita alimwita mama yake akiwa kwa rafiki yake katika nyumba ya Charlie na kukiri kwamba

alivunja taa alipotupa mpira wa miguu katika sebure yao.

"Lakini mama," alisema, "huna haja ya kuhofia kuhusu kununua nyingine, mama yake Charlie alisema ilikuwa haifidiki."



Nilibadilisha sauti ya oni ya gari yangu kuwa milio ya bunduki. Inavutia, sasa hivi watu wanapicha barabarani kwa haraka.



Leo sijaenda katika ukumbi wa mazoezi. Hiyo inafanya kuwa miaka mitano katika mstari (safu).




Nimetoka kusoma kuwa watu 4,153,237 wameoana mwaka jana. Sio kusababisha kengere au hofu, lakini hiyo haipaswi kuwa namba shufwa?

## TABIBU

**"Moyo uliochangamka ni dawa nzuri;**
**Bali roho iliyopondeka hukausha mifupa."**

**Mithali 17:22**



# Je, Unatathmini Vipi?

**Akajibu akawaambia, "Hamkusoma ya kwamba yeye aliyewaumba mwanzo, aliwaumba mtu mume na mtu mke; akasema, kwa sababu hiyo mtu atamwacha babaye na mamaye, ataambatana na mkewe, na hao wawili watakuwa mwili mmoja? Hata wamekuwa si wawili tena, bali mwili mmoja.**

**Basi aliowaunganisha Mungu, mwanadamu Asiwatenganishe Wakamwambia, jinsi gani basi Musa aliamuru kumpa hati ya talaka, na kumwacha? Akawaambia, Musa, kwa sababu ya ugumu wa mioyo yenu, aliwapa ruhusa kuwaacha wake zenu; lakini tangu mwanzo haikuwa hivi.**

**… Nami nawaambia ninyi, kila mtu atakayemwacha mkewe, isipokuwa kwa sababu ya uasherati, akaoa mwingine, azini; naye amwoaye yule aliyeachwa azini.**

**Wanafunzi wake wakamwambia, mambo ya mtu na mkewe yakiwa hivyo, haifai kuoa."**

**Mathayo 19:4-1**

# Safari ya Mbinguni

Wes McAdams



Watu wananiambia kwamba watakapokufa lengo lao kuu katika maisha ni kwenda mbinguni. Nina uhakika kabisa mimi nami nimesema kitu kama hicho. Kila mara nilifikiri kuwa hilo ndilo lengo muhimu zaidi ambalo mtu hana budi  kuwa nalo, lakini nimebadilisha msimamo. Kadiri ninavyokitafakari kirai hicho, ndivyo ninavyozidi kutafakari jinsi kinavyoibua sitofahamu nyingi ndani ya mioyo yetu.

Tunamaanisha nini hasa tunapozungumzia lengo letu la kufika mbinguni? Tunapokuwa na lengo, hatuna budi kuwa na njia fulani tunazoziamini kulifikia lengo hilo, sawa? Kama nikikwambia lengo langu ni kupunguza uzito ratili 15, unaweza ukaniuliza, “Unatarajia kulifikia vipi lengo lako? Ndipo nitakapokujibu kwa kuorodhesha

matendo yote mazuri nitakayoyatekeleza ili niweza kulifikila lengo langu. Linalosikitisha, wengi wetu tunadhani hiyo ndio njia ya kwenda mbinguni.

Tumezoea kufikiri kuhusu matendo yetu yote mazuri ndio kiwango cha mema yanayotosha kutufikisha mbinguni, jambo ambalo linatufanya baadhi yetu tujiamini sana kuwa tumefanya yote ambayo Mungu ameagiza ili tufanikiwe kuingia huko. Lakini, mara kwa mara, wengi wetu tunabaki na wasiwasi inayotokana na udhaifu wetu, hatujawa wema vya kutosha. Baadhi wanajitahidi kutenda kwa kiwango cha chini kabisa, na wengine wanajitahidi kufanya zaidi ya uwezo wao. Hivi ndio viashiria vya kwamba wengi wetu hatuelewi Habari Njema za Yesu Kristo.

## Kuielewa Neema

Tunaishi katika tamaduni (jambo la kushuru) ambapo kama tunataka kitu fulani, tunaweza kwa kawaida kuweka akiba ya fedha mpaka tutakapomudu kukinunua. Nyakati za Biblia, ingawa vitu vilikuwepo vingi ambavyo mtu wa kawaida asingemudu kuvinunua kabisa. Vitu hivyo wasingeweza kuvipata kabisa watu wa tabaka la chini katika jamii.

Ikiwa mtu wa kawaida alihitaji kitu fulani ambacho hawezi kukinunua, angeomba “msaada” kutoka kwa mtu mwema wa tabaka la juu katika jamii. Kama mtu huyu tajiri angependa kumsaidia, angekuwa mlezi au mfadhili wake. Msaada aliompatia ulijulikana kama “*charis*” neno la Kiyunani tulilolitafsiri “neema.”

Upendeleo huu ulikuja na matarajio fulani. Ikiwa mtu alitenda wema kwako, ilikuwa ni wajibu wako katika maisha yako yote kutangaza wema wake na pia kumtumikia kwa uaminifu kila mara atakapokuhitaji. Hili halikuwa jambo la kulipa deni kwa wema wake; ni njia sahihi ya kuonyesha shukrani kwa yeye aliyetendewa wema. Agano Jipya linasema, *“Lakini Mungu, kwa kuwa ni mwingi wa rehema, kwa mapenzi yake makuu aliyotupenda; hata wakati ule tulipokuwa wafu kwa sababu ya makosa yetu; alituhuisha pamoja na Kristo; yaani tumeokolewa kwa neema.”* (Waefeso 2:4-5). Hivi ndivyo wokovu unavyofanya kazi – Mungu ametoa kama zawadi (mstari wa 8). Mungu ni mkarimu asiye kifani na mfadhili wa ajabu ambaye anawatendea wema waovu ambao wanaohitaji hasa kile ambacho yeye pekee anaweza kuwapa – msamaha na kuachilia huru.

## Kuelewa Matendo Mema

Katika ulimwengu wa karne ya kwanza, moja ya jambo baya sana ilikuwa ni kukosa shukrani. Ikiwa ulikubali kupokea "*charis*," lakini hujawa mwaaminifu kwake, ungetengwa na jamii. Asingetokea mtu mwingine yeyote kukutendea wema mwingine kwa sababu dhahiri umejibainisha kuwa wewe si mtu wa shukrani.

Dhana ya neema na shukrani zinaungana na hazitenganishwi. Hakika, si vigumu kuona hata katika Kiingereza maneno "*grace*" na "*grateful*" yanayotumia mzizi mmoja. Hii ni kwa sababu "neema" si neno pekee lililotumika kwa habari za zawadi iliyotolewa, lakini pia ni kwa ajili ya mpokeaji sahihi wa zawadi. Hata sasa wakati mwingine tunaitaja sala inayotolewa kabla ya chakula kuwa kutoa shukrani (*saying grace*). Kwa Kispaniola, neno "asante" ni "*gracias*" pale mtu anapokuonyesha neema unaipokea kwa shukrani.

Hivyo ndivyo utii wetu kwa Mungu unatakiwa uwe. Ndio maana tunatenda matendo mema. Ndio maana tunaimba sifa kwake. Ndio sababu tunawaambia majirani zetu habari za injili. Hatuyafanyi hayo ili yatupeleke mbinguni. Tunaonyesha shukrani zetu kwa sababu "***ametuketisha pamoja naye katika ulimwengu wa roho, katika Kristo Yesu***" (Waefeso2:6). Kamwe kutenda mapenzi ya Mungu isionekane kama jitihada za kutupeleka mbinguni, lakini yanapaswa kudhihirika kama matendo ya shukurani kwa sababu kwa neema yake ametupa makao mbinguni. Tunatakiwa kufanya chochote kile ambacho Mungu anataka sisi tukifanye kwa sababu tuna shukurani nyingi kutokana na kile alichotukirimia.

## Usiwe mtu asiye na fadhila

"Asiyefadhila" ni mtu asiyeonyesha shukrani kwa vitu alivyopewa. Asiyefadhila ni mtu ambaye ama anaishi maisha kwa namna ambayo hayamwinui mfadhili wake au mtu anayejivuna kama anastahili kuwa na vitu alivyopewa. Wasiofadhila watajikuta wametengwa na neema ya Mungu.

Katika Galatia palikuwa na Wakristo ambao walidhihirisha kukosa fadhila kwa kuipokea injili ya nyingine ya uongo, ambayo ilifundisha kwamba mtu anaweza kuhesabiwa haki kwa njia ya torati. Paulo aliandika *"mmetengwa na Kristo, ninyi mtakao kuhesabiwa haki kwa sheria, mmeanguka na kutoka katika hali ya neema"* (Wagalatia 5:4).

Badala ya kuipokea zawadi kwa shukrani (ya kuhesabiwa haki), walijaribu kuipata kwa juhudi zao wenyewe.

Vile vile, mwandishi wa Waebrania alisema, *"Maana kama tukifanya dhambi makusudi baada ya kupokea ujuzi wa ile kweli, haibaki tena dhabihu kwa ajili ya dhambi. Bali kuna kuitazamia hukumu yenye kutisha, na ukali wa moto ulio tayari kuwala wao wapingao"* (Waebrania 10:26-27). Tukidumu katika dhambu kwa makusudi, tunajibainisha wenyewe kuwa ni watu wasiojali, tusiostahili kupokea karama ambayo Mungu amewaahidi watoto wake.

## Jambo la Msingi

Ikiwa tuna – imani yenye toba – tumemvaa Kristo kwa njia ya ubatizo (Wagalatia 3:27), Mungu kwa neema zake tutaishi pamoja naye mbinguni: ***"…Lakini Mungu, kwa kuwa ni mwingi wa rehema, kwa mapenzi yake makuu aliyotupenda; hata wakati ule tulipokuwa wafu kwa sababu ya makosa yetu; alituhuisha pamoja na Kristo; yaani, tumeokolewa kwa neema. Akatufufua pamoja naye, akatuketisha pamoja naye katika ulimwengu wa roho, katika Kristo Yesu; ili katika zamani zinazokuja audhihirishe wingi wa neema yake upitao kiasi kwa wema wake kwetu sisi katika Kristo Yesu"*** (Waefeso 2:4-7). Kwa kifo cha Kristo, tayari ametimiza mambo yote muhimu ili sisi tufike mbinguni; kwa hiyo, hatuna budi kujiweka lengo jipya! Lengo letu linapaswa kuwa kumwonyesha shukurani kwa kumsifu na kumtumikia daima.

Ikiwa tutaendelea kumtumikia kwa shukrani, hatuna haja ya kuwa na mashaka kwa lolote, kwa sababu tumeokolewa kwa ustahilifu wake…. wala si njia zetu.

**"*1* Msifadhaike mioyoni mwenu; mnamwamini Mungu, niaminini na mimi.**
***2* Nyumbani mwa Baba yangu mna makao mengi; kama sivyo, ningaliwaambia; maana naenda kuwaandalia mahali.**
***3* Basi mimi nikienda na kuwaandalia mahali, nitakuja tena niwakaribishe kwangu; ili nilipo mimi, nanyi mwepo.**
***4* Nami niendako mwaijua njia."**

**Yohana 14**

# MTANZIKO WA KUSIKITISHA

(Mtazamo wa mwanamke)

Samuel Matthew

Hakika nyakati zimebadilika! Hapo nyuma wakati fulani jamii ilimtarajia mwanamke kuwa mke mwaminifu na mama mwema. Hapo nyuma wakati fulani uzinzi ulikuwa jambo la fedheha. Wanawake walitarajiwa kuwa mabikra pindi wanapoolewa, na hao wanawake walioishi na mwanaume pasipo ndoa walipachikwa majina na kutengwa. Leo hii Marekani tumepotoka mbali kiasi gani kinyume na viwango na matarajio!

Asubuhi moja, nilibahatika kuona kipande cha mazungumzo katika runinga ambapo mtu aliyekuwa akihojiwa alikuwa ni mwanamke aliyetafuta kupata mtoto. Hadi hapo mambo yote yalikuwa ni safi kabisa. Shida pekee ilikuwa mwanaume aliyeishi naye kwa kwa miaka saba (nje ya ndoa) HAKUTAKA kuwa na watoto. Suluhisho alilolipata ni kuwekewa mbegu za mwanaume ili apate mtoto. Mwanaume alitamka kwamba ikiwa angefanya hivyo, yeye angeondoka. Naye alisema hilo lingekuwa sawa kwake; hata hivyo hakuwa na haja naye tena! Watazamaji walimdharau mwanaume kwa kutaka kuondoka. Ni mazingira ya namna gani haya yasiomcha Mungu!

Katika hadhira hiyo nzima, mwanamke mmoja alithubutu kusimama na kushauri kwamba kwanza mwanamke huyo amtafute mwanaume ampendaye, waoane, alafu, baada ya kipindi cha mpito cha kuweka sawa mambo, wazae mtoto. Sadakta, niliwaza. Hilo ni sahihi kwako kusema hivyo! Hata hivyo kilichofuata si kigeni, kinachohuzunisha na kigumu kuamini. Ghafla, watazamaji wengi wakalipinga hilo kwa sauti. Kisha mwongoza kipindi kile akatoa kauli fulani inayosema: “Mwanamke huyu anatokea wapi? Je, anaishi karne ya ishirini?” Hakika, kila mmoja akacheka na kuafiki. Wazo lake la kuanzisha familia sahihi, yenye muundo wa utauwa ukumbi mzima ulicheka na kubeza.

Nyakati hizi ni mbaya ambazo sisi tunaishi ndani yake. Vitu visivyo vya kawaida vimegeuka kuwa vya kawaida. Haishangazi

wanawake wamechanganyikiwa mno hata kushindwa kujua nafasi zao katika jamii. Nafasi alizopewa mwanamke na Mungu zimefutwa kwa makusudi katika akili za watu. Shetani yupo kazini!

Tutafanya nini juu ya hili? Je, tutakaa tukiwa tumekunja mikono, bila kusema chochote kwa kuogopa dhihaka ambazo bila shaka tutazipata ikiwa tutaongea? Je, tutayarekebisha maisha yetu ili yalingane na jamii tuliyomo? Linalosikitisha, wanawake wengi waliojibainisha kuwa Wakristo wanafanya mambo kama hayo. Naamini kwamba, "kuwa kielelzo safi" pekee hakutoshi. Kama hali ninavyoiona, wanawake wanapaswa kuwa na nguvu na uwezo wa kusimama imara na kutegemewa – kutegemewa kama viumbe kwa ajili ya Mungu na kwa nafasi ambazo Mungu amewajalia.

Kama vile kutakavyokuwa na "vita na uvumi wa vita" ulimwenguni siku zote (Marko 13:7), vilevilve kanisa la Bwana litakabiliwa na vita. Kuna watu wanaopenda madaraka, wanatamani kutawala na kutafuta mabadiliko. Kanisa ndilo linalowindwa sana na Shetani. Kwa miaka mingi ambayo nimekuwa Mkristo wa Agano Jipya, nimefuta machozi mengi kutokana na mambo kuzuka kama "mwanaume, sio kitu"; harakati za kikarismatiki, mabishano ya *Crossroads*; masuala ya ndoa, talaka na kuoa/olewa tena; "umoja katika kutofautiana"; hemeneutiksi [sayansi ya kutafsiri] mpya na kisasa – nafasi ya mwanamke.

(Biblia) ni "KITABU" pekee ambacho kinatukataza tusibadilishe neno la Mungu na mpango wake kwa pande mbili zote wanaume na wanawake. Ndicho kitabu pekee cha kufuata kwa habari ya majukumu tuliyopewa na Mungu, majukumu ambayo yanaturudisha siku za mwanzo kabisa yatakayodumu hadi mwisho wa dunia. Dada mpendwa katika Kristo, ninakuomba: usimpe nafasi Shetani akurubuni kama alivyofanya kwa Hawa. Tusiwaingize watu wa Mungu katika dhambi za ziada kwa kuhamasisha "njia mpya," njia ya uongo, kama inavyopendekezwa na Shetani.

Ninaposoma juu ya "ukweli mpya" kama ulivyobainishwa na baadhi, ni kama vile Shetani alikuwa akiwaambia wanawake, "*Je, kweli Mungu amesema kwamba hamuwezi kuwa maaskofu au wahubiri*? *Unadhani Mungu bado anataka ufuate sheria za zamani zilizopitwa na wakati katika ulimwengu wa sasa ulioendelea – kwamba kwa hali halisi muwatii waume zenu? Hakika mna akili na mmesoma vya kutosha*

*katika zama hizi za mwanga mkubwa wa elimu na mnajua vizuri zaidi ya hayo! Mbona, msomi yeyote makini anajua mwanamke ana uwezo wa kufanya jambo lolote ambalo mwanaume anaweza. Kwanini, mwanamke azuiliwe fursa ya kuongoza ibada ilhali ana uwezo mkubwa? Jinsi gani upoteze talanta yako kwa kung'ang'ania tamaduni zilizopitwa na wakati, wajibu wa kimapokeo tokea zama za giza? Ukinisikiliza tu, nitakufanya uwe na hekima na kuwa huru*."

Sadakta, Shetani anawataka wanawake waamini hayo! Bado anataka kushinda vita kama alivyowahi kushinda. Anapenda mamlaka na enzi na anajaribu kuwafanya Wakristo wamtilie mashaka Mungu na njia zake. Wanawake, tafadhali, msimpe nafasi Shetani awadanganye kama alivyofanya kwa Hawa katika bustani ya Edeni. Ebu sisi sote na tujitoe upya katika majukumu tuliyopewa na Mungu. Yana uzito mkubwa – ya thamani kubwa na yamekamilika. Na tuifurahie hekima ya Mungu, upendo wake kwetu na Baraka za rohoni anazowakirimu wanawake wote ambao wanampenda kweli.

Maombi yangu yasiyokoma ni tupate ukombozi salama watu wa Mungu tutakaposhinda vita dhidi ya Shetani siku ya mwisho! Tutashangilia ushindi na kuingia katika furaha isiyoelezeka ambayo Mungu amewaandalia wampendao. Mwanamke wa Mungu lazima amsifu yeye kwa neno lake zuri ajabu na mpango wake usiobadilika.

**Samuel Matthews ni mmisionari wa kanisa la Bwana huko St. Thomas, katika visiwa vya Virgin.**

**Mpango wa Mungu mkamilifu tangu uumbaji**: BWANA Mungu akamfanya mtu kwa mavumbi ya ardhi, akampulizia puani pumzi ya uhai; mtu akawa nafsi hai (Mwanzo 2:7). Bwana Mungu akasema, "Si vema huyo mtu awe peke yake, nitamfanyia msaidizi wa kufanana naye" (18) BWANA Mungu akamletea Adamu usingizi mzito, naye akalala, kisha akatwaa ubavu wake mmoja akafunika nyama mahali pale, na ule ubavu alioutwaa katika Adamu BWANA Mungu akaufanya mwanamke, akamleta kwa Adamu. (21-22). Kwa hiyo mwanaume atamwacha baba yake na mama yake naye ataambatana na mkewe, nao watakuwa mwili mmoja. (24).

# Mwanafunzi ni Nani?

Donny Weimar

Kwa ufupi, Agizo Kuu la Yesu ni ***"enendeni mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi"*** (Mathayo 28:19). Roho zilizoongolewa kama hizo zilikuwa zaidi ya waongofu, ni zaidi ya wanafunzi wa shule. Wanafunzi huketi mbele ya mwalimu wao kwa lengo tu la kujifunza



jambo analolinena, lakini wafuasi ni zaidi ya wanafunzi. Ah! Sadakta, hakika wao hujifunza kwa Mkuu wao, lakini kubwa zaidi, huiga mfano wake kisha nao wanakuwa waalimu. ***"Mwanafunzi hawezi kumpita mwalimu,"*** Yesu aliwaambia, ***"lakini kila mtu ambaye amehitimu hulingana na mwalimu wake"*** (Luka 6:40). Hufanana na mwalimu wake – hufanana na Yesu Kristo – ni lazima awe amejifunza kikamilifu ili aige tabia halisi za Yesu, maisha aliyoishi.

*Mambo matatu* kwa habari za wanafunzi, kama yalivyoainishwa katika Injili ya milele ya Yohana. Mosi, walikaa katika mafundisho ya Kristo. Yesu aliwaambia waaminio ***"Mkikaa katika neno langu mmekuwa wanafunzi wangu kweli kweli"*** (Yohana 8:31). Mtu asiyeielewa Biblia yu tupu asiye na imani sahihi kwa sababu, ***"imani huja kwa kusikia neno la Kristo"*** (Warumi 10:17).

Wanafunzi **hupendana wenyewe**. Mwalimu alifafanua, ***"Hivyo watu wote watatambua ya kuwa ninyi mmekuwa wanafunzi wangu, mkiwa na upendo ninyi kwa ninyi"*** (Yohana 13:35). Mkristo asiye na upendo, si mwanafunzi wa kweli (1 Yohana 4:20). Watoto wa Mungu wanaelewa upendo wa kibiblia, kwa kuwa **"Mungu ni upendo"** (1 Yohana 4:8). ***"Katika hili tumelifahamu pendo, kwa kuwa yeye aliutoa uhai wake kwa ajili yetu; imetupasa na sisi kuutoa uhai wetu kwa ajili ya hao ndugu"*** (1 Yohana 3:16).

Wanafunzi wa Yesu **huzaa matunda**. *"Hivyo hutukuzwa Baba yangu kwa vile mzaavyo sana; nanyi mtakuwa wanafunzi wangu"* (Yohana 15:8). Kuzaa matunda katika Biblia kunamaanisha imani yenye tija. Imani ya namna hii huzaa matunda ya aina mbili: *tunda la haki* (Yakobo 3:18) na *kuleta wanafunzi wengi kwa Bwana* (Wafilipi 1:22). Kila kiumbe hai huzaa na kuongezeka (Mwanzo 1:22). Kuzaa matunda ndio alama muhimu ya kuwatambua wanafunzi wa kweli.



Ili tuwe wanafunzi wa Yesu hatuna budi **kujifunza kwake kumuiga** na **kuwashirikisha** wengine injili yake. Wanafunzi hutafuta wanafunzi, wanaotafuta wanafunzi. *"....Na mkiwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi"* (Mathayo 28:20).

**Donny Weimer anafanya kazi na kanisa la Kristo huko Valley Mills, Texas, Marekani.**

# MWAMINIFU DAIMA

David A. Sargen

Askari Mwanamaji wa Marekani Caleb Earwood alitaka kupata wasaa na mchumba wake Maggie kabla ya sherehe ya arusi yao Jumamosi ya tarehe 23/5/2015. Kadhalika, walitaka wasivunje miiko kuhusiana na bwana arusi kutomwoona bibi arusi kabla ya kuoana siku ya arusi.

Muda mfupi kabla ya sherehe ya arusi haijaanza huko Asheville, Carolina ya Kaskazini, Caleb aliongozwa hadi kibanda ambacho Maggie alikuwa akimsubiri. Bila ya kumwangalia na kukiuka maekezo ya tamaduni zao, akarudi kinyume-nyume katika mlango uliokuwa wazi mahali aliposimama bibi arusi. Aliufikia mkono wake akaushika. Walipokuwa wameshikana mikono na kuinamisha vichwa vyao katika mwelekeo tofauti, Caleb akawaongoza wote katika sala kwa Mungu akiomba baraka zake katika ndoa yao. Caleb akaomba kwa ajili ya ndoa ya wawili hao, akiomba kwamba ndoa yao iwe imara kiasi cha kuwa kielelezo kwa wanandoa vijana. Maggie alikuwa akijaribu kujizuia machozi yasitoke. “Niliishiwa nguvu kabisa” Maggie alisema, “kujua kuwa sisi sote tulifikiri mamoja kuhusu Mungu. Nikafurahi sana.”

Kwa pamoja tulikuwa tumekaribia kuchukua hatua ya kwanza kabisa katika maisha, na hatukutaka kufanya hivyo bila ya kuwa katika mapenzi ya Mungu,” Caleb Earwood, 21, katika tovuti: TODAY.com.

Kuomba Baraka za Mungu pamoja na ndoa ya mtu kujengwa juu ya Mungu na Neno lake huo ndio msingi wa ndoa imara pia zinazodumu. Hakika, ni jambo muhimu sana kwa mwanandoa – YEYOTE na asiye na ndoa, kijana au mzee – kujenga maisha yao juu ya mwamba wa Yesu Kristo. *“Basi kila asikiaye maneno yangu na kuyafanya, atafananishwa na mtu mwenye akili, aliyejenga nyumba yake juu ya mwamba, mvua ikanyesha, mafuriko yakaja, pepo zikavuma zikaipiga nyumba ile, isianguke; kwa maana misingi yake imewekwa juu ya mwamba”* (Mathayo 7:24-25).

Dhambi zetu hutuhukumu (Warumi 6:23), lakini Mungu ***“Hapendi mtu yeyote apotee, bali wote wafikilie toba”*** (2 Petro 3:9). Alimtoa

mwanawe ili afe kwa ajili yetu tupate kuokolewa na kuruzukiwa kipawa cha uzima wa milele (Yohana 3:16).


Kama Caleb alivyoomba, usichukue hatua yoyote bila ya hatua hiyo kuwa katika mapenzi ya Mungu. Yesu alisema, "***Kwa kuwa mapenzi yake Baba yangu ni haya, ya kwamba kila amtazamaye Mwana na kumwamini yeye, awe na uzima wa milele; nami nitamfufua siku ya mwisho***" (Yohana 6:40).

Ni mapenzi ya Mungu kwamba kila mmoja wetu "amwangalie Mwana" na kujenga imani na tumaini letu kwake (Matendo 16:30-31), tuziache dhambi zetu na kutubu (Matendo 17:30-31), tumkiri Yeye mbele za watu (Warumi 10:9-10) na kubatizwa (kuzamishwa) kuingia katika Kristo ili tupate msamaha wa dhambi zetu (Matendo 2:38). Hao wanaopenda kufuata mapenzi yake na kupokea karama yake ya wokovu kwa majira yake watapokea msamaha wa Mungu na karama ya uzima wa milele (Warumi 6:23). Wale watakaodumu kutenda mapenzi yake wakiwa na msimamo wa kuwa "waaminifu siku zote" damu ya Yesu daima itaendelea kuwatakasa (1 Yohana 1:7).

Je, wewe hutayazingatia mapenzi ya Mungu?

**David A. Sargent mhubiri wa kanisa la Kristo huko Creekwood, Mobile, Alabama, Marekani.**

## Rubi za Robinson



Nabii wa Agano la Kale Yeremia aliishi **miaka mingi hata** Yerusalemu ulipobomolewa na majeshi ya **Babeli mwaka 589 K.K.** Alitumwa na Mungu kuwatabiria watu **ambao walijinajisi katika maovu** mengi, wakijiletea hukumu juu yao **wenyewe. Katika Yeremia 2:13 alitoa** taswira "Kwa maana watu wangu **hawa wametenda maovu mawili;** wameniacha mimi niliye chemchemi **ya maji ya uzima, wamejichimbia** mabirika, mabirika **yavujayo, yasiyoweza kuweka maji."**

Watu katika tamaduni mbalimbali wanakataa maadili mema na maelekezo ya Mungu, bila kujua kwamba hayo ndiyo maongozi ya maisha yaletayo uzima na furaha – maana ndio chemchemi yenye maji ya uzima. Wakati huo huo, wanabuni njia zao wenyewe, ambazo huwafanya wakate tamaa na kupotoka –mabirika ambayo hayawezi kuhifadhi maji. Njia za Mungu pekee ndiyo hutoa uzima, amani na matumaini!

## Nyumba ya Kikristo

# Kuishi kwa Kiasi kwa Ajili ya Kristo

Martha Lynn Rushmore

Tunapofanyika Wakristo, tunautangazia ulimwengu kwamba mimi maisha yangu ni kwa ajili ya Kristo na si kwa ajili ya Shetani. Ninakwenda kuishi na kutenda tofauti na nilivyokuwa hapo kabla sijamvaa Kristo katika ubatizo.

Ni namna gani wewe unaishi kwa ajili ya Kristo ukiwa mwanamke Mkristo? Pengine wewe ni binti, mke, mama, mama mkwe, au bibi? Tukiwa wanamke Wakristo, tunaweza kuwa zaidi ya mambo yaliyotajwa hapo juu kwa wakati tutakaojaliwa. Hatuna budi kukumbuka namna tunavyoishi na kutenda, ili watu wajue kama tunaishi kwa ajili ya Kristo au kwa ajili ya Shetani! Tunatazamwa na familia zetu, marafiki, jamaa wanaotujua, majirani pia hata hao ambao hatujawahi kukutana nao kabla. Ebu na tutafakari, tutende na kuishi kama Kristo alivyoishi. Kwa kijana wa kike kuishi kwa ajili ya Kristo ni vigumu kwa sababu mtu anawataka anaosoma nao na hasa vijana wa kiume wampende. Wakati mwingine tunataka marafiki zetu watuone sisi maarufu huku wakituongoza kuelekea njia mbaya ya maisha. Tunavaa au niseme hatuvai, kuvinjari mahali na kufanya mambo ambayo hayafai kwa Wakristo. Tunapaswa kuwashawishi marafiki zetu kwa mazuri badala ya wao kutuvuta sisi tufafanane zaidi na ulimwengu. Isivyo bahati, mavazi yetu yanayoacha mgongo na kifua wazi, mavazi yenye kuacha tumbo wazi, yenye kamba-kamba kama tambi, kaptula fupi au sketi fupi. Wakati mwingine, tunaweza kuvaa suruali ambazo zinabana kiasi kwamba hakuna kilichositirika kwa vijana wa kiume na wanaume. Isivyo bahati, hili linawalenga wanawake wa rika zote, wawe wembamba au wanene. Aina hii ya mavazi ni dhambi kwa sababu si mavazi ya kujisitiri. Katika 1 Timotheo 4:12, Paulo anawaandikia vijana, *"Mtu awaye yote asiudharau ujana wako,*



*bali uwe kielelezo kwao waaminio, katika usemi na mwenendo, na katika upendo na imani na usafi."* Vijana wadogo, unaweza kuwa na ushawishi mkubwa kwa watu wazima – pia hata kwa umri-rika lako.

Isivyo bahati, akina baba na akina maama hawawafundishi vijana wao wa kike jinsi ya kuvaa vizuri. Wasichana wanaruhusiwa kuondoka majumbani mwao wakiwa wamevaa vibaya. Sisi kama wazazi tuna jukumu kubwa la kuwafundisha vijana wetu namna gani na kwanini wanapaswa kuvaa vizuri. Sisi kama wazazi tunapaswa kuwaongoza vijana hawa wa kike kujiheshimu wenyewe na zaidi ya yote kuliheshimu Neno la Mungu. Kwa hiyo, wazazi wanapaswa kuvaa kwa kujisitiri, pia, hatuwezi kutarajia vijana wetu wavae vizuri ikiwa sisi wazazi hatuwafundishi wala hatuonyeshi kielelezo sahihi.

Timotheo wa Kwanza 2:9-10 tunasoma, *"Vivyo hivyo wanawake na wajipambe kwa mavazi ya kujisitiri, pamoja na adabu nzuri, na moyo wa kiasi; si kwa kusuka nywele, wala kwa dhahabu na lulu, wala nguo za thamani; bali kwa matendo mema, kama iwapasavyo wanawake wanaoukiri uchaji wa Mungu."* Fasili ya neno kujisitiri haina maana tuvuke mipaka kiasi cha watu kutushangaa. Tunapaswa kuvaa kwa namna ambayo inadhihirisha utauwa. Mstari huu ni kwa wanawake wote wa kila rika na ni kwa wanawake wote ulimwenguni.

Wanawake wazee wanapaswa kuwafundisha wanawake vijana kwa njia ya maelekezo na kwa mifano. Paulo aliandika katika Tito 2:3-5, **"*Vivyo hivyo na wazee wa kike wawe na mwenendo wa utakatifu; wasiwe wasingiziaji, wasiwe wenye kutumia mvinyo nyingi, bali wafundishao mema; ili wawatie wanawake vijana akili, wawapende waume zao, na kuwapenda watoto wao; na kuwa na kiasi, kuwa safi kufanya kazi majumbani mwao, kuwa wema, kuwatii waume zao wenyewe; ili neno la Mungu lisitukanwe."***

Akina mama, ebu na tuuvae utakatifu – tuishi kwa ajili ya Kristo na wala tusiishi kwa ajili ya shetani. Roho zetu hutegemea namna tunavyoishi! Roho za mabinti zetu zinaweza vilevile kutegemea namna tunavyoishi.

**Martha Lynn Rushmore ni mwandishi katika jarida la Sauti ya Kweli Kimataifa na Gazette Online. Yeye na mumewe ni waalimu wa injili. Wanaishi huko Winona, Mississippi, Marekani.**

# "Ole Wangu Bwana Wangu, Kwani Kiliazimwa!"

Michael L. King



Haya ni mafunzo muhimu sana katika Agano la Kale ambayo yanafundisha ukweli fulani wa Agano Jipya. Wana wa manabii waligundua kuwa mahali walipoishi palikuwa padogo walipokuwa wakijifunza ili wawe manabii. Walimjia Elisha ("mtu wa Mungu") na kumwomba ruhusa kwenda mto Yordani na kukata boriti na kupanua makazi yao ili yafae kwa kuishi. Ruhusa ilitolewa, na mmoja wao alipokuwa akikata mti, chuma cha shoka kikaanguka na kuzama majini. Kijana yule mdogo aliingiwa na hofu na kusema, *"**Ole wangu, Bwana wangu! Kwani kiliazimwa**"* (2 Wafalme 6:1-7). Aliingiwa na hofu isio ya kawaida maana shoka halikuwa lake, isipokuwa liliazimwa kutoka kwa mtu mwingine. Lingekuwa lake, asingewajibika kwa mtu yeyote

zaidi ya yeye mwenyewe. Jambo hilo lilipotukia Elisha alipewa taarifa, aliuliza ni wapi kilipoanguka. Kijana huyo mdogo aliamuriwa akate kijiti na kukitupa juu ya maji. Alipofanya hivyo, chuma kikaibuka na kuelea.

Leo tunapaswa kuingiwa na hofu nyingi sawa na hiyo tunapotafakari wajibu tulio nao wa "…kuwalea watoto wetu katika adabu na maonyo ya Bwana" (Waefeso 6:4). Hakikisha hatuwatekezi kama Eli kwa kutozuia uovu wake, wala uovu wa wanae (1 Samweli 3:13). Uzito huo huo tunapaswa kuubeba tunaposoma tena "Agizo Kuu" katika Mathayo 28:18-20, Marko 16:15-16 na Paulo anasisitiza kuwa ni wajibu wa kanisa kuitangaza hekima ya Mungu iliyo ya namna nyingi ijulikane ulimwenguni (Waefeso 3:10). Katika vifungu hivi vyote kazi tuliyoachiwa ni kuziokoa roho za wanadamu. Tuna muda mfupi tu wa kuwaandaa kwa ajili ya safari yao ya milele.

Roho hizi "tumeazimwa" na ni lazima zirudishwe kwa Bwana zikiwa na hali nzuri kuliko tulipoziona. Mwandishi huyu anazingatia sana tunapoazima kitu, tunakisafisha au kukirekebisha kabla ya kukirejesha, kwa kufanya hivyo tunaonyesha shukrani zetu kwa kukitumia kitu hicho na kujenga imani kwa mmiliki. Unajuaje, pengine tutahitaji tena huduma ya kitu hicho siku zijazo.

Watoto wetu tumeazimwa, ni lazima baadaye warejee kwa Mungu. Hali ya kujali lazima ionekane ili kuzuia wasije "wakapotea." Tunawasaidia kwa kujenga uhusiano na Mungu kupitia mafundisho yetu, kuwashauri na kuwa vielelezo kwao. Tumeelekezwa "***kuwalea***" (Mithali 22:6). Paulo anafafanua zaidi wazo hilo kwa kuyafanikisha mafunzo haya anaposema, *"**Katika adabu na maonyo ya Bwana**"* (Waefeso 6:4). Sehemu ya mafunzo haya ni kuwazuia "***wasifanane na ulimwengu***" (Warumi 12:2). Madhumuni hasa ya kutia kila juhudi katika kazi hii ni kuwasaidia "**wamshinde yule mwovu**" (1 Yohana 2:14). Paulo alimwonya kijana Timotheo kuwa tayari na adabu kuhakikisha kwamba ***"…kuendelea kwako kuwe dhahiri kwa watu wote." "Jitunze nafsi yako na mafundisho yako. Dumu katika mambo hayo, maana kwa kufanya hivyo utajiokoa nafsi yako na wale wakusikiao pia"*** (1 Timotheo 4:12-16).

Roho hizo za thamani, na hakika zina thamani kubwa (Marko 8:37), zinapaswa ziushuhudie upendo wa kweli, kutii mamlaka, unyenyekevu (kwa Mungu, mwanadamu, mume, mke, Mkristo

mwenzako, n.k.), furaha, matumaini, nidhamu, imani na kadhalika. Sifa zote hizi zitatakiwa Mbinguni, na ebu fikiria ni jinsi gani zinaweza pia kuyabadilisha maisha yakawa mazuri zaidi hapa.

Kanuni ambayo tunapaswa kuitafakari tunaposhika “shoka” letu ili kuwajibikaji kwa kila hali tunapotumia kitu tulichoazima, ni kutambua kwamba kanuni ya kupanda na kuvuna inaonekana. Tunaweza kuzalisha au kupata tu kulingana na mbegu au miche tuliyopanda na kuitapanya. Neno la Mungu ndio hiyo mbegu, na ukuaji wake umechochewa na usambazaji wa mpanzi mwenye uelewa (Mathayo 13:18-23). Nukuu inasema, “Siwezi kusikia unachoniambia, kwa sababu unachofanya kinanizuia nisisikie!” Pia, mtu mmoja alitoa kauli inayofurahisha kukazia umhimu wa kuwa kielelezo: “Hubiri neno ulimwenguni kote, ikiwa njia nyingine haipo, tumia maneno!”

Kama vile Mungu alivyomwezesha Elisha kupandisha na kukirejesha kichwa cha shoka kikiwa hali ya “kuokolewa” na kutumika, anaweza leo hii kuyafanya upya maisha katika mioyo ya waume kwa wake ambao vinginevyo wangepotea na kutofaa kitu. Kumbuka kwamba tutawajibika kwa hicho tulichoaminiwa tukitunze pamoja na mambo yetu wenyewe. Kama tukifundisha na tukakataliwa, atakayewajibika ni msikilizaji; iwapo hatutafundisha basi, “***roho na damu yake nitavitaka mikononi mwetu***” (Ezekieli 3:16-18). Sisi ni “walinzi” tukihakikisha kwamba kile tulichokiazima hakuna tunachokipoteza!

# Je, Unajua?

Rebecca Rushmore

Sehemu ya juu ya Bahari Mfu, inayoitwa Bahari ya Chumvi katika Mwanzo 14:3, ndio eneo la chini kabisa duniani katika usawa wa bahari takribani futi 1300 chini. Kina chake cha chini kabisa ni takribani futi 1300 kwenda chini. Ni karibu maili 50 urefu na maili 10 upana, ingawa vipimo hivi vinatofautina kulingana na kiasi cha mvua na sababu zingine.



# Mali Zenye Thamani

Charles Pugh III

Biblia ni kitabu chenye maneno mazito sana. Moja ya maneno haya yaliyotafsiriwa katika Kiswahili ni neno "thamani." Petro amelitumia neno hili mara nyingi katika nyaraka zake mbili. Neno hili ni "*timios*" kwa Kiyunani linarejea kitu "kinachoonekana cha thamani sana, kinachoheshimika sana, kilicho ghali mno, hata kinachopendwa zaidi" (Thayer 624). Petro alilitumia neno hili akirejea baadhi ya vitu vyenye thamani, vilivyo ghali mno kwa Mkristo. Angalia vifuatavyo.

**Imani ya thamani** (1 Petro 1:7; 2 Petro 1:1). Petro anasema imani hii ina thamani kuu kuliko dhahabu. Hii si kila imani, bali ni "***imani moja***." Ni ya thamani kwa sababu ya mtu aliye kiini cha imani hiyo (1 Petro 1:8), **furaha** iliyomo ndani yake (1 Petro 1:8) na matarajio yaliwekwa humo (1 Petro 1:9). Ikiwa una imani hii katika Mungu, Yesu na Biblia, ilinde, imarisha, ipiganie na ifie. Ni huzuni kubwa kuona mtu anaiacha imani hii ya thamani kuu iende zake ipotee.

**Damu ya thamani** (1 Petro 1:18-19). Hiki ni kito cha thamani kwa sababu ya jinsi ilivyo – damu. Uhai hupatikana katika damu kimwili na kiroho (Walawi 17:11; Waebrania 9:22). Ni ya thamani kwa sababu ya aina hiyo ya damu – haiharibiki (si kitu cha kuoza). Ni ya thamani kwa sababu ya **nani mwenye** hiyo damu – damu ya Kristo kama ya mwanakondoo asiye na ila au waa. Ohoo, ni ya thamani hakika itiririkayo kama theluji nyeupe!

**Ahadi ya thamani** (2 Petro 1:4). "Kushikilia ahadi ambapo hatuwezi kuvunjika moyo pindi mawimbi ya mashaka na hofu yanapovuma; kwa njia ya Neno la Mungu lililo hai nitashinda, nitashikilia ahadi za Mungu."

**Imani ya thamani** – **damu ya thamani** – **ahadi za thamani**. Hakika ni mali zenye thamani kuu!

**Charles Pugh anahuduma ya uandishi na anaishi huko Vienna, West Virginia, Marekani.**

# Muonekano wa Ubaya

T. Pierce Brown

Tangu nilipokuwa mtoto mdogo, nimekuwa nikimsikia mama yangu na watu wengine wema kadhaa wakifundisha, "***Jitengeni na ubaya wa kila namna***." Katika muda huo wote, mhubiri aliyeonyo, kwa kawaida aliongeza, "1 Wathesalonike 5:22." Kumbukumbu zangu pia zinaniambia nimesoma mara nyingi kwenye Bibia "Jiepusheni na aina yote ya ubaya," lakini hakuna tafsiri ya toleo lolote lile inalosema hivyo, basi nikahitimisha kwamba kumbukumbu zangu zimekosea. Sasa, ninaamini kabisa, kwa mantiki kidogo niliyojaliwa, na ufahamu wangu katika Biblia, kwamba ni wazo jema kujiepusha na vitu **vinavyoonekana** kuwa ni viovu. Vile vitu ambavyo kwa kawaida vinatiliwa mashaka havipaswi kufanywa. Pengine sababu zinaweza kutolewa za kulazimisha sababu ya kutenda katika baadhi ya mazingira. Kwa mfano, sidhani kama ni sahihi kwenda katika klabu ya pombe au nyumba yenye sifa mbaya, kwa kawaida, nitafanya hivyo tu ikiwa nadhani roho inaweza kunyakuliwa humo na kuokolewa kwa sababu ya mimi kuingia humo.

Karibia kila mtu ambaye nimemsikia akinukuu au kunukuu vibaya 1 Wathesalonike 5:22 alifanya hivi akiwa na wazo hili akilini mwake: "Usijitenge tu na chochote kilicho kibaya, unapaswa kujitenga na chochote kinachodhaniwa au kinachoonekana kibaya. Kwa hiyo Maandiko haya yalitumika kutetea mgogoro huu. Hoja ni hii, Maandiko haya hayamaanishi hivyo. Kwa sehemu utata huu umesababishwa na ukweli kwamba katika Kiingereza neno (*appear*) "onekana" lina maana walau mbili. Ikiwa tutasema, mtu anaonekana na sura ya hasira," kwa kawaida tunamaanisha kwamba sisi kwetu alionekana ana hasira. Ni sawa na kusema, "alijitokeza akiwa na hasira." Ikiwa tutasena, "Mtu huyu alionyesha uso wa hasira," tunamaanisha kwamba alikuwa na hasira, alijitokeza katika tukio akiwa hivyo – haina maana tu kwamba alidhaniwa kuwa hivyo. Ni sawa na kusema, "Alijitokeza, akiwa na hasira." Angalia alama ya mkato [katika Kiingereza]. Sioni mfano kwenye Biblia wa neno lililotumika katika 1 Wathesalonike 5:22,

lililotafsiriwa kwa Kiingereza "*appearance,"* likimaanisha "*seemed to be."*

Kwa kuwa najua kwamba Biblia inafundisha katika Warumi 14:14, *"Lakini kwake yeye akionaye kitu kwake kuwa najisi, kwake huyo kitu kile ni najisi"* na katika mstari wa 23, "*lakini aliye na shaka, kama akila, amehukumiwa kuwa ana hatia kwa maana hakula kwa imani,*" sichelei kufundisha kwamba kuanzia Hawa na kuendelea ingekuwa heri hata kutoikazia macho dhambi, "***kujongeza hema mpaka Sodoma***," "***kwenda katika shauri la wasio haki***," "***kusimama katika njia za wakosaji***," au "***kuketi barazani pa wenye mizaha***." Lakini, nahisi bila kuyumba kwamba sisi tunaoihubiri injili tunawajibu wa kuhakikisha kwa kadri tuwezavyo kwamba hatunukuu vibaya neno la Mungu wala hatupotoshi kile tunachokinukuu sawasawa ili kubainisha ukweli. Kipengele ambacho hakijathibitika wala kufafanuliwa na fungu la Maandiko hakifai kutetewa.

Fungu la Kiyunani katika 1 Wathesalonike 5:22 linasomeka, "***apo pantos eidous ponerou apechesthe***." Hili linaweza kutafsiriwa "epuka uovu wa kila aina." "*Edious*" kisarufi ni kihusishi cha umoja umiliki cha "*eidos*,"ambacho kimetafsiriwa katika (*UVS*) Kiswahili "uso" mara mbili (Luka 9:29; Yohana 5:37), "mfano, mara moja (Luka 3:22) na "kuona" (2 Wakorintho 5:7). Hakuna mahali nimeona likitumika kwa maana ya kitu ambacho kimedhaniwa tu. Katika *ASV* na *RSV* limetafsiriwa "Jitengeni na ubaya wa kila namna." *William* ametafsiri "Daima jitengeni na kila aina ya uovu." *Philips* anasema "Jiepusheni na uovu wa kila namna." *Biblia ya Amplified* inasema "Jitengeni na uovu – kaa mbali na usikaribie – uovu uwao wote." "Toleo la Berkeley linasema "Kaa mbali na uovu wa aina yoyote." *Beck* anasema "Kaa mbali na ubaya wa kila namna." Ni katika Agano Jipya tu katika tafsiri ya *Monsignor Ronald Knox* nimeona ametafsiri hivi, "Uvikatae vitu vyote vinavyoonekana viovu."

Ikiwa mtu yeyote anajua sababu yoyote kwa nini tunukuu vibaya au kutumia vibaya fungu hili au Maandiko mengine yoyote ili kutetea hoja, bila kujali uzuri wa hoja, nitafurahi kusikia kutoka kwake.

**T. Pierce Brown aliishi (1923-2008) na kuhubiri huko Cookville, Tennessee, Marekani.**




# Msaka Tonge

**Kupitia Ezra**

**Rebecca Rushmore**

1. Ni mwaka upi katika utawala wa Koreshi Wayahudi waliruhusu kurejea Yerusalemu ili kulijenga upya hekalu?
2. Ni mfalme yupi wa Babeli aliutwaa [ufalme wa] Yuda utumwani?
3. Kundi lililorejea Yerusalemu lilikuwa na watu wangapi?
4. Pia ni waimbaji na watumishi wangapi walirejea?
5. Wanaume walioliona hekalu la kwanza walifanya nini pindi msingi wa hekalu jipya ulipowekwa?
6. Tamko la Dario lilisema nini kingemkabilia mtu atakayebadili amri yake kwa habari ya ujenzi wa hekalu?
7. Ni katika mwaka upi wa utawala wa Dario hekalu lilikamilika?
8. Ezra alikuwa na kazi gani?
9. Ni kwa amri ya mfalme yupi Ezra alikwenda Yerusalemu?
10. Ni amri gani ilitolewa kwa wanaume waliowachukua wanawake wageni kuwa wake zao?

# Mwizi Msalabani

Steve Higginbotham

Siku ambayo Yesu alikufa ndio siku ambayo viumbe vilimsulubisha Muumbaji. Lakini, kutokana na hekima ya Mungu kuonekana upuuzi, Mungu alitumia tukio hilo baya la kuchukiza ili kutupatia uhai! Si tu kwamba Yesu alitundikwa katika msalaba ulikuwa katikati, lakini alifanya hivyo kwa ajili ya tumaini la kila mwanadamu. Wakati huo, yapo matukio yaliyotokea siku hiyo, bila shaka yalitukia kipindi muhimu sana katika historia.

Lakini, sababu ikiwa ni hiyo, kwanini habari za kifo cha Yesu ziunganishwe pamoja na habari zisizoshabihiana za mwizi ambaye naye alikufa siku ile? Hakika, ipo habari nzito sana hapa ya kifo cha Yesu kuliko kupoteza wino kuandika kifo cha mwizi alichostahili.

Vema, pengine nishauri kwamba kifo cha mwizi si tukio ndogo lisilo na umhimu, **lakini yeye ni** sehemu mhimu ya simulizi nzito zaidi? Unaona, msalaba wa Yesu unatangaza upana na kina cha upendo wa Mungu ambapo alikuwa yu tayari kumtoa Mwanawe wa pekee (Yohana 3:16). Hata hivyo pamoja na tangazo hilo, ni tangazo toka msalabani ambapo mwizi alikufa. Msalaba huo ulitangaza upeo wa upendo wa Mungu.

Ujumbe kutoka msalaba wa mwizi unatuambia sisi sote tunaoteswa na hatia huku tukipoteza muda mwingi dhambini katika maisha haya. Msalaba unaongea na hao waliosubiri kwa muda mrefu kujikabidhisha kwa Yesu. Ni ujumbe kwa hao wanaongojea muda mrefu kujisalimishe maisha yao kwa Yesu. Ni ujumbe kwetu sisi sote ambao hatuna cha kumtolea Mungu isipokuwa kuomba radhi. Msalaba wa mwizi unatangaza kwamba Mungu ni Mungu wa rehema!

Natumaini tunaweza kupata amani katika ukweli huu. Bila ya msalaba wa Yesu hakuna tumaini. Kwa kuongezea, bila msalaba wa mwizi, pengine tungetilia mashaka huo ukombozi aliotukirimia Yesu kwamba ungenikomboa hata mimi mwenye dhambi!

Mwizi msalabani alipokuwa hana cha kumpa Mungu isipokuwa kuomba radhi, Yesu alimwaahidi Paradiso! Wewe mshukuru Mungu kwa wokovu uliolipiwa gharama msalabani na Kristo, na pia kwa matumaini ya kwamba umefafanuliwa kwa msalaba wa mwizi.

# Watu waliosahaulika katika Biblia: Yusufu

Rebecca Rushmore

Wapo wahusika wa Biblia kadha wa kadha ambao tunawafahamu zaidi. Watu kama hao ndio wanaozungummzwa mara nyingi katika masomo mbalimbali na pengine kitabu au sura zote za kitabu zikijadili habari zao. Wapo watu wengine wametajwa katika Biblia ambao tuna habari chache sana. Watu hao wanaweza tu kutajwa kwa ufupi au wanapatikana sehemu moja au mbili katika Biblia. Mara nyingi watu hao hawazungumziwi kabisa, ingawa wanajitokeza ndani ya Biblia zetu kwa makusudi.

Yohana 20:30-31 panatuambia kwamba Yesu alifanya mambo mengi ambayo hayakuwandikwa katika Biblia. Mambo ambayo yameandikwa ni kwa ajili ya kuimarisha imani yetu. 2 Timotheo 3:16 panasema kila jambo lililomo ndani ya Biblia limetoka kwa Mungu na ni kwa ajili yetu sisi kujifunza. Tukiwa na hili akilini mwetu, hapana shaka kwamba hao tuliopewa habari zao kwa uchache, “waliosahaulika” waume kwa wake katika Biblia wanaweza kutufundisha masomo muhimu sana leo.

Karibu watu wengi wanapowaza habari za Yusufu wa Biblia, inawezekana wakafikiri juu ya Yusufu wa Agano la Kale. Hata hivyo, wapo watu wengine wawili walioitwa Yusufu. Wa kwanza ni baba mlezi wa Bwana wetu. Wa pili alimzika Bwana wetu katika kaburi lake.

## Baba wa Yesu

Kwanza mwangalie Yusufu, baba mlezi wa Yesu. Mtu huyu ametajwa kwa ufupi sana katika Biblia. Katika Mathayo 1:16-24, tunaweza kusoma habari kuhusu mazingira yaliyozunguka kuzaliwa kwa Yesu. Kifungu hiki kinatuambia kwamba Yusufu alimchumbia Mariamu. Hiki kilikuwa kipindi cha uchumba kabla ndoa halisi kufungwa. Bibi arusi mtarajiwa alibaki na wazazi wake, lakini machoni pa sheria, wawili hao walikuwa wameoana (Kumbukumbu 22:23-24); ili kuvunja uchumba huu hati ya talaka ilihitajika.

Ni katika kipindi hiki Mariamu alichukua mimba ya Yesu kwa uwezo wa Roho Mtakatifu. Yusufu, asijue baba halisi wa mtoto, alidhania hakuwa mwaminifu. Alimpenda Mariamu vya kutosha kiasi kwamba hakutaka kumwaibisha hadharani. Mwanamke aliyeposwa asiyemwaminifu adhabu yake ilikuwa kupigwa mawe hadi kufa (Kumbukumbu 22:23-24). Badala yake Yusufu akataka kumtaliki kwa siri kwa mujibu wa sheria (Kumbukumbu 24:1). Mungu akamtokea Yusufu katika ndoto na kumwamuru kukamilisha hatua za kumwoa Mariamu.

Mathayo 2:13-15 na 2:19-23 inasimulia kisa cha pili na cha tatu habari za Yusufu. Katika matukio yote mawili, Mungu alimtokea tena Yusufu katika ndoto. Katika ndoto ya kwanza Yusufu aliambiwa akimbie na familia yake hadi Misri, na katika ndoto ya pili aliambiwa ni salama sasa kurejea nyumbani. Katika fungu letu muhimu tunalolijadili linapatikana katika Luka 2:4-7. Hapa tunamwona Yusufu na Mariamu wakisafiri kwenda Bethlehemu kuhesabiwa kwa amri ya Kaisari. Wakiwa huko Bethlehemu ndipo Yesu akazaliwa. Mstari wa 16 wa sura hiyo hiyo unamtaja Yusufu akiwa na wachungaji walipofika kumwona Mwokozi. Luka 2:22-39 panaelezea Yusufu na Mariamu wakitenda yaliyoamuriwa wakimkabidhi [kwa Bwan] mtoto na kutoa dhabihi hekaluni (Walawi 12:1-8). Tena tunasoma kuhusu Yusufu katika Luka 2:41-51akifanya safari yake ya kila mwaka kwenda Yerusalemu kwa ajili ya Pasaka, Yesu akiwa na umri wa miaka kumi na miwili. Yusufu ametajwa mahali pengine kwa majina mara tatu tu katika Agano Jipya (Luka 3:23; Yohana 1:45, 6:42). Kila mahali hapo alipotajwa ni rejea kuwa Yesu alikuwa "*mwana wa Yusufu*."

**Kwa ujumla, hatuna habari nyingi kuhusu mtu aliyefanya kazi kubwa kama hiyo katika mpango wa Mungu kwa ajili ya wokovu wetu kupitia Kristo**. Tafakari kwa muda mafunzo ambayo tunaweza kujifunza kutoka kwa Yusufu "aliyesahaulika." Watu wengi leo wanamkumbuka Mariamu, mama wa Yesu. Msisitizo mkubwa ni juu ya namna alivyokuwa na haki hata kuchaguliwa na Mungu kuwa mama wa Bwana wetu. Ingawa ni nadra, tukiona jambo kama hilo likisemwa juu ya Yusufu. Kama ilivyo heshima kwa Mariamu kuwa mama, vilevile fikiria kuhusu heshima hiyo hiyo kupewa Yusufu.

Hapa kuna mtu aliyechaguliwa na Mungu kuwa baba wa Kristo duniani. Kama baba, Yusufu alimfundusha Yesu maana ya kuwa

mwaminifu kwa Mungu. Tunaona katika Biblia habari kwamba Yusufu alifundisha uaminifu kwa njia ya mfano. Yusufu alihakikisha kuwa mtoto wake akitahiriwa katika siku ya nane na ya kwamba mke wake anatoa dhabihu sahihi baada ya kuzaliwa kwake sawa na matakwa ya sheria. Kwa kufanya hivyo, Yusufu alikuwa kiongozi wa kidini wa nyumba yake. Tena, alidhihirisha uaminifu wake kwa safari zake za kila mwaka kwenda Yerusalemu kuadhimisha Pasaka. Sisi, kama vile Yusufu, tunapaswa kuwa waaminifu katika amri za Mungu. Wanaume wanapaswa kuhakikisha, kama Yusufu, wanakuwa viongozi wa kiroho katika nyumba zao.

Pia, kama Yusufu, tunapaswa kuwa tayari kutii amri za Mungu. Mungu alimtokea Yusufu ndotoni mara tatu akimpatia kazi ya kufanya. Kila wakati, Yusufu alikubali amri na kuitii mara moja. Yusufu ametajwa pia kuwa mtu wa "***haki***" (Mathayo 1:19). Alikuwa mwenye haki na aliishi kwa haki na kila mtu. Ni sifa hii iliyomfanya atamani adhabu ya siri yenye rehema kwa Mariamu. Hakutaka kumwaadhibu adhabu ya kifo ilhali hulka yake [Mariam] ilikuwa ya namna ambayo isingekuwa rahisi kupata mtoto kwa uasherati pengine mtoto wake alitokana na kubakwa. (Kumbukumbu 22:25-27). Kama Wakristo, tunapaswa tujulikane kwa haki zetu na kuwatendea wengine kwa adili. Kama vile Yusufu, hatuna budi kuwa tayari kusamehe na kuwa na huruma kwa wengine.

## Yusufu wa Arimathaya



Ingawa hatuna habari nyingi kuhusu baba mlezi wa Yesu, hata hivyo tunajua kidogo sana kuhusu Yusufu wa tatu katika Biblia – mtu aliyetoa kaburi kwa ajili ya Bwana. Baada ya kifo cha Yesu pale msalabani, mtu mmoja aliutaka mwili kwa ajili ya mazishi. Mtu huyo,

Yusufu kutoka mji wa Arimathaya, ametajwa sehemu nne tu katika Biblia (Mathayo 27:57-60; Marko 15:43-46; Luka 23:50-53; Yohana 19:38-42). Mafungu yote yanaelezea habari za mazishi ya Bwana wetu. Yusufu alikuwa mtu tajiri. Kaburi ambalo alimzika Bwana wetu lilikuwa lake, na lilikuwa jipya (Yohana 19:41; Mathayo 27:60). Mwili wa Bwana wetu ulizungushiwa kitani safi na kipya ambacho kilinunuliwa na Yusufu kwa kusudi hilo (Marko 15:46). Yusufu alitoa fedha zake, muda na eneo lake kwa ajili ya Bwana. Alifanya hivyo kabla hajajua hakika kuwa Yesu ni Mwana wa Mungu na angefufufuka toka kwa wafu. Sisi nasi tunapaswa kuwa tayari kufanya vivyo hivyo, hasa tunavyotambua kuwa Kristo ni Bwana na Mwokozi.

Yusufu pia alikuwa mwanachama wa *Sanhedrin*. Hili lilikuwa baraza la utawala la Wayahudi. Baraza hili ndilo lilimtafuta na kisha kumwua Kristo likimshitaki kwa madai ya kwamba yeye ni Masihi. Luka 23:51 panasema kuwa ingawa Yusufu alikuwa wanachama wa *Sanhedrin* hakukubaliana na shauri la kumwua Kristo. Hakika, alikuwa mmoja "aliyeutazamia ufalme wa Mungu" (Luka 23:51). Yusufu aliamini ahadi za Agano la Kale kwa habari ya Mwokozi na Masihi. Alitaka ifahamike kwamba hakukubaliana na Baraza dhidi ya Yesu. Ingawa Yohana 19:38 panasema kuwa Yusufu alikuwa mwanafunzi wa Yesu kwa siri kwa sababu aliwaogopa Wayahudi wengine, wakati hapakuwa na mtu mwingine yeyote wa kuuhifadhi mwili wa Bwana. Yusufu akajitokeza kufanya kazi hiyo, bila kujali nini kingempata. Sisi pia hatupaswi kusahau kutetea jambo la haki.

Yusufu wawili wote **waliosahaulika** katika Biblia wanaweza kutufundisha kuhusiana na maisha yetu kwa ajili ya Kristo. Baba mlezi wa Yesu na huyo aliyemzika Kristo wametajwa kuwa watu wenye "*haki*" (Mathayo 1:19; Luka 23:50). Walijitoa dhabihu wao wenyewe. Baba mlezi alijitoa akihatarisha jina lake kuchafuka kwa kumwoa mwanamke ambaye alionekana mzinzi na wengi siku hizo. Pia alitoa muda na kumwangalia mtoto ambaye si wake. Yusufu wa Arimathaya alitoa muda, fedha, eneo na inawezekana hadhi ya kazi na uhai wake kwa kuubeba mwili wa Yesu. Kama wakristo, tutafanya lililo jema sana tukiiga mfano wa watu hawa wa Biblia **waliosahaulika**.

**Rebecca Rushmore ni mwandishi katika jarida la Sauti ya Kweli Kimataifa na mwalimu wa shule. Anaishi Collierville, Tennessee, Marekani.**

# Vipi Kuhusu Paulo na Siku ya Sabato?

Russell G, Bell

**Swali**: Je, mbona Paulo pamoja na wenzake waliishika Sabato mara kadhaa? Na mambo haya yakiwa yameandikwa katika Agano Jipya, je tunapaswa kuishika Sabato pia?

**Jibu**: Kuna baadhi ya vifungu katika Agano Jipya ambavyo vinazungumzia kuhusu Paulo akiwa na wenzake waliofanya kazi ya kuhubiri pamoja wakihudhuria mikutano siku ya Sabato (angalia Matendo [17]:1-4). Swali ni, "Kwa nini walikuwa wakiingia katika mikutano?"

Mazingira kwa ufupi ni muhimu hapa. Mtume Paulo alikuwa Myahudi mcha Mungu mtesi wa kanisa la Kristo hadi hapo alipokutana na Yesu Kristo akiwa njiani kwenda Dameski. Tangu wakati huo na kuendelea, alizunguka akimhubiri Yesu Kristo kama mwana wa Mungu. Kitabu cha Matendo kuanzia sura ya 13-18 ni rekodi ya kazi ya Paulo akimuhubiri Kristo ulimwenguni kote.

Angalia kwanza kabisa Paulo alikuwa akiwatafuta watu ambao walipendezwa na Mungu wa kweli; hivyo ni dhahiri, aliingia katika masinagogi ya Kiyahudi siku ya Sabato mahali ambapo watu walikusanyika ili kumwabudu Mungu.

Ilikuwepo sababu nyingine. Ilikuwa ni desturi kwa nyakati hizo kwamba ikiwa mgeni, ambaye ni Myahudi alionekana katika sinagogi akiabudu, baada ya kusoma Torati na manabii (Agano la Kale), kiongozi wa sinagogi angemwomba mgeni kama alikuwa na mawaidha yoyote. Bila shaka, Paulo kila mara alikuwa na jambo la kusema. Mara zote alihubiri habari za Kristo na mapenzi yake, Agano Jipya.

Kama utayachunguza mazingira ya sura ya 13 ya kitabu cha Matendo na sura zinazoendelea, utaona kwamba Paulo na wenzake waliteswa na kufukuzwa mji hata mji kwa sababu ya wivu wa Wayahudi. Kwa nini? Kwa sababu Paulo aliwafundisha kwamba sheria ya kale (Agano la Kale) ilibatilika na sasa walitakiwa kulifuata Agano Jipya la Yesu Kristo. Hili ni pamoja na mabadiliko ya siku ya ibada. Ni sahihi hili kutokana na Matendo 20:6-7, panaposema, *"Sisi tukatweka*

*baada ya siku za mikate isiyotiwa chachu, tukatoka Filipi, tukawafikia Troa, safari ya siku tano, tukakaa huko siku saba. Hata siku ya kwanza ya juma tulipokuwa tumekutana ili kumega mkate, Paulo akawahutubu, akiazimu kusafiri siku ya pili yake, naye akafuliza maneno yake hata usiku wa manane."*

Angalia, Paulo na wenzake walikaa huko Troa siku saba, na hakuna jambo lililokuwa likiendelea siku ya Sabato. Lakini, Jumapili, siku ya kwanza ya juma, Wakristo walikusanyika kushiriki Chakula cha Bwana na kusikiliza mahubiri ya Paulo – sawa na shughuli za ibada zinazofanyika leo hii siku ya kwanza ya juma.

Ebu na tuhitimishe kwa 1 Wakorintho 9:20, ambapo panasema: "***Nalikuwa kama Myahudi kwa Wayahudi, ili niwapate Wayahudi: kwa wale walio chini ya sheria, nalikuwa kama chini ya sheria ingawa mimi mwenyewe si chini ya sheria, ili niwapate walio chini ya sheria***."

**Russell G. Bell anaishi Topeka, Kansas, Marekani na anajihusisha na kazi ya umisheni huko India**

## Ibada za Siku Hizi, Kusifu Kusiko Rasmi?

**Ernest S. Underwood**

Kama ungetakiwa kufika mbele ya Malkia wa Uingereza au kiongozi yeyote mkuu duniani, je, ungevaa kofia ya michezo, suruali ya jinsi na kandambili? Baadhi wanaweza kusema "ndiyo" isipokuwa walio wengi wangejitokeza kwa heshima zaidi kuliko kufanya hivyo. Si muda mrefu uliopita nilikuwa nikiendesha gari pembezoni mwa jengo la kanisa lililokuwa na kibao chenye maandishi yaliyosomeka, "Ibada za Siku Hizi, Kusifu Kusiko Rasmi." Hapo palikuwa na watu waliojitanabaisha kukosa heshima na kicho kwa Mungu. Hakuna mahali popote katika Maandiko Matakatifu mtu yeyote "hakuwa rasmi" katika ibada ya Mwenyenzi, Mwumbaji, Mtawala wa ulimwengu – Mungu mwenye nguvu zote. Daima pamekuwepo na utaratibu wa heshima na taadhima.

Mwandishi wa nyimbo wa kale alilibaini hili. Soma maneno ya "Ngome Imara Ndiye Mungu wetu" yaliyoandikwa na Martin Luther akiwa amependezwa mno na sifa na kicho za wimbo zikielekezwa kwa Mungu.

Rafiki zangu, Mungu si mtani wetu! Yeye ndiye Muumba, anayeushikilia uhai wetu na ni Mwokozi wetu! Habakuki alisema, "Lakini Bwana yumo ndani ya hekalu lake takatifu: dunia yote na inyamaze kimya mbele zake." Hao katika Ufunuo waliimba, "***Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu***." Hapakuwepo na uimbaji usio na utaratibu hapo. Je, wewe unaabudu namna gani?

# Ibada ya Kweli ni Ipi?

Ken Tyler

Yesu alisema katika Yohana 4:23-24, ***"Lakini saa inakuja, nayo sasa ipo, ambayo waabuduo halisi watamwabudu Baba katika Roho na Kweli. Kwa maana Baba awatafuta watu kama hao wamwabudu. Mungu ni roho, nao wamwabuduo yeye imewapasa kumwabudu katika Roho na Kweli."*** *Katika kifungu hiki, Yesu anatoa sifa mbili za ibada ya kweli:*

1. **Katika roho (usafi toka moyoni)**
2. **Katika kweli (kulingana na maelekezo ya Mungu, Yohana 17:17).**

Ningependa kusisitiza kwamba Yesu alisema ibada yetu lazima iwe "***katika roho na kweli***." Hapo tu ndipo tutakuwa waabuduo halisi. Kulingana na mafundisho ya Agano Jipya, ibada ya kweli ya Jumapili, siku ya kwanza ya juma, kuna kushiriki Chakula cha Bwana, (Mathayo 26:26-29; Matendo 20:7; Matendo 2:42), mahubiri (Matendo 20:7), kusali (Matendo 2:42); kutoa (1 Wakorintho 16:1-2) na kuimba (1 Wakorintho 14:15; Waefeso 5:19). Tafadhali zingatia kwamba hapakuwa na piano, chombo au aina yoyote ya ala za muziki iliyotumika katika ibada ya kanisa la karne ya kwanza.

Vilevile Agano Jipya linataja habari za ibada ya bure (Wakolosai 2:20-23). Hatupendi kuiona ibada yetu inafanana na mojawapo ya hizi za bure.

Lazima tuzoeleee kufanya ibada ya kweli. Hii ndiyo ibada pekee inayompendeza Mungu.

**Ken Tyler ni mhubiri wa Injili akifanya kazi na kanisa la Kristo huko Arab, Alabama, Marekani.**

# Mwanzo wa Kuandika Hotuba

Mark N. Posey

**Hotuba:** Vitu vyote Vipya!
**Kifungu:** 2 Petro 3:10-13

1. Kuna Kiumbe Kipya (2 Wakorintho 5:17).
2. Kuna Upya wa Uzima (Warumi 6:4).
3. Kuna Agano Jipya (Mathayo 26:28).
4. Kuna Amri Mpya (Yohana 13:34).
5. Kuna Utu Mpya (Waefeso 4:24).

**Hitimisho:** Mtu "anapozaliwa upya" (Yohana 3:3) ni Kiumbe Kipya.

**Hotuba:** Njoo Ushiriki Raha Pamoja Nasi!
**Kifungu:** 2 Wathesalonike 1:7, "Raha pamoja nasi."

1. Mungu Alipumzika Kiku ya Saba (Mwanzo 2:2).
2. Wayahudi Walipumzika Siku ya Sabato (Kutoka 20:10).
3. Waisraeli Walipumzika Kanaani (Yoshua 1:13).
4. Wenye Dhambi Hupumzika Wanapomwendea Yesu (Mathayo 11:28-30).
5. Waliookolewa Watapumzika Mbinguni (Waebrania 4:9-11; Ufunuo 14:13).

**Hitimisho:** Mtu atakayeingia katika raha ya milele, ni lazima aingie katika raha hii hapa duniani (Mathayo 11:28).

**Hotuba:** Hakika Mbingu ina Thamani Kuliko Vyote!
**Kifungu:** Wafilipi 1:23; 2 Petro 3:13 "mbingu mpya na nchi mpya"

1. Mbinguni Kutakuwa na Raha Mpya (Waebrania 4:9)

2. Mbinguni Kutakuwa na Uhusiano Mpya (1 Wathesalonike 4:17).
3. Mbinguni Kutakuwa na Thawabu Mpya (Mathayo 5:12).

**Hitimisho:** Je, Mbinguni Kutakuwa Ndio Makazi Yako Mapya?

**Hotuba:** Mungu Wetu, Yu Hai!
**Kifungu:** Zaburi 91:1-2
**Utangulizi:** Mtumaini Bwana kwa nguvu zako zote!

1. Mungu ni ELYON (91:1): (Aliye Juu sana)
2. Mungu ni ELSHADAI (91:1): "Mwenyezi."
3. Mungu ni YAHWEH (91:2): "BWANA."
4. Mungu ni ELOHIM (9:2): "Mungu wangu."

**Hitimisho:** Mtumaini Mungu (mstari wa 2): "***Kimbilio langu na ngome yangu, Mungu wangu nitakayemtumaini***!"

**Hotuba:** Mabadiliko Makubwa Kwa Mwendawazimu
**Kifungu:** Marko 5:14-20

1. Yesu alimbadilisha; Yesu alimtoa pepo wabaya waliomtesa.
2. Yesu amlimvisha; hakuendelea kuwa uchi tena bali alivikwa mavazi.
3. Yesu alimtuliza; sasa alikuwa na akili zake.
4. Yesu alimpatia jukumu; Yesu alimtuma kwa marafiki na majirani zake.
5. Yesu alimwagiza; Yesu alimpatia ujumbe wa kupeleka kwa watu.

**Hotuba:** Siku Zote Wakristo Wamejaa Tele!
**Kifungu:** 2 Petro 1:8.

1. Wana Imani Nyingi (2 Wakorintho 8:7).
2. Wanazidi Sana Kuwa na Tumaini (Warumi 15:13).
3. Wamejaa Upendo Mwingi (Wafilipi 1:9).
4. Wanazidi Kutenda Matendo Mema (2 Wakorintho 9:8).

5. Wanazidi Kutenda Kazi ya Bwana (1Wakorintho 15:58).

**Hotuba:** Mungu ANAWEZA!
**Kifungu:** Waefeso 3:20
1. UTAJIRI wa Mungu haupimiki (Waefeso 3:8).
2. FURAHA ya Mungu haielezeki (1 Petro 1:8).
3. AMANI ya Mungu inapita akili zote (Wafilipi 4:7).
4. UPENDO wa Mungu umepita ufahamu (Waefeso 3:19).
5. NJIA za Mungu hazichunguziki (Warumi 11:33).

**Hotuba:** Ngazi Tatu za Utoaji!
**Kifungu:** 1 Wakorintho 16:1-4
1. Ninalazimika Kutoa – SHERIA
2. Ninahitajika Kutoa – WAJIBU
3. Ninataka Kutoa – UPENDO

**Hitimisho:** Kutoa kwa upendo ni kutoa kwa moyo.

**Hotuba:** Kristo Aliyevaa Mwili!
**Kifungu:** 2 Wakorintho 8:9, "Kwa kuwa mmejua neema ya Bwana wetu Yesu Kristo."
1. Bwana –Utambulisho wa Uungu wake.
2. Yesu – Utambulisho wa ubinadamu wake.
3. Kristo – Utambulisho wa Utume wa Kimungu.

**Hitimisho:** Mungu na ashukuriwe kwa ajili ya Kristo (2 Wakorintho 9:15).

**Hotuba:** Mambo Ambayo Filipo Alihubiri!
**Kifungu:** Matendo 8:12, "***Lakini walipomwamini Filipo, akizihubiri habari njema za ufalme wa Mungu, na jina lake Yesu Kristo, wakabatizwa wanaume na wanawake.***"
1. KANISA: Filipo alihubiri "***ufalme wa Mungu***" (linga. Matendo 2:47).
2. MAMLAKA: Filipo alihubiri "***Jina la Yesu Kristo***" (linga. Wafilipi 2:9-11).

3. WOKOVU: Filipo alihubiri "***ubatizo***" (linga. Matendo 2:38; 22:16).

**Hitimisho**: Matendo 8:13, "***Na yeye Simoni mwenyewe aliamini akabatizwa, akashikamana na Filipo; akashangaa alipoziona ishara na miujiza mikubwa inayotendeka.***"

**Hotuba**: Kristo Katika Vipimo Vinne: Tunamwona Yesu!

**Kifungu**: Waebrania 2:9

1. Tunamwona Kristo kama Mwana wa Mungu (Yohana 1:49; 20:31).
2. Tunamwona Kristo kama Mwana wa Adamu (Luka 9:22; 19:10).
3. Tunamwona Kristo kama Dhabihu kwa ajili ya Dhambi (Waebrania 9:22; 10:12).
4. Tunamwona Kristo kama Mwokozi kwa Wakosaji (1 Timotheo 1:15; Warumi 5:8).

**Mark N. Posey ni mhubiri wa kanisa la Kristo Austinville huko Decatur, Alabama, Marekani.**

## Je, Unajua?

**Elimu ya mambo ya kale (Archaeology) inathibitisha ukweli wa habari za kibiblia kuhusiana na kuta za Yeriko kuangukia upande wa nje (Yoshua 6:1-21).**

# KIANGAZI (KARIBIA) KIISHE

Patrick Morrison

Hapo kale, siku za Yeremia, watu wa Mungu katika Yuda walizidi kuasi na kutotii. Mbali ya maonyo na kutoa maelezo mengi, Yuda ilizidi kudidimia hata hatua ya kutoamini hivyo basi wangelipwa kwa maasi yao. Yehova aliitumia Babeli kama fimbo ya hukumu ya Mungu ili kuwafanya watu wake waone umhimu wa kutubu. Nebukadneza aliuzingira mji wa Yerusalemu kwa zaidi ya miaka miwili. Ni katika kipindi hicho cha kuzingirwa wana wa Yuda waliomboleza, *"**Mavuno yamepita, wakati wa hari umekwisha, wala sisi hatukuokoka**"* (Yeremia 8:20). Hawakuwa tayari kuwajibika kutokana na makosa yao, na walikuwa wakimtafuta Mungu awaokoe wakati wote mbali ya kutokuwa tayari kuvunjika mioyo yao na kutubu.

Majira ya joto yaliwasili na kutoweka, na walikuwa bado wamezingirwa na adui. Kipindi kingine cha joto kikawasili walakini bado hali yao ilikuwa ile ile. Walidhani kuwa Mungu aliwaacha, lakini walichoshindwa kuelewa ni kwamba wao ndio walimwacha yeye kitambo, na sasa walikuwa wakiyakabili madhara ya ukafiri wao. Yuda ikazidi kuhoji na kusema, *"**Je! Hapana zeri katika Gileadi? Huko hakuna tabibu? Mbona basi haijarejea afya ya binti ya watu wangu**?"* (Yeremia 8:22). Ilikuwepo zeri kwa ajili ya dhiki zao, na alikuwepo Tabibu Mkuu ambaye angewatibu kwa dawa, lakini hawakumrudia ili waweze kutibiwa. Hivyo, majira ya joto yakapita, na bado walikuwa hawajaokolewa.

Ni wengi leo hii ambao wanapuuza maelezo na maonyo ya Maandiko ambayo huwasihi watubu na kumrudia Mungu. Halafu, shida zinapotokea, wanashikwa na bubuazi na kuuliza Yehova yupo wapi na kwa nini hawaokoi katika dhiki walizojiletea wenyewe. Jamii zetu zimedhamiria kutoa lawama lakini kukwepa majukumu. Lazima tukumbuke kuwa tutavuna matokeo ya kile tulichopanda (Wagalatia 6:7). Wengi wanapenda kudharau wingi wa uvumilivu wa Mungu, bila kujua kuwa uvumilivu wake siku moja utafika mwisho. Uvumilivu wa Mungu unapaswa utuvute tupate kutubu (Warumi 2:4), lakini kwa

wengi ni kibali cha kuendelea na dhambi. Kama Yuda ya kale, wapo ambao wanataka kumtwisha Mungu majukumu. Ukombozi unapatika unaotutoa katika utumwa wa dhambi kwa njia ya damu ya Yesu (Warumi 6:16-18), lakini watu wengi hawataki kumgeukia Tabibu Mkuu ili wapate tiba wanayohitaji pia ambayo wanaitamani. Kundi kubwa la wanadamu hugalagala katika dimbwi la dhambi zao, lakini mpiga mbiu anapopiga, wanataka mtu mwingine alipie gharama. Yesu anaonyesha kulipa gharama ya dhambi zetu (1 Petro 1:18-19), lakini mwanadamu lazima akubali kwa njia ya kutii imani ili apate wokovu (Waefeso 2:8).

Mungu hakuwasahau watu wake. Ingawa waliasi na kutotii, na ingawa walipaswa kuteseka kutokana na dhambi zao, bado Mungu aliwapenda na alitaka kuwaponya. Hukumu ya muda isingeweza kuepukika, lakini hukumu ya milele ambayo wangeipata kwa kuendelea kuasi na kutokutii, ingeepukika ikiwa wangemgeukia yeye. Tunapokuwa tumekabiliwa na madhara ya dhambi ya muda mfupi, hiyo isiwe sababu ya kumshutumu Mungu kwamba ametuacha au hatupendi. Watakaoigeuza mioyo yao kumwelekea yeye wataokolewa na adhabu ya milele. Mungu anatamani kuwaokoa watu wote katika maumivu ya dhambi (1 Timotheo 2:4; 2 Petro 3:9), lakini lazima tutumie fursa tunazojaliwa kumkaribia yeye. Usiku unakuja ghafla (Yohana 9:4). Majira ya joto yanafikia mwisho. Je umeokoka?

**Patrick Morrison ni mhubiri wa wa kanisa la Kristo Sixth Avenue huko Jasper, Alabama, Marekani.**



# Sarafu za Kenny

"(Yesu) *kwa kuwa ni mng'ao wa utukufu wake na chapa ya nafsi yake, akivichukua vyote kwa amri ya uweza wake, akiisha kufanya utakaso wa dhambi, aliketi mkono wa kuume wa Ukuu huko juu"* (Waebrania 1:3).

Neno "mng'ao" lina wazo la miale inayoangaza, kama ile inayotoka kwenye jua. Kama ilivyo hakuna miale bila jua au jua bila miale, vivyo hivyo hakuna Mwana bila Baba au Baba bila Mwana. Nafsi zote hizi mbili ni za milele na ni Mungu!

**David R. Kenney ni mhubiri wa kanisa la Kristo Wadsworth, Ohio, USA.**

# Imani ya Mabaki

Rebeca Rushmore

Sura ya kumi na moja ya Waebrania inafahamika vema kwa mjadala juu ya imani. Mstari wa kwanza wa sura hii muhimu unasomeka, ***"Basi Imani ni kuwa na hakika ya mambo yatarajiwayo, ni bayana ya mambo yasiyoonekana."*** Neno "Imani" linaelezea msimamo wetu katika ukweli wa neno la Mungu. Imani hii inazaliwa ndani yetu tunapolisikia neno la Mungu (Warumi 10:17). Watumishi wengi waaminifu kwa Mungu wametajwa katika Waebrania 11 kama mifano kwa Mkristo.

Tafakari kwa muda mfupi mfano mwingine wa imani unaopatikana katika kitabu cha Ezra. Watu wa Babeli waliitwaa Yuda kama adhabu ya Mungu kwa sababu ya kumkataa Mungu. Yeremia alitabiri kuwa utumwa huo ungedumu kwa miaka sabini (25:12; 29:10) kabla ya masalia kurejea katika nchi ya ahadi (Kumbukumbu 30:1-10). Kama kitabu cha Ezra kinavyoanza, Mfalme Koreshi aliwarejesha Yerusalemu zaidi ya Wayahudi 40,000 halafu wakalijenga upya hekalu na kufanya makaazi katika nchi. Watu wa Mungu walikuwa mbali na nyumbani kwa miaka sabini. Wengi wao walipewa viwanja Yerusalemu hawakuwepo hapo kabla. Hawakuwahi kuona fahari ya hekalu lililojengwa na Sulemani. Lakini, kizazi hicho kipya kilikwenda Yerusalemu kujenga hekalu mahali ambapo wangemwabudu Mungu. "***Kama ilivyoandikwa katika kitabu cha Musa***" (Ezra 6:18). Msingi wa hekalu ulipowekwa, kulikuwa na mwitikio wa aina mbili. Watu wenye umri mkubwa, wale walioliona jengo la kwanza, walilia. Vijana walipiga kelele kwa furaha (3:12).

Makundi yote mawili yalionyesha imani kubwa katika ahadi za Mungu. Kwanza, watu wenye umri mkubwa walionyesha imani yao. Wakati Koreshi alipowaruhusu Wayahudi kurejea Yerusalemu, hakuchagua nani wa kwenda. Isipokuwa, mfalme aliwataka waondoke kwa hiari (Ezra 1:3). Kizazi chenye umri mkubwa walitambua Mungu aliuruhusu utumwa na uhamisho wao. Kundi hili lilielewa, kupitia ujumbe wa manabii na kumbukumbu za maneno ya Musa, kwamba kurudi kwao nyumbani kulitegema kumgeukia Mungu na kumtii. Je,

kama wangelimtilia mashaka Mungu mabaki hao wangerejea Yerusalemu, mbona walirejea kwa hiari? Hakika walikuwa na imani kwamba Mungu angefanya kama alivyosema. Imani na msimamo wao katika neno la Mungu, viliwaongoza kufika nyumbani Yerusalemu.

Pili, kizazi kipya kilidhihirisha imani yao. Kundi hili pia lilijua habari za ujumbe wa manabii na maneno ya Musa. Inawezekana walisikia habari juu ya fahari za Hekalu la Sulemani na maisha katika Nchi ya Ahadi kutoka kwa kizazi cha zamani (Kumbukumbu 6:1-7). Kutokana na elimu hiyo kundi hili pia lilijitolea kurejea Yerusalemu na kujenga tena hekalu la Mungu, ingawa hawakuwahi kuliona lile hekalu zuri, wala kumwabudu Mungu kwa kutoa dhabihu "***kama ilivyoandikwa katika sheria ya Musa***" (Ezra 3:2), kizazi hiki pia cha vijana kilikuwa na imani kuwa Mungu angefanya kama alivyosema. Imani yao, msimamo katika kweli ya Mungu, viliwaongoza kufika katika makazi mapya huko Yerusalemu.

Kama Wakristo, tunatazamia pia makao katika "Yerusalemu mpya"(Ufunuo 21:2). Tunatarajia – ngojea – kuishi milele mbinguni mahali Mungu amewaahidi watoto wake waaminifu (Mathayo25:31-46; 2 Timotheo 4:8; Ufunuo 2:10), hata ingawa hatujawahi kupaona mbinguni, tunaposoma maelezo kuhusiana na mbinguni (Yohana 14:1-6; Ufunuo 211) na ahadi za Mungu juu ya mbinguni, imani yetu inatuhakikishia kwamba mbinguni ni mahali halisi ambapo Mungu amewaandalia wafuasi wake waaminifu. Je, una imani ile iliyoonyeshwa na watu 40,000 siku za Ezra? Kama hapana, jifunze neno la Mungu ili uweze kudhihirisha imani muhimu na kuwa yakini, kwa njia ya kuitii injili, siku moja upate makao katika Yerusalemu mpya.

## Rubi za Robison



Mtume Paulo alikamatwa huko Yerusalemu na kufanya kazi akiwa safirini kuelekea mahakama ya Rumi, akiutetea Ukristo hakuwahi kupatikana na hatia kwa madai yoyote, kama ilivyoandikwa katika kitabu cha Matendo. Kadhalika, alilaumiwa mara nyingi kwa uongo. Liwali mmoja wa Rumi alisema kwa sauti kuu, "***Paulo, una wazimu, kusoma kwako kwingi kumekugeuza akili***!" Paulo kwa upole akamjibu, "***Sina wazimu, ee Festo mtukufu, bali nanena maneno ya kweli na ya akili kamili***" (Matendo 26:24-25).

Ukristo, hakika ni dini ya kweli na mantiki. Sio dini yenye imani isiyoeleweka. Ushahidi wa imani upo, ingawa watu wengi wanaupinga kwa makusudi. Siku zote watu huwalaumu Wakristo wakiwaita wendawazimu, lakini majibu yanatakiwa kuwa ya upole kila mara tunapowajibu washitaki wetu.